

19 MEI, 2026

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA TATU

Kikao cha Thelathini na Mbili — Tarehe 19 Mei, 2026

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Mwenyekiti (Mhe. Cecilia D. Paresso) Alisoma Dua

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Waheshimiwa Wabunge, karibuni katika Mkutano wetu wa Tatu, Kikao cha Thelathini na Mbili.

Katibu.

NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na: -

NAIBU WAZIRI WA UJENZI:

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

19 MEI, 2026

MHE. CHRISTINA S. MNDEME K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA:

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

MWENYEKITI: Ahsante.

Katibu.

NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:

MASWALI NA MAJIBU

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tunaanza na maswali, na swali la kwanza linaelekezwa Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, ninamwita Mheshimiwa Hawa Subira Mwaifunga, Mbunge wa Tabora Mjini, aweze kuuliza swali lake. *(Makofi)*

Na. 372

Ujenzi wa Zahanati Zugumlole

MHE. HAWA S. MWAIFUNGA aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga zahanati Kijiji cha Zugumlole itakayohudumia Vitongoji vya Kaung'ando, Ibaso "A" na "B", Mkombozi, Ulinda na Ndevelwa?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa

19 MEI, 2026

Hawa Subira Mwaifunga, Mbunge wa Jimbo la Tabora Mjini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kijiji cha Zugumlole kipo katika Kata ya Ndevelwa, Halmashauri ya Manispaa ya Tabora. Kijiji hicho kina jumla ya wakazi 1,989, kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022. Kwa sasa wananchi wa Kijiji cha Zugumlole wanapata huduma katika Zahanati ya Ndevelwa iliyopo kilometa 25 kutoka kijijini hapo. Aidha, kwa upande wa huduma za upasuaji wanahudumiwa kwenye Hospitali ya Halmashauri ya Manispaa ya Tabora iliyopo kilometa 42.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutoka na umuhimu wa kuwepo kwa zahanati katika Kijiji cha Zugumlole, Serikali ya Wilaya ya Tabora ilifika na kuzungumza na wananchi wa Kijiji cha Zugumlole na kuhamasisha wananchi ili waanze ujenzi wa boma la zahanati na Serikali itatoa fedha za kukamilisha boma kadri utaratibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kutoa fedha kwa ajili ya ukamilishaji wa maboma ya zahanati yaliyoanzishwa kwa nguvu za wananchi kote nchini kwa awamu. Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Hawa Subira Mwaifunga, swali la nyongeza.

MHE. HAWA S. MWAIFUNGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu ya Serikali, Kata ya Ndevelwa ina wananchi zaidi ya 11,000 kwa mujibu wa sensa, kijiji hiki mpaka kufika kwenye Zahanati ya Ndevelwa ni zaidi ya kilometa 25 kama majibu ya msingi yalivyoeleza. Kumekuwa na changamoto kubwa sana na hususani kwa akina mama wajawazito wanapokwenda kujifungua, barabara ni mbovu lakini pia kufika kwenye zahanati ni shughuli.

Je, Serikali haioni sasa umefika wakati wa kuharakisha ujenzi wa zahanati hii ili wananchi wa Kijiji za Zugumlole, Shaurimoyo na Inala waweze kupata huduma za afya kwenye eneo la karibu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili, je, Serikali haioni sasa umefika wakati wa kupandisha hadhi Zahanati ya Ndevelwa

19 MEI, 2026

ambayo inahudumia zaidi ya vijiji sita ili iweze kuwa kituo cha afya?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, kwanza, nimpongeze sana dada yangu Mheshimiwa Hawa Subira Mwaifunga, Mbunge wa Jimbo la Tabora Mjini kwa namna ambavyo anafanya kazi kubwa ya kuwasemea na kufuatilia maendeleo ya Wananchi wa Tabora Mjini na sisi tukuhakikishie kwamba Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI tutaendelea kukupa ushirikiano kuhakikisha wananchi wa Tabora wananufaika na matunda ya Serikali yao sikivu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba umbali kutoka Zahanati ya Zugumlole mpaka kituo cha afya na hospitali ya halmashauri ni mkubwa na ndio maana Serikali tumeona umuhimu wa kuanza ujenzi wa zahanati katika Kijiji cha Zugumlole, na tayari Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya na Serikali ya Wilaya ilifika na kuongea na wananchi na kuwahamasisha wananchi ili waanze kwa utaratibu wetu wa mpango wa maendeleo ya afya msingi, waandae eneo la ujenzi wa zahanati, waanze hatua za awali za ujenzi wa boma na Serikali yetu itaweka mpango wa fedha kwa ajili ya kwenda kukamilisha ujenzi wa zahanati hiyo.

Kwa hiyo, nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali itashirikiana na wananchi na Serikali za Mkoa wa Tabora na Halmashauri ya Tabora kuhakikisha Zahanati ya Zugumlole inajengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, ni kweli tumekuwa na kata ambazo zina idadi kubwa ya wananchi kama ambavyo Kata hii ya Ndevelwa ina idadi kubwa ya wananchi, lakini umbali mkubwa kwenda hospitali ya halmashauri. Tayari tumeshaweka utaratibu kwamba zahanati ambazo zina sifa ya kupandishwa hadhi kuwa vituo vya afya, Mkurugenzi wa Halmashauri alete maombi rasmi Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, tutatuma wataalam, watafanya tathmini na ikiwa vigezo vitaafikiwa tutahakikisha kwamba tunaweka utaratibu wa kujenga kituo cha

19 MEI, 2026

afya. Kwa hiyo, nikuombe Mheshimiwa Mbunge na nitumie nafasi hii kumsisitiza Mkurugenzi wa Manispaa ya Tabora kufuata utaratibu huo ili Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI iendelee na hatua zinazofuata.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mariam Kisangi.

MHE. MARIAM N. KISANGI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mitaa ya Temeke iliyoko katika Kata ya Temeke, Jimbo la Temeke haina kabisa zahanati wala kituo cha afya na hawawezi kutibiwa kwa urahisi katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa. Je, Serikali haioni haja ya kujenga zahanati katika Kata ya Temeke?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, Serikali iliweka mpango wa ujenzi wa zahanati katika vijiji na mitaa, lakini pia katika kata za kimkakati ujenzi wa vituo vya afya.

Ninaomba nikuhakikishie Mheshimiwa Mariam Kisangi kwamba Serikali inaendelea na utaratibu wa kuainisha maeneo ya kimkakati kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya afya, lakini pia mitaa ile yenye sifa kwa ajili ya ujenzi wa zahanati na tutahakikisha kwenye mipango yetu tunaweka kipaumbele Jimbo la Temeke kupata huduma ya zahanati na vituo vya afya.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Sikudhani Chikambo.

MHE. SIKUDHANI Y. CHIKAMBO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, tunafahamu kwamba viko vijiji mpaka leo havina zahanati, lakini kuna vijiji vingine wananchi wameamua kukusanya nguvu na kuanza ujenzi kikiwemo Kijiji cha Sisi kwa Sisi na tayari wamejenga boma wamefikia hatua ya lenta.

19 MEI, 2026

Ni nini kauli ya Serikali katika kuhakikisha nguvu za wananchi haziendi bure na wanapata zahanati kwenye kile kijiji? Ahsante.

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, katika kipindi cha miaka mitano iliyopita mwaka wa fedha 2021/2022 mpaka sasa Serikali imepeleka zaidi ya shilingi 40,000,000,000 katika halmashauri zetu na katika vijiji vyetu kwa ajili ya ujenzi wa maboma ya zahanati na hasa kumaliza maboma ambayo wananchi wameanza ujenzi kwa nguvu zao na kufikia hatua za lenta. Serikali ilikuwa inatoa shilingi 50,000,000 kila boma na maboma zaidi ya 3,500 yamekamilishwa.

Kwa hiyo, ninaomba nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inaendelea na utaratibu wake kila mwaka wa bajeti tunaendelea kutenga fedha, kuhakikisha kwamba tunakamilisha maboma ya zahanati yaliyoanzishwa kwa nguvu za wananchi yakiwemo maboma katika Wilaya ya Tunduru.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mwita Waitara, swali dogo la nyongeza.

MHE. MWITA M. WAITARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru, kituo cha afya kwa maana ya majengo Bumera, Kwihancha, Magoma, Genkuru vimekamilika pamoja na Mtana. Ni lini sasa huduma itaanza kutolewa katika maeneo hayo? Ahsante.

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli tulifanya ziara mara kadhaa na Mheshimiwa Waitara katika Jimbo la Tarime Vijijini na tulikwenda moja ya vituo vya afya kikiwepo cha Magoma pamoja na Kwihancha, na tuliona kazi kubwa iliyofanywa na Serikali kupeleka fedha kuhakikisha majengo yanakamilika.

19 MEI, 2026

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge, tulianza na awamu ya kwanza ya ujenzi wa miundombinu, tumekwenda awamu ya pili ya kununua vifaa tiba na ninafahamu Tarime Vijijini na vituo hivyo vimepokea vifaa tiba na tumekwenda awamu ya tatu ya kuajiri watumishi kwa ajili ya kutoa huduma. Nikuhakikishie majengo yote yaliyojengwa yatapewa vifaa tiba stahiki na watumishi wataendelea kuongezwa ili kuhakikisha kwamba vituo hivyo vinatoa huduma stahiki. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Selemani Kakoso.

MHE. MOSHI S. KAKOSO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, Kijiji cha Kamsanga ni kijiji ambacho kimejenga zahanati kwa kutumia nguvu za wananchi, zahanati nzuri na ya kisasa na ina zaidi ya watu 25,000. Ni lini zahanati hii mnaipandisha hadhi ili kiwe kituo cha afya?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo yote ambayo yana zahanati, lakini idadi kubwa ya wananchi zaidi ya 15,000 sera yetu ya afya inaelekeza kuwa na vituo vya afya. Kwa hiyo, eneo hilo la Zahanati ya Kamsanga ambayo ina idadi ya wananchi zaidi ya 25,000 ina sifa ya kuwa na kituo cha afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu wetu ni kwamba halmashauri wanaainisha kama eneo hilo lina ukubwa unaotosheleza kujenga kituo cha afya, lakini pili wanapeleka maombi yao Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI ili tathmini ifanyike na iweze kuingizwa kwenye mpango kwa ajili ya ujenzi.

Kwa hiyo, ninaomba nikuhakikishie Mheshimiwa Kakoso, sisi tutawasiliana na Halmashauri ya Tanganyika ili tuweze kuweka utaratibu wa kupata taarifa kwa ajili ya kufanya tathmini na kuweka kwenye mipango yetu kwa ajili ya kupandisha hadhi zahanati hiyo kuwa kituo cha afya.

19 MEI, 2026

MWENYEKITI: Mheshimiwa Anne Kilango Malecela.

MHE. ANNE K. MALECELA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kata ya Kalemawe ni kata ambayo iko pembezoni sana na imesimama yenyewe sehemu za ziwani. Wakati wa kampeni kata hii tuli ahidi na ilia hidiwa kwamba itajengewa kituo cha afya na Mkurugenzi wa Wilaya ya Same akalisimamia hili. Je, Serikali mnasemaje kuhusu ujenzi wa kituo cha afya kwenye Kata ya Kalemawe?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, ni dhamira ya Serikali kusogeza huduma za afya karibu na wananchi na hususani vituo vya afya ili kupata huduma za dharura za upasuaji kwa akina mama wajawazito, lakini na wananchi wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo hili suala la muhimu ni kufanya tathmini ya vigezo, kwanza idadi ya wananchi katika kata husika, lakini pili ni umbali wa kutoka kituo cha jirani zaidi na kinachotoa huduma za upasuaji, lakini tatu upatikanaji wa eneo linalotosheleza mahitaji ya kituo cha afya.

Kwa hiyo, ninaomba nikuhakikishie Mheshimiwa mama yangu Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, kwamba tutafanya tathmini na nitumia nafasi hii kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, kumwelekeza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Same kuwasilisha taarifa hiyo na kuchanganua ikiwa vigezo vinafikiwa ili Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI tuone namna ya kuanza kutenga bajeti ili tuanze ujenzi wa kituo hicho ikiwa vigezo vitafikiwa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Agnesta Lambert, swali dogo la nyongeza

MHE. AGNESTA L. KAIZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kuniona.

19 MEI, 2026

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kata ya Minazi Mirefu iliyoko ndani ya Jimbo la Segerea yenye wakazi 31,000 haina zahanati wala haina kituo cha afya, lakini eneo la kujenga kituo cha afya lipo. Mheshimiwa Naibu Waziri ningepomba kufahamu, nini kauli ya Serikali kwa ajili ya wakazi wa Minazi Mirefu kwa ajili ya wao kupata kituo cha afya? Ahsante.

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa vituo vya afya kwa mujibu wa mwongozo wa mpango wa maendeleo ya afya msingi ni kuendana na kata za kimkakati, na kwa aina ya *setup* ya Dar es Salaam yako maeneo ambayo yana idadi kubwa sana ya wananchi, lakini yako jirani na hospitali au vituo vya afya vingine na wanapata huduma katika maeneo hayo, lakini kuna maeneo mengine kata ziko mbali na zinahitaji ujenzi wa vituo vya afya.

Kwa hiyo, ninaomba nikuhakikishie Mheshimiwa Agneta Lambert, Kata hiyo ya Minazi Mirefu tutaifanyia tathmini na kuona kama iko mbali zaidi na vituo vya afya vya jirani tuweze kufanya mipango kwa ajili ya ujenzi.

MWENYEKITI: Waheshimiwa tunaendelea, sasa ninamwita Mheshimiwa Devotha Daniel, Mbunge wa Viti Maalum, aweze kuuliza swali lake.

Na. 373

Ushirikishwaji wa Wabunge wa Viti Maalum katika Mikopo ya 10% kwenye Halmashauri

MHE. DEVOTHA D. MBURARUGABA aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani kuhakikisha Wabunge wa Viti Maalum wanashirikishwa katika utoaji wa mikopo ya 10% kwenye halmashauri?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

19 MEI, 2026

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Devotha Daniel Mburarugaba, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatatanmbua umuhimu wa kuwashirikisha Waheshimiwa Wabunge wote wakiwemo wa Viti Maalum, katika utoaji na usimamizi wa mikopo ya 10% katika halmashauri. Kufuatia maboresho ya sheria, kanuni na mwongozo wa utoaji na usimamizi wa mikopo hiyo wa mwaka 2024, Serikali imeweka utaratibu wa ushirikishwaji wa Waheshimiwa Wabunge kuhusu hatua za utoaji mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, chini ya utaratibu huo, Waheshimiwa Wabunge wanatakiwa washirikishwe kikamilifu kupitia vikao vya kisheria vya halmashauri, hususani Baraza la Madiwani na Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango ambapo hupokea taarifa, kujadili na kutoa maoni kuhusu upangaji, ugawaji na usimamizi wa mikopo ya 10% kwa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.

Aidha, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI imewaelekeza Wakurugenzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa kuwataarifu na kuwaalika Waheshimiwa Wabunge kushiriki kwenye shughuli za utoaji mikopo katika halmshauri zao ili kuwapa fursa ya kuhamasisha, kuelimisha na kufuatilia shughuli za vikundi kutokana na mikopo hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inazisistiza halmashauri zote nchini kuendelea kuimarisha utaratibu wa mawasiliano na kuwapa taarifa kwa wakati Waheshimiwa Wabunge kuhusu ratiba za vikao, orodha ya wanufaika na mwenendo wa urejeshaji wa mikopo ili kuongeza uwazi na uwajibikaji. Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Devotha Daniel, maswali ya nyongeza.

19 MEI, 2026

MHE. DEVOTHA D. MBURARUGABA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa majibu ya Serikali, lakini ningependa kutoa ushauri ufuatao; tunafahamu kabisa kwamba Wabunge hawa ndio wawakilishi wa wananchi ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na hivi hii mikopo imekuwa ikitolewa bila taarifa kwa Wabunge hawa na inaleta changamoto kubwa sana Wabunge wamekuwa wakifika majimboni wanalalamikiwa na wananchi kwa sababu mikopo hii imetolewa, wanashirikishwa pale zinapotokea changamoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe Serikali yako Tukufu waze kuzingatia hili kuwashirikisha Wabunge ili waweze kutatua matatizo ya mikopo hii. Pia nimuombe sana Waziri aweze kufanya *impact analysis* kwa ajili ya mikopo hii ilituweze kufahamu umuhimu wa mikopo hii kwa wananchi. Ninashukuru sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, haya yalikuwa ni maoni, nina imani mtayachukua na kuyafanyia kazi.

Tunaendelea Waheshimiwa, sasa ninamwita Mheshimiwa Dickson Nathan Lutevele, Mbunge wa Mafinga Mjini, aweze kuuliza swali lake.

Na. 374

Ujenzi wa Stand ya Mabasi – Mafinga

MHE. DICKSON N. LUTEVELE aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga *stand* ya kisasa ya mabasi Halmashauri ya Mji wa Mafinga?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa

19 MEI, 2026

Dickson Nathan Lutevele Villa, Mbunge wa Jimbo la Mafinga Mjini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ina mapango wa kujenga *stand* ya kisasa ya mabasi katika Halmashauri ya Mji wa Mafinga katika Kata ya Kinyanambo kupitia Mradi wa Kuboresha Miundombinu ya Miji (*TACTIC*) Awamu ya Tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upembuzi yakinifu na usanifu wa awali ulikamilika mwezi Februari, 2026 na taarifa ilishawasilishwa kwa timu ya uratibu wa miradi ya Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI na Halmashauri ya Mji wa Mafinga. Kwa sasa Mtaalam Mshauri Kampuni ya *Botek Bosphorus Consulting Corporation* kwa kushirikiana na kampuni ya *Building design Authority (P) Ltd* wanaendelea kufanya usanifu wa mwisho ambao unatarajiwa kukamilika mwezi Mei, 2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya usanifu kukamilika, hatua itakayofuata ni kutangaza zabuni kwa ajili ya kupata mkandarasi mjenzi. Pindi taratibu hizo zikikamilika, ujenzi wa *stand* ya mabasi katika mji wa Mafinga utaanza mara moja. Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Dickson Nathan Lutevele, maswali ya nyongeza.

MHE. DICKSON N. LUTEVELE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwanza, naishukuru Serikali kwa majibu yake mazuri, lakini nilikuwa na swali moja tu la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na utaratibu baada ya upembuzi yakinifu kufanyika, kuchelewesha sana mkandarasi kuanza kazi. *Stand* hii, sisi Halmashauri ya Mji wa Mafinga mpaka sasa hatuna *stand*. Pale ambapo mabasi yanasimama ni kandokando ya barabara, eneo ambalo limekuwa na ajali nyingi sana, lakini kwa sisi Wana-Mafinga pia, *stand* hii tunaisubiri kama moja kati ya vyanzo vya mapato kwa sababu mji wetu una msongamano mkubwa sana wa magari, lakini hatuna *stand*.

19 MEI, 2026

Je, nini kauli ya Serikali, ni kwa uharaka upi kwenye kuhakikisha kwamba *stand* hii, pindi tu upembuzi utakapokuwa umekamilika, tunapata mkandarasi na *stand* hii inajengwa kwa sababu Wana-Mafinga wameisubiri *stand* hii kwa muda mrefu sana?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, kwanza, nimpongeze sana Mheshimiwa Dickson Nathan Lutevele, Mbunge wa Mafinga Mjini, amefuatilia mara kadhaa kuhakikisha kwamba ujenzi wa *stand* ya kisasa ya mabasi ya mji wa Mafinga inafanyika. Nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Jimbo la Mafinga Mjini kwamba ni dhamira ya Serikali kuhakikisha kwamba *stand* hiyo inajengwa mapema iwezekanavyo na ndiyo maana tayari tumeshafanya hatua za awali za usanifu na upembuzi yakinifu na tuko hatua ya pili ya mtaalamu mshauri ambaye anakamilisha kazi yake mwezi Mei mwaka huu, kwa maana ya mwezi huu mwishoni. Tutahakikisha baada ya ukamilishaji huo, tunaendelea na taratibu zetu za Serikali pamoja na Benki ya Dunia ili kutoa fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi huo.

Kwa hiyo, kauli ya Serikali Mheshimiwa Mbunge ni kwamba dhamira yetu ni kuhakikisha tunaanza ujenzi mapema iwezekanavyo baada ya hatua hizi kukamilika.

MWENYEKITI: Tunaendelea Waheshimiwa. Sasa namwita Mheshimiwa Tarimba Gulam Abbas, Mbunge wa Kinondoni, aweze kuuliza swali lake.

Na. 375

Mgongano wa Vikao vya Bunge na Halmashauri

MHE. TARIMBA G. ABBAS aliuliza: -

19 MEI, 2026

Je, kuna mpango gani wa kuondoa mgongano wa Vikao vya Bunge na Halmashauri za Majiji, Manispaa na Miji ili Wabunge washiriki?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE) alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Tarimba Gulam Abbas, Mbunge wa Jimbo la Kinondoni, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kwenye nyakati tofauti, imekuwa ikitoa maelekezo kwa halmashauri ili kuhakikisha kwa kiwango kikubwa, ratiba za vikao vya halmashauri hazigongani na ratiba za Vikao vya Bunge. Halmashauri zilielekezwa kuzingatia kalenda ya shughuli za Bunge wakati wa kuandaa kalenda zao za vikao vya mwaka husika ili kutoa fursa kwa Wabunge ambao ni wajumbe wa mikutano hiyo, kushiriki kikamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, itaendelea kuzisimamia halmashauri kuhakikisha zinaandaa ratiba ya vikao kwa mwaka 2026/2027 kwa kuzingatia ratiba za vikao vya Bunge kwa kadri itakavyowezekana. Aidha, Wakurugenzi wa Halmashauri zote nchini, wanaelekezwa kuwasiliana na Waheshimiwa Wabunge wakati wa kupanga ratiba za Vikao vya Kamati na Mabaraza ya Madiwani, ili kuona namna viongozi hao wanaweza kushiriki katika vikao hivyo. Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Tarimba Gulam Abbas, maswali ya nyongeza.

MHE. TARIMBA G. ABBAS: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini naomba niseme yafuatayo; kwamba najua halmashauri zinafanya kazi nzuri, Madiwani wanafanya kazi nzuri na hatuna sababu ya kupata mashaka ya kazi zao wanazozifanya, isipokuwa ushiriki wa Wabunge ni

19 MEI, 2026

muhimu kwa sababu utaongeza, nitumie neno la kiingereza *value* katika majadiliano ya vikao vile. *(Makofi)*

Sasa kutokana na ukweli kwamba, hizi juhudi, Mheshimiwa Naibu Waziri anazosisema kwamba Serikali imekuwa ikiagiza, ukweli hazitekelezwi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ushauri wangu, sio ushauri, ni swali je, Serikali iko tayari kupeleka barua, kwa sababu Serikali inaendeshwa kwa barua. Barua mahususi zikieleza kwamba ama vikao vifanyike *weekend* ili Wabunge waweze kwenda au wakubaliane na ratiba za Mbunge bila kuathiri shughuli za halmashauri?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, nichukue nafasi hii nimpongeze sana Mheshimiwa Abbas Tarimba, Mbunge wa Jimbo la Kinondoni, amekuwa msemaji mahiri sana wa wananchi wa Jimbo la Kinondoni, lakini si mara yake ya kwanza kutoa hoja hii ambayo ameuliza leo kuhusiana na Waheshimiwa Wabunge kupata fursa ya kushiriki Vikao vya Mabaraza ya Madiwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na hoja hii imekuwa ni hoja ya miaka mingi ya Waheshimiwa Wabunge. Serikali inatambua umuhimu wa mchango wa Waheshimiwa Wabunge kushiriki kwenye Mabaraza ya Madiwani na Kamati za Kudumu za Halmashauri katika halmashauri zetu. Serikali ilishotoa maelekezo kwa Wakurugenzi wa Halmashauri zote nchini, kwamba kwanza wawasiliane na Waheshimiwa Wabunge ili kukubaliana tarehe za vikao na Waheshimiwa Wabunge wapate fursa ya kushiriki kwenye vikao hivyo na kutoa maoni yao, lakini pia kusimamia shughuli za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba ziko baadhi ya halmashauri ambazo hazijazingatia maelekezo ya Serikali na

19 MEI, 2026

kuendelea na vikao hivyo wakati Waheshimiwa Wabunge wakiwa kwenye majukumu mengine ya kibunge.

Naomba nitumie nafasi hii kwanza, niwaelekeze kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, Wakurugenzi wote wa Halmashauri zetu kote nchini, wahakikishe wanafuata na kusimamia maelekezo ya Serikali kwamba kabla ya kupanga tarehe ya Vikao vya Baraza au Kamati za Madiwani, ni lazima wawasiliane na Wabunge husika, wakubaliane na ikiwezekana Waheshimiwa Wabunge washiriki kwenye vikao hivyo. Vivyo hivyo katika Mabaraza ya Madiwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nitoe angalizo kidogo, kwamba mara nyingine vikao vyetu vya Bunge vinakuwa virefu, kwa mfano Bunge hili la kuanzia Machi mpaka Juni, lakini kwa mujibu wa kanuni na miongozo pia, kuna vikao ambavyo vinatakiwa vifanyike kwenye ngazi za halmashauri kipindi hiki. Kwa hiyo, mara nyingine kuna changamoto za mwingiliano wa majukumu. Kwa mara hizo chache tunaweza tukakubaliana, tukafanya *weekend* au tukaruhusu wenzetu wakaendelea na vikao kwa niaba yetu na tukaenda kupata mrejesho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge tunalitambua suala hili na tuko tayari kuandika barua, maelekezo rasmi kwa Wakurugenzi ili waweze kusimamia utaratibu huu na Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, tutafuatilia utekelezaji wa maelekezo haya. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Isack Joseph, swali la nyongeza.

MHE. ISACK J. COPRIANO: Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili limekuwa likijirudiarudia mara zote na kauli ya Serikali ni hiyo, tunatoa maelekezo kwa wakurugenzi, kwa wakurugenzi. Sasa ni vyema, kama jambo haliwezekani, ni afadhali Mheshimiwa Waziri akatuambia jambo hili haliwezekani ili tusiwe tunauliza jambo mara kwa mara tunaonekana...

Kwa hiyo swali langu ni, je, kwa nini sasa Serikali isiwe na maelekezo mahususi, kama alivyotoa kauli Mheshimiwa Naibu

19 MEI, 2026

Waziri Mkuu na haitekelezwi. Sasa nini kauli ya Serikali juu ya jambo hili? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, kwanza nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Monduli, kaka yangu Kadogoo kwamba kwanza Serikali ilitoa maelekezo na si kwamba hayajatekelezeka. Baadhi ya halmashauri zimeteteleza na baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wamekuwa wakiwasiliana na halmashauri zao na kupanga vikao, na baadhi ya Waheshimiwa Wabunge kwa kiasi kikubwa wamekuwa wakishiriki vikao hivyo. Kwa hiyo, maelekezo yaliyotolewa na Serikali yameendelea kutekelezwa, lakini ufanisi wa utekelezaji wake bado unahitaji kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kauli ya Serikali ni kwamba tutaendelea kusimamia maelekezo ya Serikali na kuhakikisha kwamba Waheshimiwa Wabunge wanashirikishwa, ili waweze kushiriki kwenye vikao hivyo vya Kamati na Mabaraza ya Madiwani, lakini kama ambavyo nilitoa angalizo, viko vipindi ambavyo Waheshimiwa Wabunge wana ratiba ambazo zimebana, lakini kwa mujibu wa kanuni na miongozo ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa, vikao vya Kamati ya Fedha ambavyo vinafanyika kila mwezi, lazima vifanyike ndani ya mwezi. Kila mwezi Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango, kila mwezi lazima vifanyike, mara nyingine Waheshimiwa Wabunge wanakuwa na majukumu mengi.

Kwa hiyo, lazima twende kwa ku-*balance* mazingira haya, kwamba kuna vikao vingine tunaweza tusishiriki, lakini vikao vilivyo vingi tutashiriki. Sisi tutafuatilia halmashauri kuzingatia utaratibu na mwongozo huo. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

19 MEI, 2026

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea, sasa ni Ofisi ya Rais, Maendeleo ya Vijana. Namwita Mheshimiwa Latifa Khamis Juwakali, Mbunge wa Viti Maalum, aweze kuuliza swali lake.

Na. 376

Fursa za Kuwawezesha Vijana

MHE. LATIFA KHAMIS JUWAKALI aliuliza: -

Je, Serikali imejipangaje katika kutafuta fursa za kuwawezesha vijana?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MAENDELEO YA VIJANA alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Latifa Khamis Juwakali, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kutekeleza mikakati mbalimbali ya kuongeza fursa za uwezeshaji wa vijana ikiwemo ajira na kujiajiri, kupitia miradi ya maendeleo, uboreshaji wa mazingira ya biashara na uwekezaji, na kuondoa vikwazo mbalimbali vya kimfumo. Miongoni mwa hatua zinazotekelezwa ni uratibu wa programu za uwezeshaji vijana kupitia Wizara za Kisekta kama vile Kilimo, Mifugo na Uvuvi, Madini, Viwanda na Biashara, Sanaa na Michezo, Teknolojia ya Habari na nyinginezo, sambamba na utoaji wa mikopo yenye masharti nafuu kupitia mfuko wa maendeleo ya vijana, asilimia nne ya mapato ya halmashauri na asilimia kumi ya zabuni za umma kwa vijana kupitia *Public Procurement Regulatory Authority (PPRA)*. Hatua ambazo zimeendelea kuongeza upatikanaji wa mitaji, ajira na fursa za kiuchumi kwa vijana nchini. Aidha, Serikali imeendelea kutafuta na kuratibu fursa za vijana za ajira ndani na nje ya nchi kwa lengo la kuongeza ushiriki wa vijana katika shughuli za kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

19 MEI, 2026

MWENYEKITI: Mheshimiwa Latifa Khamis Juwakali, maswali ya nyongeza.

MHE. LATIFA KHAMIS JUWAKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, nilikuwa na maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza, Mheshimiwa Waziri utaungana na mimi, huwezi kumtaja kijana bila kuigusa Wizara ya Kazi, Ajira na Mahusiano. Nilikuwa nataka kufahamu, Wizara ya Vijana mna ushirikiano gani wa karibu na Wizara hiyo ambayo nimeitaja katika kuzitafuta, kuzitangaza na kuzilinda ajira zote za nje ya nchi na pia kuwasimamia vijana wote ambao wanapata ajira nje ya nchi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili, Mheshimiwa Waziri wewe unafahamu kwamba ajira na fursa nyingi hazipo tu katika Wizara ya Vijana, zipo pia katika Wizara nyingine za kisekta.

Je, Wizara au Serikali kupitia Wizara ya Vijana haioni haja sasa kuanzisha *Youth Desk Officers* katika kila Wizara ili kuona namna gani Wizara ya Vijana inazisimamia fursa zote zinazotoka katika wizara za kisekta? Nakushukuru sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MAENDELEO YA VIJANA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naomba nimpongeze Mheshimiwa Latifa kwa kuwa mstari wa mbele kila wakati kufuatilia masuala yanayohusu vijana na kuongeza tija katika utekelezaji wake, kuhakikisha fursa zinapatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama alivyoeleza, Serikali inafanya kazi kwa muunganiko na sisi kama Wizara ya Maendeleo ya Vijana, tunafanya kazi kwa karibu sana na Wizara ya Kazi, Ajira pamoja na Mahusiano. Ahadi ya Chama Cha Mapinduzi ni kutoa ajira takribani 8,000,000 katika miaka mitano ijayo. Katika hilo, ilielekeza waziwazi kwamba inalenga pia kutafuta ajira nje ya nchi.

19 MEI, 2026

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia Wizara ya Kazi, Ajira na Mahusiano, mikataba mbalimbali imekuwa ikiingiwa kati ya Serikali na nchi mbalimbali. Mpaka sasa kuna vijana 7,593 ambao wameenda katika mataifa mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kuchukua nafasi hii nitoe wito kwamba tumekuwa na changamoto ya vijana kadhaa ambao wamekuwa wakielezea changamoto kuhusiana na mchakato huu. Serikali inaingia mikataba hii kupitia Balozi zetu na Serikali ndiyo *custodian* wa mikataba ya ajira kupitia mawakala wa ajira binafsi ambao wamesajiliwa na Serikali. Mwezi Februari mwaka huu zaidi ya mawakala 148 walifanya kikao na Serikali, katika kuhakikisha kwamba vijana wanatumia utaratibu unaofaa, wakitembelea tovuti ya Serikali wataona mawakala hao ambao wameidhinishwa na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi ya hayo ni kwamba vijana huwa wanapewa taarifa kwa maana ya kupewa mafunzo, wanapopata nafasi ya kwenda nje ya nchi ili kuepusha changamoto ambazo wanakutana nazo. Serikali itaendelea kufanya hivyo ili kuhakikisha fursa nyingi zinaendelea kupatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili Mheshimiwa Latifa, ni kwamba Serikali ina Maafisa Maendeleo ya Vijana wanaopatikana katika halmashauri mbalimbali. Mara tu baada ya kuundwa kwa Wizara hii, mwezi Desemba tulifanya kikao cha pamoja cha uratibu na Maafisa Maendeleo ya Vijana wote wanaopatikana katika halmashauri zetu, nia ikiwa ni pamoja na kuongeza ufanisi katika mfumo. Nimepokea wazo ulilolitoa kuhusiana na *Youth Desk*, na nikuahidi kwamba Serikali italifanyia kazi ili kuhakikisha taarifa zinawafikia vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Mheshimiwa *Engineer* Johnston Mutasingwa, swali la nyongeza.

MHE. ENG. JOHNSTON J. MUTASINGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, tuna vijana wengi sana wamejiajiri hasa upande wa *garage*. Kwa mfano pale Jimbo la Bukoba Mjini, tuna

19 MEI, 2026

vijana zaidi ya 250 wako kwenye *garage* ya Mnyonge, lakini wako barabarani.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuweza kuwatengea maeneo maalumU ya kufanyia shughuli zao hizo za *garage* ili waweze kwanza kuwa na uhakika wa shughuli zao, lakini waweze kuwa na sifa za kupata mikopo ya Serikali? Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MAENDELEO YA VIJANA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa swali la Mheshimiwa Mutasingwa na bahati nzuri nilishafanya ziara katika jimbo lake na nilipita katika maeneo ya *garage* na tulikuwa naye pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kuhakikisha kwamba vijana hawa kwanza tunawarasimisha ili kupata urahisi wa wao kupata fursa ambazo Serikali inazitengeneza. Mpaka sasa kupitia programu ya urasimishaji ambayo inafanyika kupitia VETA, mwaka huu pekee yake malengo ni kurasimisha vijana 14,400. Ninaamini vijana mojawapo watakaopata fursa hii ni vijana wanaopatikana katika jimbo lako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, kupitia TAMISEMI kumekuwa na utaratibu wa kupanga maeneo rasmi kwa ajili ya kuhakikisha kwamba wanapata maeneo ambayo hawatabugudhiwa. Nimhakikishie, Serikali itaendelea kuratibu zoezi hilo na vijana wataendelea kupata nafasi na fursa za kufanya kazi katika maeneo ambayo ni rasmi. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Josephine Kapoma, swali la nyongeza.

MHE. JOSEPHINE J. KAPOMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, vijana wengi wamekuwa wanapata hizi fursa za mikopo na Serikali imejitahidi sana kufungua hizi fursa, lakini tumekuwa na shida kubwa sana kwa vijana kwa sababu wengi hawana nidhamu ya fedha (*finance mistress*), lakini sasa Serikali ina mkakati gani wa kuanzisha Vyama vya Ushirika vya Kuweka na

19 MEI, 2026

Kukopa (SACCOS) ili waweze kujengewa uwezo wa kuwa na nidhamu ya fedha? Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MAENDELEO YA VIJANA:

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, Serikali imeendelea kujitathmini kila wakati kuona namna ambavyo mikopo inayotolewa hasa kwenye kundi la vijana inakuwa na ufanisi. Kama alivyoeleza Mheshimiwa Kapoma, ni kwamba kumekuwa na changamoto kubwa sana hasa katika urejeshaji, kwa mfano tukiangalia Mfuko wa Maendeleo wa Vijana, zaidi ya shilingi bilioni 3.9 zimeshindwa kurejeshwa. Tumefanya tathmini kuangalia changamoto ni nini, ikiwepo pia na asilimia nne zinazotolewa kupitia halmashauri zetu. Moja ya changamoto tuliyoiona, ni elimu ya kifedha na ndiyo maana kupitia awamu hii ya mikopo tuliyoitoa, tumeingia utaratibu wa makubaliano rasmi na taasisi ya kifedha hasa CRDB, ambayo kabla kijana hajapata mkopo, huwa anapata fursa ya kupewa mafunzo maalum yanayohusiana na usimamizi wa kifedha, nidhamu pamoja na biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafunzo haya yanakuwa endelevu pia, ili kuhakikisha kwamba wanaendelea kupata elimu hiyo kwa namna endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napokea wazo lako na ushauri wako juu ya kuwa na SACCOS za vijana, na kama ambavyo Serikali imeendelea kuwezesha kwenye vikundi, tutaendelea kuifanyia kazi ili kuhakikisha kwamba vijana wanafikiwa kwa wingi. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Asia Halamga, nilikuona.

MHE. ASIA A. HALAMGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana wa Wilaya ya Hanang, wameniagiza na kunituma, wanakuhitaji, Mheshimiwa Waziri, je, ni lini utakuja kukutana na vijana wa Wilaya ya Hanang?

19 MEI, 2026

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MAENDELEO YA VIJANA:

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa swali la Mheshimiwa Asia na nimpongeze pia kwa kuendelea kufuatilia masuala yanayohusu vijana hasa katika Jimbo lake la Hanang.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama Wizara, tunao utaratibu na ratiba ya kutembelea vijana katika maeneo mbalimbali kama ambavyo tumefanya tayari katika maeneo kadhaa ya nchi yetu. Nimhakikishie Mheshimiwa Asia, tutakapokuwa tunaweka ratiba kwa mara nyingine tena, basi tutafika pia katika Jimbo la Hanang kuweza kuwafikia na kuweza kusikia changamoto zao, lakini pia kuwaletea fursa ambazo zinapatikana. Nashukuru sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Rashid Shangazi.

MHE. RASHID A. SHANGAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti,

ahsante, tatizo la vijana sio mitaji na ajira pekee, lakini yako matatizo makubwa sana ya kisera kwenye sekta mbalimbali yanayowafanya vijana wasikue kwa haraka. Ni upi mkakati wa Serikali kuhakikisha kwamba sera zote katika kila sekta zinapitiwa ili kuruhusu ukuaji wa wa mitaji na uwezo wa wa kiuchumi kwa vijana?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MAENDELEO YA VIJANA:

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na nashukuru kwa swali la Mheshimiwa Shangazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba changamoto za vijana ni zaidi ya mitaji na ndiyo maana kwa mujibu wa Sera yetu ya Maendeleo ya Vijana Toleo la mwaka 2024, limeainisha maeneo 13 ambayo tunayalenga na mitaji ni sehemu mojawapo tu ndogo. Nimhakikishie Mheshimiwa Shangazi kwamba tumeendelea kufanya marejeo na mapitio ya sera ambazo zitatusaidia pia kuelekea katika sheria. Moja ya mafanikio ya sera ya mwaka 2007 ilikuwa ni kutungwa kwa sheria ya asilimia nne

19 MEI, 2026

katika halmashauri zetu, lakini pia 30% ya manunuzi kwa ajili ya makundi maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tutaendelea kufanya hivyo kama Serikali na kuhakikisha kwamba kila eneo ambalo vijana wanaweza wakapata fursa tunaendelea kuleta marekebisho hayo ya kisera zaidi. Nashukuru sana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Joel Nanauka, Waziri, tunakushukuru kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea, sasa ni Wizara ya Uchukuzi, namwita Mheshimiwa Kassimu Amari Mbaraka, Mbunge wa Tanga Mjini aweze kuuliza swali lake.

Na. 377

Ujenzi wa Reli ya Kisasa kutoka Bandari ya Tanga hadi Musoma

MHE. KASSIMU A. MBARAKA aliuliza:-

Je, lini ujenzi wa Reli ya Kisasa (SGR) kutoka Bandari ya Tanga - Kilimanjaro - Arusha - Singida hadi Musoma (kilometa 1108) utaanza?

MWENYEKITI: Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Uchukuzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kassimu Amari Mbaraka, Mbunge wa Tanga Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia TRC imekamilisha upembuzi yakinifu na usanifu wa awali kwa ajili ya kuunganisha reli ya Bandari ya Tanga na Mikoa ya Kilimanjaro, Arusha, Singida hadi Musoma. Kwa sasa hatua inayoendelea ni kuhuisha yaani review tafiti hizo, ili kuendana na mahitaji ya sasa ikiwemo ushirikishwaji wa makampuni ya madini yanayowekeza kwenye

19 MEI, 2026

ushoroba huo. Aidha, Serikali inaendelea na kufanya majadiliano na kampuni mbalimbali ili kufanya uwekezaji wa reli hii ya kimkakati.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kassimu Amari Mbaraka, swali la nyongeza.

MHE. KASSIMU A. MBARAKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, shukrani, nina maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza, kwa kuwa hii ndiyo reli ya kwanza kujengwa, ndani ya Taifa hili la Tanzania wakati huo ikiitwa Tanganyika. Je, Serikali ina mpango gani sasa kuimarisha na kuiboresha reli ya *meter gauge* yaani MGR, kuweza kutoa shehena nyingi, kubwa na kutosha kutoka pale Tanga, Kilimanjaro hadi Arusha? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili la nyongeza, je, ni upi mpango wa Serikali kukifanya sasa Kituo cha Pugu, *Pugu Station* kwenye reli yetu ya mwendokasi inayoenda *speed* ili ya *express*, kuweza kukifanya kuwa sasa ni kituo kama kituo kingine cha kushukia, tuseme cha tatu kutokea Dodoma na pia kutokea Dar es Salaam kiweze kutumika *effectively*, kwa reli ya mwendokasi inayoenda *speed*. Ni lini Serikali itakifanya kile kituo ni cha muhimu? (Makofi)

MWENYEKITI: Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Kassimu Amari Mbaraka kwa maswali yake ya nyongeza na nampongeza jinsi anavyofuatia maendeleo ya Mkoa wa Tanga na Kaskazini kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza, Serikali inasimamia Reli ya *meter gauge* yenye urefu wa kilometa 2,707 ambayo ilipokuwa inajengwa ufanisi wake ilikuwa ni kubeba mzigo wa takribani tani milioni tano. Kutokana na changamoto mbalimbali, reli ya Kati pamoja na Kaskazini uwezo umeshuka mpaka umefika takribani 290,000 sawa na 5.8%.

19 MEI, 2026

Mheshimiwa Mwenyekiti, tayari maboresho yameshaanza kwa upande wa reli ya kati na tayari ninavyozungumza Serikali imeshaagiza *material* kwa ajili ya kuhakikisha kwamba tunapata vitendea kazi vya kuanza ujenzi wa kutoka Ruvu kuelekea Dar es Salaam na hatua ya pili itakuwa kutoka Ruvu - Tanga mpaka Kilimanjaro, ili kuhakikisha kwamba tunaijengea uwezo kutoka kwenye *speed* ya ratili 20 mpaka 15 iliyopo sasa iweze kwenye uwezo wake wa 80 mpaka 70.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yake ya pili kuhusu Kituo cha Pugu ili tuweze kuongeza. Msingi wa reli ya kisasa ni kufupisha safari. Tunayo treni yetu ya kawaida inayofanya safari zake za kawaida kutoka Dar es Salaam mpaka Dodoma, na kutoka Dar es Salaam mpaka Morogoro na Morogoro mpaka Dar es Salaam na kadhalika ambayo kutoka Dar es Salaam mpaka hapa tuna vituo karibu 10. Serikali iliamua kuweka treni nyingine ya *express* ambayo inatoka Dar es Salaam mpaka Morogoro, ikitoka Morogoro kituo kinachofuatia ni hapa. Tumepokea maombi yake, lakini msingi tulidhani kwamba, tuendeleze ratiba hii kwanza, ikionekana kuna uhitaji sana baada ya uchambuzi wa kina tutafanya hivyo, kwa muda huu tunawashauri abiria wa pale Ruvu waweze kupanda treni ya kawaida ya kisasa ambayo na yenyewe inatumia masaa kama manne tu, na hii nyingine ni kama karibu masaa matatu na robo. Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea sasa ni Wizara ya Ujenzi, namwita Mheshimiwa John Francisco Nzilanyingi, Mbunge wa Nyamagana aweze kuuliza swali lake.

Na. 378

Ujenzi wa Barabara ya Njia Nne - Nyamagana

MHE. JOHN F. NZILANYINGI aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga barabara ya njia nne kutoka Mjini – Usagara na kutoka Mjini – Kisesa?

19 MEI, 2026

MWENYEKITI: Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa John Francisco Nzilanyingi, Mbunge wa Nyamagana, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekamilisha usanifu wa kina wa barabara za kutoka Mwanza Mjini hadi Usagara na kutoka Mwanza Mjini hadi Kisesa kwa ajili ya ujenzi wa njia nne kwa kiwango cha lami. Ujenzi wa barabara hizi utafanyika kwa awamu ambapo kwa sasa Serikali iko katika hatua ya mwisho ya manunuzi ya kumpata mkandarasi atakayejenga barabara ya kutoka Mwanza Mjini hadi Usagara yenye urefu wa kilometa 25 kwa njia nne kwa kiwango cha lami. Kwa sehemu ya Mwanza Mjini hadi Kisesa, tayari Serikali imejenga sehemu ya meta 500 kwa njia nne sambamba na ujenzi wa Daraja la Mabatini. Ujenzi wa sehemu iliyobaki utaendelea kulingana na upatikanaji wa fedha. Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa John Francisco Nzilanyingi, maswali ya nyongeza.

MHE. JOHN F. NZILANYINGI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jiji la Mwanza ni jiji ambalo linakuwa kwa kasi sana na ukuaji wa jiji hili linaenda sambamba na ongezeko la watu jambo ambalo linapelekea kuwa na foleni kubwa sana. Naomba kufahamu kutoka Serikalini, pamoja na majibu mazuri ya Serikali ni lini sasa *tender* ya ujenzi wa barabara ya kutoka Mwanza kwenda Usagara itatangazwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, Jiji letu la Mwanza lina malango makuu mawili kwa maana ya njia ya Usagara Mjini pamoja na ya Mwanza - Kisesa. Ujenzi wa barabara hizi unapaswa kwenda sambamba kwa sababu ni barabara ambazo ni mapacha na yanategemeana sana kwa ukuaji wa uchumi wa

19 MEI, 2026

jiji letu. Naomba kufahamu, tunavyoendelea na mchakato wa upande wa Mwanza – Usagara, ni lini sasa Mwanza - Kisesa nayo itawekwa kwenye mchakato wa kutangazwa ili iweze kujengwa kwa kiwango cha njia nne? Ahsante.

MWENYEKITI: Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jibu la msingi nimesema tuko kwenye hatua za mwisho na kama tuko hatua za mwisho ni kwamba, tulishatangaza *tender* na mkandarasi alishapatikana. Tunachofanya sasa hivi ni majadiliano ama *negotiations*, kulingana na ukweli kwamba sisi tunakuwa na *engineer estimate*, yaani makadirio. Sisi tunategemea hiyo barabara itakwenda, itajengwa kwa kiasi gani na mkandarasi anakuja na bei zake ambazo tuko kwenye majadiliano ili tukikubaliana na sisi tutakuwa tuko tayari kumpa hiyo kazi ya kuanza ujenzi.

Kwa hiyo, hatua ya kutangaza tulishakamilisha, tuko kwenye majadiliano na mkandarasi ambaye tunadhani anaweza akatujengea hiyo barabara na tukishakamilisha, maana yake tutakuwa tunaanza ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala lako la pili kwamba ziende sambamba na nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge, Jiji la Mwanza linakuwa sana, lakini kama nilivyosema kwamba, inategemea na uwezo wa kibajeti kwa wakati huo.

Kwa hiyo, kwa sasa tumeamua kwamba, kwanza tuanze na hiyo na kama fedha Serikali itapatikana na ndiyo maana tumeshasanifu na hata wakati tunafanya marekebisho ya pale Mabatini, tumejenga katika mtazamo huo huo wa njia nne, ambazo tunaamini barabara itakapoanza kujengwa, basi itafuata utaratibu huo huo. Kwa hiyo, ni matumaini yetu kwamba, tutaijenga pia hiyo Barabara ya Mwanza-Kisesa kwa njia nne. Ahsante.

19 MEI, 2026

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ester Bulaya, swali dogo la nyongeza.

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naomba niulize swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Barabara ya Balili – Mugeta, tayari upembuzi yakinifu umeshafanyika, na wewe Naibu Waziri unaijua, na iko kwenye Ilani yetu ya Chama Cha Mapinduzi na juzi Mwenezi ametoka kwenye Jimbo la Bunda Mjini na wananchi wamemwomba kuhusu barabara hii. Nataka kujua ni lini itajengwa kwa kiwango cha lami?

MWENYEKITI: Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, tukishafanya usanifu inakuwa ndiyo hatua za mapema ambazo Serikali sasa tunakuwa tumejua gharama ya hiyo barabara. Nimhakikishe Mheshimiwa Mbunge kwa maana ya kufanya usanifu, maana yake Serikali imeweka hiyo barabara kwenye mpango, kujenga kwa kiwango cha lami. Bajeti yetu tunaanza kesho, kwa hiyo nimhakikishe Mheshimiwa avute subira tuone kwenye bajeti tutakuja na nini kuhusu hiyo barabara. Ahsante

MWENYEKITI: Ahsante Waheshimiwa. Tunaendelea sasa namwita Mheshimiwa Edibily Kazala Kinyoma, Mbunge wa Kasulu Vijijini, aweze kuuliza swali lake.

Na. 379

Ujenzi wa Barabara kwa Kiwango cha Lami – Kasulu

MHE. EDIBILY K. KINYOMA aliuliza:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Barabara ya Uvinza – Kasulu na Makere – Nyarugusu Kitanga kwa kiwango cha lami?

MWENYEKITI: Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI alijibu:-

19 MEI, 2026

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Edibily Kazala Kinyoma, Mbunge wa Kasulu Vijijini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Barabara ya Uvinza hadi Kasulu na Barabara ya Makere – Nyarugusu hadi Kitanga ni barabara za mkoa zinazohudumiwa na TANROADS Mkoa wa Kigoma. Kwa sehemu ya Uvinza hadi Kasulu yenye urefu wa kilometa 56.8, kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina imekamilika, na Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami. Aidha, kwa sehemu ya Makere – Nyarugusu hadi Kitanga, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina ikiwa ni maandalizi ya kuijenga kwa kiwango cha lami. Ahsante

MWENYEKITI: Mheshimiwa Edibily Kazala Kinyoma, maswali ya nyongeza.

MHE. EDIBILY K. KINYOMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hizi ni ahadi ya Mheshimiwa Rais, lakini pia Mheshimiwa Naibu Waziri amekuwa Mkurugenzi kwenye Halmashauri yetu anafahamu umuhimu wa hizi barabara. Je, Serikali haioni haja ya kutenga fedha kwenye hii bajeti kuhakikisha barabara hizi zinajengwa kwa kiwango cha lami?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia swali la pili, barabara hizi zimepita karibu na SGR, mahali ambapo SGR inajengwa kuelekea Burundi. Je, Serikali haioni iko haja ya kuzijenga barabara hizi kwa haraka ili wananchi waweze kunufaika na fursa za SGR kabla SGR haijamalizika kujengwa? (Makofi)

MWENYEKITI: Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Kasulu Vijijini kama ifuatavyo:-

19 MEI, 2026

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nianze na Barabara ya Uvinza - Kasulu. Barabara ya Uvinza - Kasulu nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge, kimsingi ndiyo tunayoita *T Number Nine* ambayo inatoka Tunduma – Mpanda – Uvinza - Kasulu hadi Nyakanazi. Nakubaliana naye kwamba ni kipande hicho tu ambacho kwa sasa kinatafutiwa fedha ili kiweze kujengwa na tukamilishe barabara yote Nyakanazi – Kasulu - Mpanda, Sumbawanga hadi Tunduma. Kwa hiyo, nakubaliana na wewe na Serikali inalijua hilo. Kwa hiyo, tunafanya kila jitihada tutafute fedha kuanza kujenga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Barabara ya Makere - Nyarugusu kwenda Kitanga, Mheshimiwa Mbunge anakubaliana nami kuwa hiyo barabara ilikuwa inahudumiwa na wenzetu wa *TARURA*, ndiyo imepandisha hadhi na nadhani ndiyo kwanza tunataka tuitengeneze iwe katika mfumo wa *TANROADS*, wakati tunaendelea kutafuta fedha ya kuisanifu ili kwa kweli iweze kujengwa kwa kiwango cha lami, kwa sababu inaenda sambamba pia na *SGR*, pia inaenda mpakani, nchi ya Burundi. Kwa hiyo, tunalifahamu hilo, ndiyo maana tumeipandisha na tunaitafutia fedha kuisanifu ili tuweze kujenga kwa kiwango cha lami. Ahsante

MWENYEKITI: Nilikuona na Mheshimiwa Yustina Rahhi, swali la nyongeza.

MHE. YUSTINA A. RAHHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali itaanza kujenga lini barabara ya Karatu - Mbulu kipande cha kilometa 76, kwa kuwa iko kwenye Ilani, lakini vilevile ni ahadi ya viongozi? Ahsante sana.

MWENYEKITI: Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, Barabara ya Karatu – Mbulu – Haydom - Sibiti hadi Lalago – Maswa ni barabara ambayo ilitakiwa ijengwe yote, lakini baada ya kusitisha ule mpango, tumeigawa katika vipande vitatu ambao tumeshaanza kujenga. Tumeanza Mbulu hadi Garbabi -

19 MEI, 2026

Labay hadi Haydom. Sasa hivi tunaenda Nkoma kwenda Lalago. Kwa hiyo, tutakuja baada ya kukamilisha hivyo vipande vitatu, utaratibu utakaofuata sasa itakuwa ni kujenga Mbulu kwenda Karatu. Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa tunaendelea. Sasa namwita Mheshimiwa Haran Nyakisa Sanga, Mbunge wa Kigamboni aweze kuuliza swali lake.

Na. 380

**Tofauti ya Daraja la Tanzanite na Daraja la Mwalimu Nyerere
Kigamboni**

MHE. HARAN N. SANGA aliuliza:-

Je, kuna tofauti gani kati ya Daraja la Tanzanite na Daraja la Mwalimu Nyerere Kigamboni?

MWENYEKITI: Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Haran Nyakisa Sanga, Mbunge wa Kigamboni, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitaalam Daraja la Kigamboni ni *Cable Stayed Bridge* lenye urefu wa meta 680 ambalo lilijengwa kwa makubaliano maalum kati ya Serikali na Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF). Katika makubaliano hayo, Serikali ilichangia 40% ya gharama za ujenzi na NSSF ilichangia 60%. Aidha, ilikubalika kuwa daraja hilo litakuwa la kulipia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Daraja la Tanzanite kitaalam ni *Extradosed Bridge* lenye urefu wa kilometa 1.03 ambalo lilijengwa na Serikali kwa utaratibu wa kawaida na kwa sasa siyo la kulipia. Ahsante.

19 MEI, 2026

MWENYEKITI: Mheshimiwa Haran Nyakisa Sanga, swali la nyongeza.

MHE. HARAN N. SANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa niseme sjaridhika na majibu ya Mheshimiwa Waziri, kwa sababu haioneshi utofauti wa Daraja la Kigamboni na Daraja la Tanzanite.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachoelewa mimi, haya madaraja yote yamejengwa kwa fedha za mkopo, lakini pia Serikali inahusika katika kulipa ile mikopo ambayo imetumika katika kujenga haya madaraja. Ukianza kuangalia Serikali hapa imechangia 40% na *NSSF* imechangia 60%. Wananchi wa Kigamboni wamekuwa wakilia sana kulingana na tozo zinazotolewa pale darajani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuuliza swali kwa Mheshimiwa Waziri; je, Serikali iko tayari kutoa 40% kama sehemu ya huduma, ikabaki 60% ili kushusha tozo inayotolewa pale Kigamboni? *(Makofi)*

Swali la pili, wananchi wa Kigamboni wamechangia sana tozo pale darajani. Nini kauli ya Serikali kufuta tozo kabisa ili waendeleo kupita kama wanavyopita watu wa Tanzanite? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, kwanza si vyema kulirudia swali kama lilivyoulizwa. Swali liliulizwa nini tofauti kati ya Daraja la Tanzanite na Daraja la Kigamboni?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumetoa tofauti hiyo, kwanza kitaalamu kwa maana swali liko hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, kuna tofauti gani kati ya Daraja la Tanzanite na Daraja la Mwalimu Nyerere Kigamboni. Tumetoa tofauti kitaalamu kwa maana ya ujenzi ilivyojengwa, lakini pia *operations* zake zinafanyikaje. *(Makofi)*

19 MEI, 2026

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka niliweke wazi hivyo, ili sijui, lakini ndiyo swali lilivyoulizwa.

Sasa naomba nijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge. *(Makofi/Kicheko)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, pamoja na maelezo yako, ndiyo maana wakati mwingine tunaruhusu maswali ya nyongeza ambayo yako chini ya Wizara yako, ambayo unaweza kuyajibu. Yale ambayo unaweza kuyajibu, unayajibu hapo, yale ambayo huna majibu basi utayeta majibu baadaye. Kwa hiyo, naomba ujibu maswali mawili ya nyongeza. *(Makofi)*

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, kwanza niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge kwamba sasa hivi mwelekeo wa Serikali na hata mwelekeo wa Dira ya 2050 ni 70% *private sector* na 30% Serikali na huko ndiyo maana hata leo, tunafikiria kujenga barabara ya kutoka Kibaha kuja Chalinze, kuja Morogoro ikiwezekana mpaka Dodoma kwa Mpango wa PPP ambazo hizo barabara zitakuwa ni za kulipia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa NSSF sisi tunasema tuna kivuko ambacho tunasema ni daraja linalotembea na hili daraja lingine la Kigamboni Serikali iliingia ubia na wenzetu wa NSSF na ndiyo maana likawa la kulipia tangu mwanzo. Hili Daraja la Kigamboni ambalo lililinganishwa tumesema ni kama madaraja mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimhakikishe Mheshimiwa Mbunge maoni hayo tumeyapokea na tutakwenda kuyafanyia kazi, lakini niwajulishe tu Waheshimiwa Wabunge tunakoelekea sasa hivi hata kwenye barabara na nchi zingine sasa hivi ni PPP na ndiyo utaratibu ambao hata Mheshimiwa Rais ametuelekeza tuanze kufanya kazi na wenzetu wa *private sector*, ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Asha Feruz swali la nyongeza.

MHE. ASHA J. FERUZ: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi.

19 MEI, 2026

Mheshimiwa Waziri pamoja na ufafanuzi ulioutoa uchumi wa watu wa Kinondoni ambalo lipo Daraja la Tanzanite ni mkubwa kuliko uchumi wa watu wa Kigamboni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tozo inayotozwa pale kwenye Daraja la Kigamboni inasababisha nauli kuwa kubwa na kuendelea kuwafanya wananchi wa Kigamboni kuona kupita darajani ni kama adhabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuingia Kigamboni ni pesa na kutoka Kigamboni ni pesa. Ni lini mkataba huo ambao umeingiwa na Serikali pamoja na NSSF utakwisha kwa maana ya kulipa hilo deni na wananchi wa Kigamboni wanufaike na wao waone ni sehemu ya Tanzania na ku-enjoy kupita kwenye daraja? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naomba nikubaliane na Mheshimiwa Mbunge, lakini niseme tu kwa swali la msingi lilivyokuja ningemuomba Mheshimiwa Mbunge muuliza swali atuletee swali la msingi tuliweze kulifanyia kazi ili tuweze kutoa maelezo yanayojitosheleza, ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa sawa. Nilikuona Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kuweza kunipa fursa ya kuuliza swali na tunamshukuru Mheshimiwa Waziri kwa kuweza kutoa utofauti kati ya madaraja yale mawili.

Swali langu ni kutaka kujua Serikali imejifunza nini kutokana na uendeshaji wa madaraja haya mawili ili kuweza kuongeza ufanisi kwenye miundombinu mingine ya kimkakati ambayo mnajenga nchini?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ukishakuwa na *private sector* kwanza una uwezo wa kufanya

19 MEI, 2026

miradi mingi kwa sababu *private sector* wanachangia na wewe unachangia na kwa maana hiyo ndiyo maana nadhani utaona hata kwenye maboma Serikali tunasema wananchi wakishachangia tunaweza tukajenga maboma 30 badala ya kujenga maboma 15 kwa sababu kuna nguvu ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili ndiyo maana wenzetu maana yake hili siyo suala jipya labda sisi ndiyo tumeanza na wengine wanasema tumechelewa, ndiyo maana miradi mingi sasa hivi tunasema tutakwenda kwenye *PPP* na huo ndiyo mtazamo wa Serikali. Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru kwa kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Nilikuwaona Waziri wa Mipango, Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo.

WAZIRI WA MIPANGO NA UWEKEZAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Kwanza nataka nichukue nafasi kumshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri anavyojibu maswali kwa umahiri wa hali ya juu sana kwa sekta ambayo amei-master sana tangu awe Mheshimiwa Naibu Waziri katika Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka tu nijibu swali na niweke maelezo ya msingi na swali la Mheshimiwa Matiko ni la muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya fundisho ambalo tunalipata tunapoelekea kwenye ushirikiano wa sekta binafsi na sekta ya umma, ni kwamba ni muhimu tutoe elimu mapema kwa wananchi juu ya *nature* ya mradi wenyewe. Mradi wa Daraja la Kigamboni kuanzia mwanzo ilikuwa ni kwamba huu ni mradi ambao utajengwa kwa fedha zitakazotolewa na *NSSF* na utakapokamilika ni kwamba fedha zitarudi kwa wananchi kulipa fee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Daraja la Tanzanite tumelijenga kwa fedha za mkopo nafuu (*concessional loan*) na mule ndani mpaka ukupe *concessional loan* maana yake ni kwamba siyo *business* tungeweka tangu mwanzo kwamba wananchi watalipa isingekuwa *concessional loan*.

19 MEI, 2026

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ambacho tunajifunza hapa ni kwamba lazima sisi Serikali tutoe maelezo ya kina kuhusu mradi unapoanza. Hapa tunajiandaa kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri tunajiandaa kutekeleza mradi wa PPP wa barabara ya Dar es Salaam - Chalinze kuja huku kwa PPP maana yake lazima tuambie wananchi kwamba mradi huu utajengwa kwa PPP na kwamba fedha ambazo zitajenga zitarudishwa kwa njia ya kulipa.

Kwa hiyo, watakapokuwa wanapita siyo tumejenga leo kesho wakasema ah! kwa nini tunalipia, kwa hiyo nadhani kitu kikubwa hapa ni kwamba ni elimu kwa umma na tutaongeza jitihada katika eneo hilo. Ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri ahsante na Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yenu kwa maswali Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea sasa ni Wizara ya Maji na namwita Mheshimiwa Twaha Said Mwakioja, Mbunge wa Mkinga, aweze kuuliza swali lake.

Na. 381

Utafiti wa Vyanzo vya Uhakika vya Maji Tarafa ya Maramba

MHE. TWAHA S. MWAKIOJA aliuliza: -

Je, lini Serikali itafanya utafiti wa vyanzo vya uhakika vya maji Tarafa ya Maramba, Wilaya ya Mkinga ili kutatua changamoto ya maji kwa wananchi?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji napenda kujibu swali la Mheshimiwa Twaha Said Mwakioja, Mbunge wa Jimbo la Mkinga kama ifuatavyo:-

19 MEI, 2026

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeanza utafiti wa maji chini ya ardhi katika maeneo yenye changamoto ya upatikanaji wa maji Wilayani Mkinga, mkoani Tanga ikiwemo baadhi ya maeneo ya Tarafa ya Maramba. Utafiti huo umeonesha uwepo wa maji chini ya ardhi katika vijiji vinne vya tarafa hiyo ambavyo ni Kichangani, Gombero, Maramba A na Matemboni, sanjali na Kijiji cha Mkota kilichopo Kata ya Mwakijembe wilayani humo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa taratibu za kuanza uchimbaji wa visima virefu katika maeneo yaliyobainishwa zinaendelea. Aidha, Serikali itaendelea na zoezi la utafiti wa vyanzo vingine vya maji katika maeneo yenye changamoto wilayani Mkinga ili kukidhi mahitaji ya wananchi wa wilaya nzima ikiwemo wale wa Tarafa ya Maramba.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Twaha Said Mwakioja swali la nyongeza.

MHE. TWAHA S. MWAKIOJA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu ya Serikali japo kwa maoni yangu nayaona bado ni majibu mepesi. Hivyo nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Mkinga na hususan tarafa ya Maramba imekuwa na miradi ambayo haijakamilika na ilipaswa kukamilika tangu mwaka 2023 na wakandarasi wameshaondoka maeneo ya mradi na sababu kuu ni kwamba wakandarasi hawa hawajalipwa; Kata ya Gombero mkandarasi ameondoka na anadai shilingi bilioni 1.2, Kata ya Mhinduro, mkandarasi ameondoka na anadai shilingi milioni 368, Kata ya Mapatano mkandarasi ameondoka na anadai shilingi milioni 196, Mradi wa Mkinga - Horohoro mkandarasi anadai zaidi ya shilingi bilioni 1.7.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, pamoja na fedha nyingi tunazopewa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, miradi hii imechelewa zaidi ya miaka minne wananchi hawapati maji. Je, sasa ni lini Serikali ituambie kwa uhakika kabisa wakandarasi hawa watalipwa ili wakandarasi warudi na wananchi waweze kupata maji safi na salama waliyoahidiwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan?

19 MEI, 2026

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; tarafa hii ya Maramba ina hali ngumu sana ya upatikanaji wa maji na hususan wakati wa kiangazi. Naomba Serikali ituambie, Mheshimiwa Waziri yuko tayari kuambatana nami mara tu baada ya Bunge hili la bajeti ili tutembee kata kwa kata tujionee hali halisi na ikiwezekana tupate vyanzo vya uhakika na ikibidi tarafa hii ya Maramba tuweze kuiunganisha na mtandao wa Gridi ya Maji ya Taifa? Ahsante. (Makofi)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Twaha Said Mwakioja, Mbunge wa Mkinga kwa kazi nzuri, kubwa anayoifanya na kwa ufuatiliaji na kwa kata hii ya Maramba natambua kwamba Mheshimiwa Mbunge aliongea kwenye bajeti yetu ya maji, lakini pia amekuwa na mawasiliano ya karibu sana na Mheshimiwa Waziri wa Maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na swali lake la kuhusu miradi iliyoko katika kata tatu; mradi wa kwanza ambao umesema upo Gombero ni kweli, lakini Mradi wa Mapatano pamoja na Mhinduro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Gombero umeshafikia 100% maana yake umeshakamilika, mkandarasi natambua anadai kiasi cha shilingi bilioni 1.2. Mradi wa Mapatano kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge amesema upo katika hatua ya 35% ya utekelezaji na Mradi wa Mhinduro upo 46%. Tunatambua tulikuwa tunafanya uhakiki wa zile hati zake za madai ili tulipe fedha inayoendana na kazi ambayo kule imefanyika kwa sababu tumebaini kuna maeneo mengine hati zinazoletwa haziiendani na hali halisi ya kazi iliyofanyika *site*, hizi ni fedha za Watanzania za walipakodi wa Tanzania lazima tuzisimamie ili ziweze kutoa matokeo halisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nakuhakikishia kazi ya uhakiki tumeshaimaliza, sasa tunasubiri kuwalipa wakandarasi ili waweze kurudi *site* kwa upande wa Mapatano pamoja na Mhinduro waweze kufanya kazi nzuri.

19 MEI, 2026

Mheshimiwa Mweyekiti, lakini pia upande wa Mkinga Horohoro Mheshimiwa Rais amewekeza zaidi shilingi bilioni 35 katika mradi huu na mradi huu upo hatua nzuri kabisa sisi tunachokifanya hatupeleki fedha kwa kasi tunayotaka sisi, tunapeleka fedha baada ya hati ya madai kuja mezani.

Kwa hiyo, sisi tutahakikisha kwamba tunaongeza msukumo pale ambapo hati imeshafika mezani lazima mkandarasi alipwe na kuhakikisha kwamba mradi uweze kuendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia hali ya upatikanaji wa maji Mheshimiwa Mbunge hata wewe unafahamu, hivi sasa ni zaidi ya 72.9% natambua changamoto ya kwenda kufanya utafiti. Mheshimiwa Waziri ulimuomba kwenda katika jimbo lako, nataka nikupe taarifa nzuri ni kwamba Mheshimiwa Waziri pamoja na wataalam wa Wizara pamoja na wewe, yupo tayari kuambatana nawe kwenda katika jimbo lako ili kwenda kufanya kazi hiyo, lakini lengo kubwa ni nini, lengo kubwa la kwenda Mkinga la kwanza ni kwenda kufanya tathmini ya vyanzo vya maji vilivyopo na la pili kwenda kubaini vyanzo vipya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu, kama ambavyo umeomba kuangalia uwezekano wa Tarafa ya Maramba inaunganishwa kwenye Gridi ya Taifa ya Maji. Katika hili hatutosubiri Mheshimiwa Waziri aende, ninawaelekeza bonde waanze kufanya hii kazi kabla ya Mheshimiwa Waziri hajaenda ili anapofika wampatie taarifa ya tathmini ambayo watakuwa wameshaifanya na wewe Mheshimiwa Mbunge ukiwepo ili sasa tuanze kuchukua hatua ya kufanya *feasibility study*, baada ya hapo tupate fedha na baada ya hapo tuanze kutekeleza mradi bila kuwa na cha...

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafahamu sauti yako ni sauti ya wananchi wa Mkinga na sisi kama Serikali tutaendelea kushirikiana na wewe ili kutatua changamoto ya upatikanaji wa maji ndani ya Jimbo la Mkinga, ahsante sana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa *Engineer* Ramadhan Singano swali dogo la nyongeza.

19 MEI, 2026

MHE. RAMADHANI H. SINGANO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, Wilaya Lushoto miongoni ya wilaya ambazo maeneo machache yana changamoto ya maji juu ya ardhi ikiwemo Kata ya Milingano maeneo ya Kwebamba na Kishimai, lakini Kata ya Mbwei na Malibwi kwa Tarafa ya Mlola. Je, Serikali ina mpango gani madhubuti wa kimkakati na wa kiutafiti kuhakikisha kwamba maeneo hayo yanafanyiwa utafiti na kuwapatia suluhu ya changamoto ya maji?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa *Engineer* Ramadhani Singano, Mbunge wa Bumbuli, lakini kwa kumbukumbu yangu napata kujua kwamba kata hizi ambazo ameziongelea ziko katika Jimbo la Profesa Shemdoe ambazo ziko upande wa Lushoto, lakini kwa Kata ya Mbwei mwaka 2022 tulipata fedha za UVIKO kiasi cha shilingi milioni 430 mradi huu ulitekelezwa na unafanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tunaendelea kuboresha kuna kuna chanzo cha mto fulani kitu kama Kiloleli, Kilole kitu kama hicho tunaendelea kufanya tafiti ili kubaini kama tuna uwezo wa kutumia chanzo hicho ili tupeleke maji tena kwenye Kata ya Mbwei lengo ni kuhakikisha kwamba tunaendelea kuboresha zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Ramadhani Singano ni mtaalamu wa masuala haya ya maji (*water resources*) tunatambua kwamba namna gani anatamani tuendeleo kuhakikisha kwamba tunawatumia wataalam wa Wizara ya Maji kubaini vyanzo vipya ili tuhakikisha kwamba tunaendelea kuboresha huduma ya maji safi na salama. Tunaendelea kupokea maoni na ushauri ili tuendeleo kuboresha upatikanaji wa huduma maji safi na salama kwa wananchi, ahsante sana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa, ahsante. Mheshimiwa Abdallah Chaurembo, swali dogo la nyongeza.

19 MEI, 2026

MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kata ya Kilungule ina changamoto ya upatikanaji wa maji safi ya kunywa na matamu. Je, Serikali ina mpango gani wa kutoa maji kutoka Mashine ya Maji Mtoni kupeleka Kata hiyo ya Kilungule?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Chaurembo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Dar es Salaam ni eneo ambalo tunasema kwamba ni eneo la kiuchumi na ni muhimu sana kuhakikisha kwamba huduma ya maji inakuwa sehemu ya kichocheo cha uchumi wa Jiji la Dar es Salaam, lakini nikizingatia kwamba chanzo tayari tunacho, kinachohitajika tu ni kuongeza mtandao kufika katika kata ambayo Mheshimiwa Mbunge amesema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunalipokea na nimwelekeze kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji *Chief Executive Officer* wa DAWASA atume wataalamu wake, wakafanye tathmini na kujiridhisha kwamba tunaweza tukachukua hatua ipi ili kuhakikisha kwamba wananchi wa kata ambayo Mheshimiwa Mbunge ameitaja basi wapate huduma ya maji safi na salama baada ya kuwa tumetengeneza mtandao wa kuwafikia wananchi hao, ahsante sana.

MWENYEKITI: Waheshimiwa tunaendelea sasa namwita Mheshimiwa *Engineer* Fadhili Sandali Chilombe Mbunge wa Tunduru Kusini aweze kuuliza swali lake.

Na. 382

Utekelezaji wa Miradi ya Maji – Tunduru Kusini

MHE. ENG. FADHILI S. CHILOMBE aliuliza: -

Je, lini Miradi ya Maji ya Tuwemacho, Masuguru-Mchoteka, Liwanga, Msingi na Azimio itakamilika?

19 MEI, 2026

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji napenda kujibu swali la Mheshimiwa *Engineer* Fadhili Sandali Chilombe Mbunge wa Tunduru Kusini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea na utekelezaji wa Miradi ya Maji ya Tuwemacho, Masuguru-Mchoteka, Liwanga, Msingi pamoja na Azimio iliyopo katika Wilaya ya Tunduru, mkoani Ruvuma. Baadhi ya kazi zinazotekelezwa kupitia miradi hiyo ni pamoja na ujenzi wa vyanzo vya maji, ujenzi wa nyumba za mitambo kwa maana ya *pump stations*, ujenzi wa matenki matano ya kukusanyia maji (*sump well*) na kuhifadhi maji yenye jumla ya ujazo wa lita 1,250,000. Ulazaji wa mtandao wa mabomba umbali wa kilometa 59.9 sanjari na ujenzi wa vituo 20 vya kuchotea maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi hiyo ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji ambapo miongoni mwake, Mradi wa Masuguru-Mchoteka umeanza kutoa huduma kwa wananchi wa vijiji vya Masuguru pamoja na Mchekeni wakati utekelezaji ukiwa ukiendelea. Serikali itatoa kipaumbele cha kupeleka fedha za utekelezaji wa miradi hiyo kadri zinavyopatikana ili iweze kukamilika ndani ya mwaka wa fedha 2026/2027 kama ilivyokusudiwa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa *Engineer* Fadhili Chilombe Mbunge maswali ya nyongeza.

MHE. ENG. FADHILI S. CHILOMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, kimsingi hoja za maswali haya nilikuwa nimeshapeleka Wizarani, tumeshaongea nao na yapo kwenye utekelezaji wa hatua mbalimbali. Kwa hiyo, sina swali la nyongeza zaidi ya yote ni kwamba naishukuru Serikali kwa kuchukua hatua za haraka kwenye miradi hii. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa, ahsante. Mheshimiwa Patali Patali maswali ya nyongeza.

19 MEI, 2026

MHE. PATALI S. PATALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, kwa mwaka wa fedha uliopita na mwaka wa fedha huu unaoendelea Serikali imekuwa ikitekeleza miradi sita Jimbo la Mbeya Vijijini ambayo ni Mradi wa Maji Zira, Mbagara - Yunga Mradi wa Maji wa Masoko Mradi wa Maji wa Ilea pale Ihango, Mradi wa Maji wa Ranje, Tembela pamoja na Mradi wa Maji wa Kisima, Isuto. Miradi hii imesimama kutokana na wakandarasi kukosa fedha za kuendelea na miradi hii.

Je, ni lini Serikali itawalipa wakandarasi hawa ili wakandarasi warejee *site* kutekeleza miradi hii Wanambeya Vijijini wapate maji? Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Patali Patali, Mbunge wa Mbeya Vijijini kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipaumbele cha Serikali kwa sasa ni kuhakikisha kwamba tunamalizia miradi yote ya maji ambayo inaendelea na hivi sasa tuna miradi 1206 ambayo inaendelea kote nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na kwa Mheshimiwa Patali Patali ambaye nakumbuka nikiwa katika ziara alikuja kushiriki katika mradi ule wa Kiwira ambapo tunatambua kwamba ushirikiano wa Mbeya yote na ni dhamira ya Serikali kuhakikisha kwamba tunaendelea kutekeleza na utekelezaji na kuanzishwa kwa miradi hii ya 1206 ni ishara tosha ya dhamira ya kweli ya Serikali ya kuhakikisha inaleta huduma ya maji safi na salama na toshelevu kwa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la wakandarasi kuendelea kulipwa tumeshakwisha weka mkakati kuanza kuwalipa awamu kwa awamu kulingana na vipaumbele vya maeneo husika, lengo ni kwamba tukitekeleza mmoja ukakamilika ukatoa matokeo basi tunakuja na mradi mwingine. Hatuwezi kuipeleka miradi yote kwa pamoja ikakamilika kwa pamoja, lazima mkakati wetu sasa Waheshimiwa Wabunge tuelewe kwamba tumekubaliana tuweke

19 MEI, 2026

awamu kwa awamu ili Wabunge wote waweze kuguswa katika maeneo yao, tusije tukajikuta tunapeleka fedha zote katika miradi yote katika eneo moja na eneo lingine likakosa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nimtoe hofu Mheshimiwa Mbunge wa Mbeya Vijijini tutakupatia vipaumbele ambavyo tumeviweka katika mkakati wetu na wewe utashiriki kushauri ili tuone namna gani tutafanya vizuri zaidi kwa ajili ya wananchi wako wa Mbeya Vijijini. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru kwa majibu yako kwa maswali Waheshimiwa Wabunge.

Sasa ni Wizara ya Fedha ninamwita Mheshimiwa Lucy Edward Mwakyembe, Mbunge wa Viti Maalum, aweze kuuliza swali lake.

Na. 383

Madeni ya Wakandarasi na Wazabuni

MHE. LUCY E. MWAKYEMBE aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kulipa madeni ya wakandarasi na wazabuni?

MWENYEKITI: Naibu Waziri wa Fedha, majibu.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ENG. MSHAMU A. MUNDE) alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Lucy Edward Mwakyembe, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Wizara ya Fedha imekuwa ikitenga bajeti kila mwaka kwa ajili ya kugharamia ulipaji wa madeni ya wakandarasi, wazabuni na watumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2025/2026, shilingi bilioni 700 zilitengwa ambapo hadi Februari, 2026 jumla ya shilingi

19 MEI, 2026

bilioni 477.6 zimetolewa. Kadhalika, Serikali imetenga kiasi cha shilingi bilioni 800 katika mwaka wa fedha 2026/2027 kwa ajili ya kugharamia ulipaji wa madeni yaliyohakikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhakikisha kuwa suala la madeni ya wakandarasi na wazabuni linadhhibitiwa, Serikali inaendelea kutoa maelekezo kwa Maafisa Masuuli kupitia waraka mbalimbali za utekelezaji wa bajeti na Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti katika mwaka husika. Maelekezo ya Serikali ni kama yafuatayo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafungu kutenga bajeti kwa ajili ya ulipaji wa madeni ya wakandarasi, wazabuni na watumishi, lakini pia Maafisa Masuuli kutumia mifumo ya kudhibiti matumizi hali kadhalika kuhakikisha kuwa mchakato wowote wa ununuzi unaanzishwa baada ya kujiridhisha uwepo wa bajeti na uhakika wa upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Fedha ninaomba kuwasilisha. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Lucy Edward Mwakyembe, maswali ya nyongeza.

MHE. LUCY E. MWAKYEMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na ninamshukuru sana Naibu Waziri kaka yangu Mheshimiwa Munde kwa majibu mazuri ya Serikali pamoja na mikakati ambayo imewekwa kwa ajili ya ulipwaji madeni hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajua Serikali inaendelea kutekeleza upatikanaji wa ajira milioni nane ambazo zimeainishwa kwenye ilani ya Chama Cha Mapinduzi mpaka kufikia mwaka 2030 na pia niwapongeze sekta binafsi ambapo zinavyoongeza kuongeza ajira za vijana wa kike na kiume katika kutekeleza ilani hiyo ya Chama Cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuuliza swali moja la nyongeza. Serikali ina mpango gani katika kusimamia madeni hayo yasiongezeke hasa ya wazabuni na wakandarasi wazawa ili kuendelea kulinda mitaji yao na wao hao kuendelea kulinda ajira

19 MEI, 2026

za vijana wa kike na wa kiume, lakini pia na kuhakikisha madeni ya watumishi yanalipwa na madeni ya watumishi hayaongezeki? Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ENG. MSHAMU A. MUNDE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Lucy Edward Mwakyembe, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli madeni ya wazabuni na wakandarasi pamoja na watumishi ni kero ambayo Wizara imeipata, lakini pia kupitia Wabunge mbalimbali jambo hili limekuwa likiongelewa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuliona hilo, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kesho siku ya Jumatano, tarehe 20 Mei itakutana na Wizara ya Fedha katika kutafakari na kuhakikisha kwamba madeni hasa hasa ya wazabuni na wakandarasi wa ndani yanaweza kulipwa ili uchumi uweze kuzunguka lakini pia vijana ambao wamefanya kazi kwenye miradi hiyo waweze kupata kujikimu na kuinua vipato na uchumi wa mmoja mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Lucy Mayenga, swali dogo la nyongeza.

MHE. LUCY T. MAYENGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili la madeni Serikalini ni suala ambalo limeumiza watu wengi sana, kwanza kwa sababu uhakiki wa madeni hauna kipindi maalum kwamba uhakiki wa madeni utafanyika ndani ya mwaka mmoja, ndani ya miaka miwili, ndani ya miaka mitatu. Kwa hiyo, wale wakopaji ambao walifanya miradi hii ya Serikali kwa nia njema wamekuwa wakiumizwa kwa *interest* za mabanki na wengi wamekuwa wakilalamika.

19 MEI, 2026

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini Wizara hii ya Fedha isikae na hao Maafisa Masuuli, kwa sababu hata hicho kinachosemwa kuanzisha miradi mipya baada ya ile miradi mingine kulipwa hakifanyiki. Kwa nini Wizara hii isingekuwa inakaa inawasaidia hawa ambao wanadai kuweza kuongea na mabenki walau kuangalia njia sahihi za kuwasaidia ikiwemo kupatana kwenye suala zima la *interest* badala ya kutoa maelekezo ambayo kwa kweli yamekuwa akiumiza sana watu? Ahsante. (Makofi)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ENG. MSHAMU A. MUNDE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Lucy kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatambua ni kweli wakandarasi na wazabuni wamekuwa wakiumia sana kutokana na kutolipwa kwa wakati ambazo wamezifanya katika miradi ya maendeleo ambayo inahudumia wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uhakiki kwa sasa kama nilivyotangulia kusema umefanyika kupitia Maafisa Masuuli, lakini pia Wizara za Kisekta na baadhi ya taarifa zilizo nyingi tumeshazipata na ndio maana kesho tuna kikao mahsusni kwa ajili ya kupitia orodha zote za madeni ili tuweze kupanga mkakati ambao utaenda kupunguza kabisa na kama sio kuondoa kwa kiwango kikubwa madeni yote ambayo wazabuni wanadai Serikali ili mwisho wa siku twende kuangalia miradi mipya badala ya kuhangaika na madeni ambayo mpaka sasa hivi wazabuni na wakandarasi wanadai.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Edifonsi Kanoni swali la nyongeza.

MHE. EDIFONSI J. KANONI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niulize swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara katika Jimbo la Kalambo ya kutoka Matai kwenda Kasesha kilometa 50 mkandarasi anadai katika kipande cha kilometa 25 shilingi bilioni 9.5; lini Serikali itatoa

19 MEI, 2026

fedha ili mkandarasi huyu akamilishe ujenzi wa barabara katika kipande cha kilometa 25? Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Edifonsi Kanoni, sitaruhusu hilo swali kwa sababu limeenda tofauti kabisa na swali la msingi, liko kwenye barabara na hapa ni masuala ya madeni ya wakandarasi na wazabuni.

Mheshimiwa Tinnar Chenge.

MHE. EDIFONSI J. KANONI: Hilo deni si la mkandarasi?

MHE. TINNAR A. CHENGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, ni lini Serikali italipa madeni ya wakandarasi wa Wilaya ya Meatu ambayo yameshafanyiwa uhakiki na kutumwa TAMISEMI na Hazina kwa ajili ya malipo? Nashukuru sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri kama unaweza kulijibu kwa sasa maana yake limeenda *specific* kwenye Wilaya husika, kama unaweza kujibu tafadhali jibu, kama hapana atajibiwa baadaye.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ENG. MSHAMU A. MUNDE): Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nijibu kwa ujumla.

Mheshimiwa Tinnar Chenge ninashukuru sana kwa swali lako lakini niseme wazi kwamba amesema madeni ya Wilaya ya Meatu. Hayo ni madeni jumuishi ambayo haijulikani sasa ni wakandarasi wa Wizara ya Maji au miradi ya barabara au ni miradi gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaongea naye nje ya *forum* hii ili kupata uhakika na *specific* hoja yake iko vipi ili tuweze kumjibu kiuhalisia kutokana na swali ambalo atakuwa ametupatia nje ya kikao hiki. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Janeth swali la nyongeza.

19 MEI, 2026

MHE. JANETH E. MAHAWANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante ninakushukuru kwa nafasi.

Swali langu linasema je, Serikali imeweka mikakati gani katika kuongeza uwazi na uwajibikaji kwenye mchakato wa ulipaji wa madeni ya wakandarasi na wazabuni?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ENG. MSHAMU A. MUNDE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali la dogo la nyongeza la Mheshimiwa Janeth kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyotangulia kusema kuhusiana na uwazi na uwajibikaji Kamati ya Kudumu ya Bajeti ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kesho linapitia taarifa zote za madeni ya wakandarasi na wazabuni. Kamati hiyo wajumbe wake ni Wabunge, Wabunge ambao wanawakilisha wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, taarifa ambazo tunazipeleka sisi kama Wizara ya Fedha inaenda kuwekwa wazi mbele ya Kamati ambayo mwisho wa siku tunaonesha ule uwazi wa kwamba madeni yote ambayo yamehakikiwa, ambayo hayajahakikiwa kiasi gani tunaenda kulipa na mkakati gani tunaenda kuufanya ili kulipa madeni hayo. Huo ndio uwazi na uwajibikaji ambao tunaongelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea Wizara ya Afya, sasa ninamwita Mheshimiwa Saashisha Elinikyo Mafuwe, Mbunge wa Hai aweze kuuliza swali lake.

19 MEI, 2026

Na. 384

Kudhibiti Watoa Elimu ya Afya na Ulaji Mtandaoni

MHE. SAASHISHA E. MAFUWE aliuliza: -

Je, kuna mpango gani wa kudhibiti watoa elimu ya afya na aina ya ulaji mitandaoni bila kuwa na taaluma inayotambulika jambo linalowachanganya wananchi?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA AFYA alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampenda kujibu swali la Mheshimiwa Saashisha Elinikyo Mafuwe, Mbunge wa Hai, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua ongezeko la watu binafsi au wataalamu wanaotoa elimu au ushauri wa afya na lishe kupitia mitandao ya kijamii, hali inayoweza kupotosha na kuhatarisha afya za wananchi. Hii inatokana na kukua kwa uelewa wa masuala ya lishe, afya, utandawazi na ongezeko la vyombo vya kutolea habari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatekeleza Sheria ya Afya ya Jamii ya Mwaka 2009 Kifungu Namba 173(1) ambacho kinamtaka mtoa maudhui, mada au matangazo yanayohusu afya ya jamii kupata kibali kutoka kwa Waziri wa Afya au Afisa aliyeidhinishwa na Waziri. Kushindwa au kwenda kinyume na sheria hii mtoa maudhui au mtoa mada atachukuliwa hatua za kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Saashisha Mafuwe maswali ya nyongeza.

MHE. SAASHISHA E. MAFUWE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, kwa kuwa tuko hivi kutokana na aina ya ulaji wetu; na

19 MEI, 2026

kwa kuwa tunakula kutokana na aina ya elimu tunayopewa; na kwa kuwa Serikali imekubali kwamba tatizo hili la utoaji wa elimu iliyochanganyikana na mambo mengi isiyothibitika lipo; na kwa kuwa Serikali imekubali kwamba sheria ipo hai inayodhibiti mambo haya; na kwa kuwa Mheshimiwa Waziri Mkuu wakati akijibu swali langu maswali ya papo kwa papo alitoa maagizo kwa Serikali sheria hii izingatiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, ni mpango gani thabiti wa Serikali na ni lini Serikali itaanza kutekeleza sheria hii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili Serikali imesomesha Maafisa Lishe na wataalamu wengine wanaohusika na lishe, lakini Serikali imeajiri Maafisa Lishe ngazi zote na wapo kwenye maeneo yetu.

Je, ni lini sasa Serikali itawatumia maafisa lishe kutoa elimu hii pamoja na kuunda Baraza la Lishe Tanzania ili waweze kushauriana na elimu hii iwe *centralized* kwa watu ambao wana taaluma ya kutoa elimu ya lishe kuliko ilivyo sasa hivi kila mtu ni mwalimu wa lishe?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA AFYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Saashisha kwa kazi nzuri anayofanya ya kufuatilia lishe za Watanzania ambazo lishe ni kigezo muhimu katika kukuza uchumi wa nchi hii, lakini nimshukuru pia Mheshimiwa Waziri Mkuu ambaye amelijibu swali hili tarehe 7 Mei na akalitolea ufafanuzi mzuri sana na sina sababu ya kurejea ufafanuzi ule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na alituelekeza tufanye tathmini ya suala hili linavyoendelea. Tathmini ambayo itatusaidia kwanza, kuwatambua hao wato wa elimu wanaotoa elimu bila kuwa na vibali. Pili, kuweka kanuni na taratibu ambazo zitawafanya waweze kufuatilia kupata vibali; tatu, tuweze kuwa na Kamati ambayo itafuatilia kwa ukaribu zaidi maudhui ya hayo na mengine mengi yatakayotufanya tuweze kufanya *reinforcement* ya hiyo sheria ambayo kiukweli haijafanyiwa *reinforcement*.

19 MEI, 2026

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba nimhakishie Mheshimiwa Mbunge tayari wataalamu wako kazini wanaendelea kufanyia kazi tathmini hizo na pindi zitakapoisha basi tutaanza utekelezaji wa sheria hii kiukamilifu ili tuweze kuendana na hali ya sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili, kwanza nimpungeze Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ambaye ukweli ndio mwanalishe wa kwanza ambaye ameajiri Maafisa Lishe nchi nzima. Kila halmashauri ina zaidi ya Maafisa Lishe wawili mpaka watatu. Tunao zaidi ya Maafisa Lishe 600 nchi nzima ambao wanafanya elimu hii ya lische lakini wanatumia taratibu za kizamani. Wanatumia redio rasmi, wanatumia mitandao rasmi, ambayo dunia sasa haiko huko kwa sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ninaomba nitoe rai, niwaelekeze Maafisa Lishe wote sasa tubadilike, twende na dunia inavyoenda, tuwafuate hao wananchi waliko. Wanataka huko kwenye *Instagram* kwenye *Facebook* ndiko waliko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia sasa waendane na hali ya sasa. Watoe elimu ambayo inavutia walaji ili wale wananchi waweze kusikiliza hicho wanachokifundisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa watumie *influencers* kwa sababu sisi Wizara ya Afya tunayo *page* ya elimu kwa jamii lakini ina *followers* wachache. Kwa hiyo, niwaombe kwamba tutumie *influencers* ili watu waweze kufikia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, na mwisho kabisa niwaombe Watanzania, nchi yetu inao wataalamu wa lische ambao wamekidhi vigezo ambao wanatoa elimu, basi tuwasikilize kule kwenye jamii zetu tunazo redio za *local content* ambazo Maafisa Lishe wanazitumia. Tufuate huko tuwasikilize lakini na Watanzania basi tusikilize elimu ya wataalamu ambao wameaminiwa na Serikali kulingana na mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha.

19 MEI, 2026

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Kilimo sasa ninamwita Mheshimiwa Esther Edwin Malleko, Mbunge wa Viti maalum, aweze kuuliza swali lake.

Na. 385

Upatikanaji wa Mbegu Bora kwa Bei Nafuu Nchini

MHE. ESTHER E. MALLEKO aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza upatikanaji wa mbegu bora na kwa bei nafuu nchini?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Esther Edwin Malleko, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kuongeza uzalishaji wa mbegu nchini kwa kutenga maeneo kwa ajili ya kuanzisha mashamba mapya ya kuzalisha mbegu, kuhamasisha kampuni binafsi za mbegu kuingia mikataba maalum na ASA ili kuzalisha mbegu bora kwa kutumia mashamba ya Serikali, na kuhamasisha uzalishaji wa mbegu za daraja la kuazimiwa ubora kwa maana ya *Quality Declared Seeds – QDS* kwa wakulima wadogo ili kuwaruhusu wakulima kuzalisha na kuuza mbegu zinazofaa kwenye maeneo husika kwa bei nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuimarika kwa uzalishaji wa mbegu nchini kutasababisha kupungua kwa ongezeko la bei linalotokana na uagizaji wa mbegu nje ya nchi. Vilevile, Wizara inaendelea kutekeleza azma ya Serikali ya kutoa ruzuku ya mbegu bora ya mazao ya kimkakati.

19 MEI, 2026

MWENYEKITI: Mheshimiwa Esther Edwin Malleko, maswali ya nyongeza.

MHE. ESTHER E. MALLEKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa majibu mazuri na maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza; Serikali ina mkakati gani basi wa kuhakikisha wananchi hasa wa vijijini wanapatiwa mbegu bora kwa wakati?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; nini mkakati wa Serikali katika kudhibiti mbegu *fake* ambazo zimekuwa ni changamoto kubwa sana kwa wakulima wanapata hasara?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na ninamshukuru Mheshimiwa Esther Edwin Malleko, Mbunge wa Viti Maalum kutoka Mkoa wa Kilimanjaro, kwa maswali madogo ya msingi yenye maslahi mapana kwa wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimthibitishie tu kwamba moja, Serikali katika mkakati wetu wa kupeleka mbegu vijijini ni kuhakikisha sasa hivi kwamba mbegu zinapatikana kabla ya msimu, lakini la pili; Serikali kupitia *TFRA* tumesajili mawakala na wasambazaji wa mbegu na tumeongeza idadi ya wasambazaji kwenda kule vijijini, na sasa hivi tunataka walau karibu katika kila kijiji kuwe na wakala ambapo mwananchi wa kawaida anaweza kufika na kupata mbegu kwa urahisi.

Kwa hiyo, hiyo ni sehemu ya mikakati ambayo Serikali tunaifanya sasa hivi ili kuhakikisha mbegu zile zinawafikia wakulima kwa urahisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu udhibiti wa mbegu *fake*, sisi kutumia mamlaka yetu ya *TOSCI* ambao ndio wathibitishaji wa hizi mbegu na ndio ambao wanadhibiti matumizi ya mbegu, wamekuwa na jukumu moja la kufanya *patrol* za mara kwa mara lakini pili, kwa wale ambao wamekuwa wakikiuka taratibu, moja tunawanyang'anya leseni za kufanya biashara ya mbegu hapa nchini, lakini pili tunawafungulia mashtaka katika mahakama zetu,

19 MEI, 2026

na wale wanaokutwa na hatia kuna fidia pamoja na hatua nyingine za kisheria ambazo zimekuwa zikichukuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo hiyo ni sehemu ya jitihada ambazo Serikali tumeendelea kuzifanya, lakini tutaendelea kuongeza elimu bora kwa wananchi ikiwemo za kutumia zile code maalum ili mwananchi anaponunua mbegu ile anatuma kwenye ile code maalum ambayo ataweza kuambiwa mbegu hii ni *fake*, imezalishwa wapi ama imepakwa sehemu gani, na mtu gani ambaye anasambaza hiyo mbegu. Kwa hiyo, hizo ni taratibu ambazo tunataka tumsaidie mkulima na ndio maelekezo ya Serikali na sasa hivi tupo katika kuyatekeleza, ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali na majibu.

Ninaomba sasa niwatangazie wageni walioko Bungeni asubuhi ya leo. Tunaanza na wageni waliokaa Jukwaa la Spika ambao ni wageni wa Mheshimiwa Dkt. Rhimo Simeon Nyansaho, Mbunge na Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, ambao ni Dkt. Faraji Mnyepe, Katibu Mkuu - Wizara ya Ulinzi. *(Makofi)*

Yupo Jenerali Jacob Mkunda, Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi. *(Makofi)*

Yupo Luteni Jenerali Salum Haji Othman, Mnadhimu Mkuu wa Jeshi. *(Makofi)*

Yupo Meja Jenerali Rajabu Mabele, Mkuu wa Jeshi la Kujenga Taifa. *(Makofi)*

Yupo Dkt. Florens Turuka, Katibu Mkuu Mstaafu; yupo Balozi John Masima, Katibu Mkuu Mstaafu; yupo Jenerali George Waitara, Mkuu wa Majeshi Mstaafu; yupo Jenerali Davis Mwamunyange, Mkuu wa Majeshi Mstaafu; na yupo Jenerali Venance Mabeyo, Mkuu wa Majeshi Mstaafu. *(Makofi)*

19 MEI, 2026

Pia yupo Luteni Jenerali Mathew Mkingule, Balozi wa Tanzania nchini Cuba na Mnadhimu Mkuu wa Jeshi Mstaafu. *(Makofi)*

Yupo pia Meja Jenerali Shabani Mani, Mkuu wa Kamandi ya Jeshi la Anga. *(Makofi)*

Pia yupo Rear Admiral Ameir Ramadhan, Mkuu wa Kamandi ya Jeshi la Wanamaji. *(Makofi)*

Yupo Meja Jenerali Iddi Nkambi, Mkuu wa Kamandi ya Vikosi chini ya Makao Makuu ya Jeshi. *(Makofi)*

Yupo Meja Jenerali Erick Mlelwa, Mkuu wa Kamandi ya Jeshi la Akiba. *(Makofi)*

Pia yupo Meja Jenerali Ibrahim Mhona, Mkuu wa Tawi la Mafunzo na Operesheni Jeshini. *(Makofi)*

Yupo Bwana Obed Sayore, Kamishna wa Sera na Mipango. *(Makofi)*

Yupo Brigedia Jenerali Bright Msuya, Kaimu Mkuu wa Mipango na Maendeleo Jeshini. *(Makofi)*

Pia yupo Brigedia Jenerali Godfrey Nyoni, Mdhiliti Mkuu wa Jeshi. *(Makofi)*

Yupo Brigedia Jenerali Hassan Mabena, Mkuu wa Utawala Makao Makuu JKT. *(Makofi)*

Yupo Luteni Jenerali Abdulrahman Shimbo, Mnadhimu Mkuu wa Jeshi Mstaafu. *(Makofi)*

Yupo Luteni Jenerali Samuel Ndomba, Mnadhimu Mkuu wa Jeshi Mstaafu. *(Makofi)*

Yupo Luteni Jenerali James Mwakibolwa, Mnadhimu Mkuu wa Jeshi Mstaafu. *(Makofi)*

19 MEI, 2026

Yupo Luteni Jenerali Charles Makalala, Mwenyekiti wa Bodi ya Shirika la Mzinga ambaye pia ni mstaafu. *(Makofi)*

Yupo Luteni Jenerali Paul Mella, Mwenyekiti wa Bodi ya Shirika la Nyumbu. *(Makofi)*

Yupo Meja Jenerali Mstaafu Michael Isamuhyo, Mwenyekiti wa Bodi ya SUMA JKT. *(Makofi)*

Yupo Meja Jenerali Hawa Kodi, Mkuu wa Tawi la *Logistics* na Uhandisi. *(Makofi)*

Pia yupo Brigedia Jenerali Fabian Machemba, Kaimu Mkuu wa Usalama na Utambuzi Jeshini. *(Makofi)*

Yupo pia Brigedia Jenerali Athananius Kamhambwa, Mkurugenzi Mkuu Tanzania Automotive Technology Centre. *(Makofi)*

Yupo Brigedia Jenerali Petro Ngata, Mkurugenzi Mkuu SUMA JKT. *(Makofi)*

Pia yupo Brigedia Jenerali Solotina Nshushi, Mkurugenzi Masuala ya Kijamii Makao Makuu ya Jeshi. *(Makofi)*

Yupo Brigedia Jenerali Janet Izengo, Mkurugenzi wa Manunuzi Makao Makuu ya Jeshi. *(Makofi)*

Yupo Brigedia Jenerali Simon Pigapiga, Kaimu Mkuu wa Utumishi Jeshini. *(Makofi)*

Waheshimiwa viongozi wetu wa majeshi, karibuni sana Bungeni na tunatambua na kuthamini kazi kubwa mnayoifanya kwa nchi yetu, hongereni sana. *(Makofi)*

Wapo wageni wengine wa Mheshimiwa Dkt. Nyansaho, ambao ni Wakuu wa Mkoa; yupo Mheshimiwa Balozi Simon Sirro, Mkuu wa Mkoa wa Kigoma; yupo Kanali Donald Msengi, Mkuu wa Mkoa wa Mtwara; yupo Kanali Evans Mtambi, Mkuu wa Mkoa wa Mara; yupo Mheshimiwa Kanali Yahaya Kido, Mkuu wa Mkoa wa

19 MEI, 2026

Kagera; yupo Mheshimiwa CPA Amos Makalla, Mkuu wa Mkoa wa Arusha; yupo Mheshimiwa Balozi Dkt. Batilda Burian, Mkuu wa Mkoa wa Tanga; na yupo Mheshimiwa Jabir Makame, Mkuu wa Mkoa wa Songwe. *(Makofi)*

Waheshimiwa viongozi wetu Wakuu wa Mikoa, karibuni sana Bungeni Dodoma na sisi tunawapongeza kwa kazi kubwa mnayoifanya. *(Makofi)*

Wageni wengine wa Mheshimiwa Dkt. Nyansaho; yupo Ndugu Musa Kuji, Mkurugenzi Mkuu Hifadhi ya Taifa TANAPA. *(Makofi)*

Pia yupo Mhandisi Mohamed Besta, Mkurugenzi Mkuu Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS). *(Makofi)*

Yupo Ndugu Timothy Mgaya, Mwakilishi wa Mkurugenzi Mkuu Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO). *(Makofi)*

Pia yupo Ndugu Masha Mshomba, Mkurugenzi Mkuu Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF). *(Makofi)*

Yupo Ndugu Esther Mang'anya, Mkurugenzi Mtendaji Benki ya Azania. *(Makofi)*

Pia yupo Ndugu Filbert Mponzi, Mwakilishi wa Mtendaji Mkuu Benki ya NMB. *(Makofi)*

Yupo Ndugu Stephen Adili, Mwakilishi wa Mkurugenzi Mtendaji Benki ya CRDB. *(Makofi)*

Karibuni sana viongozi wetu. *(Makofi)*

Wapo wageni wengine wa Mheshimiwa Dkt. Nyansaho ambao ni Wakurugenzi Makao Makuu ya Jeshi, Wakuu wa Idara na Vitengo Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na uongozi wa TUGHE Tawi la Wizara. *(Makofi)*

Wapo pia wanamichezo waliofanya vizuri kitaifa na kimataifa. *(Makofi)*

19 MEI, 2026

Wapo wageni wa Waheshimiwa Wabunge; yupo mgeni mmoja wa Mheshimiwa Suma Ikenda Fyandomo ambaye ni Ndugu Ernest Paulo ambaye ni kaka yake kutoka mkoani Iringa. *(Makofi)*

Wapo wageni nane wa Mheshimiwa Rebeca Sanga Nsemwa ambao ni Kampuni ya Uuzaji wa Vifaa vya Michezo yaani *Smart Sports* ya Jijini Dar es Salaam wakiongozwa na Ndugu George Wakunda, Mkurugenzi Mkuu. *(Makofi)*

Wapo pia wageni watatu wa Mheshimiwa Haidary Hemed Sumry, wafanyabiashara na wachimbaji wadogo kutoka Mpanda, mkoani Katavi. *(Makofi)*

Wapo pia wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo; wapo wanafunzi 61 na walimu sita wa Shule ya Msingi Nyamunge kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Ilemela, Jijini Mwanza. *(Makofi)*

Wapo wanafunzi 97 na walimu sita wa Shule ya Msingi Ilolo kutoka Chamwino, mkoani Dodoma. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hao ndio wageni wetu waliotufikia kwa siku ya leo hapa Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ninalo tangazo kutoka kwa Mwenyekiti wa *Bunge Sports Club*, Mheshimiwa Rebeca Nsemwa, anaomba kuwatangazia Waheshimiwa Wabunge kuwa leo timu yetu ya *Bunge Sports Club* itapokea vifaa vya michezo kwa ajili ya mazoezi kutoka Kampuni ya *Smart Sports* ambao ni wauzaji wa vifaa vya michezo. Manahodha wa michezo yote wanaombwa wahudhurie upokeaji wa vifaa hivyo saa 5.00 asubuhi kwenye ukumbi wa Jengo la Habari.

Katibu.

19 MEI, 2026

NDG. YONA KIRUMBI – KATIBU MEZANI:

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, sasa ni Hoja ya Serikali, namwita Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimiwa Dkt. Rhimo Simeon Nyansaho, aweze kuwasilisha hotuba yake. *(Makofi)*

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama ninaomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likubali kupokea na kujadili taarifa ya utekelezaji wa mpango wa bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka wa fedha 2025/2026, kwa mafungu yetu matatu, kwa maana ya Fungu 057 - Wizara; Fungu 038 - NGOME; na Fungu 039 - JKT, na kupitisha mpango wa makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nitumie fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema, kwa kujalia nchi yetu amani, utulivu na mshikamano, na kutuwezesha kuendelea kuitumikia kwa uaminifu, uadilifu tukiwa wenye afya njema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kuungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu waliotangulia kuwapongeza viongozi wa kitaifa kwa kuchaguliwa kwenye nafasi mbalimbali katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025. Kipekee nitumie fursa hii kumpongeza kwa dhati, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu, na Mheshimiwa Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuchaguliwa kuiongoza nchi yetu. Namwomba Mwenyezi Mungu azidi kuwapa maarifa, busara, hekima na nguvu katika kuliongoza Taifa letu. *(Makofi)*

19 MEI, 2026

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile napenda kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwa kuendelea kuaminiwa na wananchi kuiongoza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kipindi cha muhula wa pili. *(Makofi)*

Pia nampongeza Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, Mbunge wa Iramba Magharibi, kwa kuteuliwa kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie pia nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Musa Azzan Zungu, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuchaguliwa kuongoza mhimili huu muhimu katika kusimamia maslahi ya Taifa letu, lakini vilevile nimpungeze Mheshimiwa Daniel Baran Sillo, Mbunge, kwa kuchaguliwa kuwa Naibu Spika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatoa shukrani za dhati pia kwa Katibu wa Bunge, Ndugu Baraka Leonard, kwa ushirikiano anaotupatia katika kutekeleza majukumu yetu ya kibunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie pia nafasi hii kuwapongeza Wenyeviti wetu watatu, nikianza na Mheshimiwa Deodatus Philip Mwanyika, Mbunge wa Jimbo la Njombe Mjini; Mheshimiwa Najma Murtaza Giga, Mbunge wa Viti Maalum; na wewe mwenyewe Mheshimiwa Mwenyekiti Cecilia Daniel Parreso, Mbunge wa Viti Maalum, kwa kuchaguliwa kuwa Wenyeviti wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, ninawapongeza kwa jinsi mnavyoliongoza Bunge letu Tukufu kwa weledi na maarifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii kumpongeza pia Mheshimiwa Najma Murtaza Giga, kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, lakini pia Mheshimiwa Pascal Inyasi Chinyele, Mbunge, kuwa Makamu Mwenyekiti pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote walioteuliwa kuwa wajumbe wa Kamati hii muhimu ya NUU. Wizara inaahidi kutoa ushirikiano kwa Kamati hii,

19 MEI, 2026

katika kuhakikisha mipaka, mamlaka na maslahi ya taifa letu yanaendelea kulindwa kikamilifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza kusimama katika Bunge lako Tukufu kuwasilisha hotuba hii nikiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Kwa namna ya kipekee namshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, lakini pia Amiri Jeshi Mkuu, kwa kuniamini na kuniteua kwanza kuwa Mbunge, lakini pia kuwa Waziri wa Ulinzi, uteuzi huu ni muhimu na unanipa dhamana na heshima kubwa kwangu katika kusimamia na kuendeleza sekta ya ulinzi nchini ambayo ni kichocheo cha ukuaji wa sekta nyingine za kiuchumi, kijamii na maendeleo ya Taifa letu kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia miongozo na maelekezo ya Mheshimiwa Rais na Amiri Jeshi Mkuu, lakini pia na Dira yetu ya 2050 ambayo msingi wake mkuu ni utawala bora, amani, usalama na utulivu. Ninaahidi kutekeleza majukumu yangu kwa weledi na uadilifu kwa kushirikiana na Bunge lako Tukufu ili kuhakikisha kuwa maono ya Mheshimiwa Rais na Amiri Jeshi wetu Mkuu yanatekelezwa na maendeleo ya Taifa yanafikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ninawashukuru ndugu Dkt. Faraji Kasidi Mnyepe, Katibu Mkuu, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Vilevile, ninamshukuru Jenerali Jacob John Mkunda, Mkuu wetu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nitumie nafasi hii kumshukuru Luteni Jenerali Salum Haji Othman, Mnadhimu Mkuu wa Jeshi letu na watendaji wote wa Wizara kwa ushirikiano mnaonipatia katika kutekeleza majukumu yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda pia kutumia nafasi hii kuishukuru kwa dhati Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kwa maoni na ushauri kwa kukabiliana na changamoto katika sekta ya ulinzi. Vilevile, ninawashukuru kwa ushauri waliotupatia katika maandalizi ya bajeti hii. Maoni, ushauri, na maelekezo ya Kamati wakati wakichambua Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti ya mwaka wa fedha 2025/2026 na

19 MEI, 2026

Mapendekezo ya Mpango wa Bajeti ya mwaka wa fedha 2026/2027 yamesaidia kuboresha makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2026/2027. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaungana na wenzangu waliotangulia kutoa salamu za pole kwako na Bunge lako Tukufu, familia ndugu, jamaa na Watanzania wote kwa ujumla kwa kuondokewa na Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Peramiho aliyefariki tarehe 11 Disemba, 2025, na Mheshimiwa Halima Iddi Nassor, aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum Kundi la Wafanyakazi, alifariki tarehe 18 Januari, 2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niungane kutoa pole kwa kwa familia ya Mheshimiwa William Vangimembe Lukuvi aliyekuwa Waziri mwenzetu akishughulikia Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu, Bunge na Watu Wenye Ulemavu, lakini pia alikuwa ni Mbunge wa Jimbo la Isimani aliyetutoka tarehe 25 Machi, 2026. Ninaminamuomba Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sasa nijikite kuzungumzia hali ya ulinzi na usalama katika mipaka ya nchi yetu. Katika mwaka wa fedha 2025/2026 hali ya mipaka ya nchi yetu yenye urefu wa jumla ya kilometa 5,923.41 ambayo inahusisha eneo la nchi kavu, anga na eneo la maji; vyombo vyetu vya ulinzi vimeendelea kuchukua hatua madhubuti kuhakikisha ulinzi na usalama katika mipaka hiyo unaimarika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mipaka ya nchi kavu ni baina ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na nchi za Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Kenya, Malawi, Msumbiji, Rwanda, Uganda, Zambia na mipaka ya Bahari ya Hindi inayojumuisha nchi za Comoro na Visiwa vya Shelisheli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo ya kina ya hali ya ulinzi na usalama kwa kila mpaka imeoneshwa katika aya ya 13 hadi 25 katika hotuba hii ninayoiwasilisha. *(Makofi)*

19 MEI, 2026

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utekelezaji wa maagizo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama; Wizara iliwasilisha taarifa ya utekelezaji wa maazimio ya Bunge yaliyotolewa katika Bunge la Kumi na Mbili, Mkutano wa 19, Kikao cha 28, kilichofanyika tarehe 20 Mei, 2025. Kamati iliridhika na hatua zilizofikiwa katika utekelezaji wa maazimio hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, tarehe 10 Machi, 2026, Kamati ilipokea na kujadili taarifa ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa mwaka wa fedha 2025/2026 na taarifa ya utekelezaji wa mpango wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2025/2026 lakini pia na Mapendekezo ya Mpango wa Bajeti ya mwaka wa fedha huu wa 2026/2027. Kamati ilitoa maoni, ushauri na maelekezo yaliyolenga kuboresha usimamizi wa miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kuishukuru Kamati na kulihariarifu Bunge lako Tukufu kuwa maoni, ushauri na maelekezo yaliyotolewa yamezingatiwa na kufanyiwa kazi wakati wa kuandaa na kukamilisha mpango wa bajeti ya mwaka wa fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi - CCM (2025) kwa mwaka wa fedha 2025/2026; katika kutekeleza Mpango wa Bajeti ya mwaka wa fedha 2025/2026 Wizara imeendelea kutekeleza Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ya Uchaguzi Mkuu wa 2025 ambayo miongoni mwa malengo yake ni kudumisha Muungano, amani, utulivu, usalama na diplomasia ya kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhakikisha lengo hili linafikiwa, Wizara ya Ulinzi imeendelea kutekeleza ipasavyo masuala yaliyoainishwa kwenye Sura ya Ibara ya 50 ya ilani yetu ya uchaguzi kama ilivyoainishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mapitio katika utekelezaji wa mpango wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2025/2026, tathmini ya makusanyo ya maduhuli; kwa mwaka wa fedha 2025/2026 Wizara ilikadiria kukusanya maduhuli ya jumla ya shilingi 87,603,000 kutoka katika mafungu yetu matatu; Fungu 38 ambalo ni NGOME,

19 MEI, 2026

ilikusanya shilingi milioni 22; Fungu 39 ambalo ni JKT, ilikusanya shilingi 64,4003,000; na Fungu 57 ambalo ni Wizara ilikuwa na shilingi 1,200,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia mwezi Aprili, 2026 Wizara imefanikiwa kukusanya maduhuli ya jumla ya shilingi 180,505,418 kutoka kwenye mafungu yetu matatu ambayo hii ni sawa na kufikia kiwango cha 206.05% ya makadirio yaliyowekwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Fungu 38 - NGOME imekusanya shilingi 22,349,954, Fungu 39 JKT limekusanya shilingi milioni 65,603,000 na Fungu 57 Wizara imekusanya jumla ya shilingi milioni 92,552,464. Mchanganuo wa maduhuli kwa kila Fungu imeoneshwa kwenye jedwali namba moja ukurasa wa 15.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu tathmini ya utekelezaji wa bajeti ya matumizi ya kawaida na maendeleo; nianze na fedha zilizoidhinishwa. Katika bajeti ya mwaka wa fedha 2025/2026 Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa iliidhinishwa jumla ya shilingi 3,645,912,947,000; kati ya fedha hizo shilingi 3,327,115,385,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 318,797,562,000 ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu 38 - NGOME liliidhinishwa fedha za matumizi ya kawaida shilingi 2,733,729,204,00 na shilingi 48,867,636,000 kwa ajili ya matumizi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwenye Fungu 39 ambalo ni JKT matumizi ya kawaida ilikuwa ni shilingi 567,023,845,000 na matumizi ya maendeleo ilikuwa ni shilingi 9,929,926,000; lakini mwisho ilikuwa ni Fungu 57 ambalo ni Wizara na matumizi ya kawaida ilikuwa ni shilingi 26,362,336,000 na matumizi ya maendeleo ilikuwa ni 260,000,000,000. Muhtasari wa mchanganuo wa bajeti kwa kila Fungu umeainishwa katika jedwali namba mbili ukurasa wa 16.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu fedha zilizopokelewa kuanzia Julai, 2025 hadi Aprili, 2026; hadi kufikia mwezi Aprili fedha zilizopokelewa kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo ni

19 MEI, 2026

shilingi 3,122,326,357,215.44. Hii ni sawa na 85.64% ya bajeti iliyoidhinishwa; kati ya fedha hizo shilingi 3,011,737,307,354.91 ambayo ni sawa na 90.52% ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 110,589,049,860.53 ambayo hii ilikuwa ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu 38 ambalo ni NGOME limepokea fedha za matumizi ya kawaida shilingi 2,516,758,703,569.18 ambayo hii ni sawa na 92.06% na matumizi ya maendeleo ilikuwa ni shilingi 9,309,160,031.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu 39 ambalo ni JKT limepokea pia fedha za matumizi ya kawaida shilingi 470,874,925,482.33 ambayo hii ni sawa na 83.04%; kwa matumizi ya maendeleo pia JKT imepokea shilingi 9,929,926,000 ambayo hii ni sawa na 100% ya kiwango tulichokuwa tumeidhinishwa na Bunge lako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu 57 - Wizara imepokea fedha za matumizi ya kawaida shilingi 24,103,678,303.40 sawa na 91.44% na pia kwenye matumizi ya maendeleo shilingi 91,349,963,829.53 na muhtasari wa mchanganuo wa mapokezi ya fedha kwa mafungu yote umeainishwa katika jedwali namba tatu ukurasa wa 17.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uhamisho wa fedha kwa matumizi mengineyo na maendeleo; katika kipindi cha kuanzia Julai, 2025 hadi Aprili, 2026 Fungu 57 - Wizara limepokea uhamisho wa fedha za maendeleo kiasi cha shilingi 1,331,467,213,231.82 kwa ajili ya kugharamikia shughuli mbalimbali; kati ya fedha hizo shilingi 1,210,974,680,107.34 zimetolewa kugharamia mikataba ya ununuzi wa zana na vifaa kwa matumizi ya JWTZ na shilingi 117,692,467,011 kwa ajili ya kugharamia malipo ya deni la kimkataba, lakini pia shilingi 2,980,066,113 zimepokelewa kugharamia miundombinu wezeshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Wizara imepokea uhamisho wa fedha kiasi cha shilingi 7,000,000,000 katika bajeti ya matumizi mengineyo kwa ajili ya kugharamia malipo ya madeni ya huduma za matibabu kwa Hospitali za Benjamin Mkapa, MOI na Jakaya Kikwete, Jijini Dar es Salaam.

19 MEI, 2026

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu 38 - NGOME limepokea pia uhamisho wa fedha za maendeleo yenye jumla ya 20,272,046,086.54 kugharamia ununuzi wa vifaa vya mawasiliano vya JWTZ, lakini pia na kugharamia mradi wa ujenzi wa jengo la mahafali, mlango mkuu wa uzio wa Chuo chetu cha Taifa cha Ulinzi (NDC), lakini vilevile tumepokea uhamisho wa fedha zenye jumla ya shilingi 56,132,873,378 za matumizi mengineyo, fedha hizo zimetumia operesheni maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu matumizi ya fedha za kawaida; fedha zilizotolewa kwa matumizi ya kawaida katika mwaka wa fedha 2025 zimetumika kwa shughuli zifuatazo: -

- (i) Kuratibu na kusimamia mafunzo mbalimbali ya kozi za kijeshi kwa maafisa na askari ndani na nje ya nchi;
- (ii) Matunzo ya zana na vifaa vya kijeshi;
- (iii) Kuwapatia wanajeshi mafunzo ya awali na kuwaendeleza katika taaluma mbalimbali ikiwemo taaluma ya uongozi;
- (iv) Kuwapatia vijana wa Kitanzania mafunzo ya awali ya kijeshi ya ukakamavu na kuwajengea uzalendo na umoja wa kitaifa na stadi za kazi ili kuweza kujitegemea;
- (v) Kutoa huduma za afya na tiba kwa maafisa, askari, watumishi wa umma na familia zao, vijana wa Jeshi la Kujenga Taifa, wananchi wanaoishi karibu na vituo vya afya vya kijeshi.
- (vi) Kutatua migogoro ya ardhi;
- (vii) Kushirikiana na mamlaka za kiraia katika uokozi kwenye majanga mbalimbali na kutekeleza na kulinda miradi ya kimkakati;

19 MEI, 2026

- (viii) Kutoa stahili mbalimbali ikiwemo mishahara, malipo ya likizo kwa maafisa, askari na watumishi wa umma;
- (ix) Kuwasafirisha wastaafu na mizigo yao; na
- (x) Kutoa lishe kwa wenye mahitaji maalum, lakini na kuimarisha utawala bora; pia na ushirikishwaji wa watumishi kupitia vikao mbalimbali ikiwa ni pamoja na Baraza la Wafanyakazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo ya kina ya shughuli zilizotekelezwa kwa fedha za matumizi ya kawaida zimeainishwa katika aya ya 35 - 66 ukurasa wa 19 wa hotuba hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu matumizi ya fedha za maendeleo; katika mwaka wa fedha wa 2025, Fungu 57 kwa maana ya Wizara limetumia fedha za maendeleo kutekeleza shughuli mbalimbali zifuatazo: -

- (i) Kugharimia malipo ya mikataba mbalimbali ya ununuzi wa zana na vifaa kwa matumizi ya JWTZ;
- (ii) Utafiti na uhuishaji wa silaha, zana na vifaa kwa matumizi ya jeshi;
- (iii) Ununuzi wa mitambo na malighafi za kuzalisha mazao ya msingi kwa Shirika letu la Mzinga;
- (iv) Kufanya maboresho ya vifaa vya ulinzi wa anga;
- (v) Kutekeleza shughuli za utafiti na uhawilishaji wa teknolojia katika Shirika letu la Nyumbu;
- (vi) Kugharamia maboresho, huduma ya ulinzi na malipo ya huduma za umeme kwenye minara ya mawasiliano salama jeshini;
- (vii) Kugharamia ufuatiliaji na tathmini wa miradi ya shughuli mbalimbali za Wizara; na

19 MEI, 2026

(viii) Kulipa fidia ya ardhi katika maeneo yaliyofanyiwa uthamini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo yaliyofanyiwa fidia ya ardhi kuanzia mwezi Julai, 2025 hadi Aprili, 2026 yameoneshwa katika jedwali namba nne ukurasa wa 39.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2025/2026, Fungu 38 kwa maana ya NGOME, imetumia fedha za maendeleo kutekeleza shughuli mbalimbali kama ifuatavyo: -

- (i) Kwanza kugharimikia ununuzi wa risasi, mabomu na milipuko kwa ajili ya mafunzo, operesheni na mazoezi;
- (ii) Kuendeleza ujenzi wa Shule ya Polisi Jeshi Mafinga Mkoani Iringa;
- (iii) Kuendeleza ujenzi wa Makao Makuu ya Kamandi ya Jeshi la Anga;
- (iv) Umaliziaji wa ujenzi wa ukumbi wa shule yetu ya anga iliyopo Tanga;
- (v) Ujenzi wa makao makuu ya Kamandi ya Jeshi la Akiba; lakini mwisho
- (vi) Kugharimikia uboreshaji wa miundombinu ya vyuo, shule pamoja na vikosi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2025/2026, Fungu 36 - JKT limetumia fedha za maendeleo kutekeleza miradi kama ifuatavyo:-

- (i) Kuendeleza ujenzi wa kikosi kipya cha Tanganyika;
- (ii) Kumalizia ujenzi wa majengo ya makao makuu ya JKT;

19 MEI, 2026

- (iii) Ujenzi wa mahanga katika kiteule cha Chenene, kikosi cha Makutupora JKT; na mwisho
- (iv) Kuendeleza ujenzi wa Skimu ya Umwagiliaji ya Chita iliyopo Morogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kupitia mashirika yake yaani *Tanzania Automotive Technology Centre (TATC)* au Nyumbu na Shirika la Mzinga pamoja na Shirika la Uzalishaji Mali la Jeshi la Kujenga Taifa kwa maana ya SUMA JKT, imeendelea kutekeleza majukumu yake kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikianza na Nyumbu, katika mwaka wa fedha 2025/2026 Shirika la Nyumbu au *Tanzania Automotive Technology Centre* liliidhinishiwa fedha kiasi cha shilingi bilioni 15 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Kati ya fedha tumepokea hizo shilingi bilioni 5.5 na fedha hizo zimetumika kugharimikia ukamilishaji wa miundombinu ya jengo, ununuzi wa mashine na mitambo kwa ajili ya karakana, ununuzi wa malighafi na mitambo kwa ajili ya kukamilisha mradi uliopo na ukarabati wa miundombinu ya miliki na kuendeleza tafiti za teknolojia ya magari na bidhaa za viwandani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikija kwenye Shirika letu la Mzinga, katika bajeti ya mwaka wa fedha 2025/2026, Shirika la Mzinga liliidhinishiwa kiasi cha shilingi bilioni 6 kwa ajili ya kutekeleza shughuli za maendeleo. Hadi kufikia Aprili, 2026 shirika lilikuwa limepokea shilingi 4,674,582,595.94 ambayo ni sawa na 77.9% na fedha hizo zimetumika kugharimia ununuzi wa mashine na malighafi kwa ajili ya uzalishaji wa mazao ya msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, shirika katika kuongeza uzalishaji wa mazao ya msingi kwa ajili ya Jeshi letu la Wananchi na vyombo vingine vya ulinzi na usalama lipo katika mchakato wa kuanzisha kiwanda kipya kwa maana ya Mzinga II ambapo hatua iliyofikiwa sasa ni kuandaliwa kwa mkataba kati ya sisi Mzinga na mzabuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Shirika la Uzalishaji Mali la JKT kwa maana ya SUMA, katika bajeti ya mwaka 2025/2026

19 MEI, 2026

Shirika la Uzalishaji Mali la Jeshi letu la Kujenga Taifa kwa maana ya SUMA-JKT liliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni mbili kwa ajili ya kugharimia ununuzi wa mitambo. Hadi kufikia Aprili, 2026 shirika limekwisha pokea kiasi kilichoidhinishwa ambacho kimetumika kugharimia ununuzi wa mitambo na zana za kilimo kwa ajili ya kuongeza uzalishaji wa mazao mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutumia vyanzo vya ndani vya mapato, shirika limeendelea na shughuli za uzalishaji mali kupitia kampuni tanzu na viwanda vyake ili kuchangia katika uchumi wa nchi na kuipunguzia Serikali gharama za malezi ya vijana wanaojiunga na mafunzo ya JKT. Shughuli hizo zinatekelezwa kupitia sekta ya ujenzi, viwanda, biashara, huduma, kilimo, mifugo pamoja na elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ushirikiano wa ulinzi kikanda na kimataifa na ushirikiano na nchi nyingine; Wizara imeendelea kuimarisha ushirikiano wa kikanda na kimataifa kwa kushiriki vikao vya kikanda na kimataifa na kuimarisha ulinzi na usalama duniani. Wizara kupitia JWTZ imeendelea kushirikiana na nchi rafiki katika masuala ya ulinzi na usalama kwenye maeneo mbalimbali ikiwemo mafunzo, mazoezi na misaada ya kitaalamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tumeendelea kushirikiana na Umoja wa Mataifa yaani UN, Umoja wa Afrika (AU), Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) na Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC). Tunashirikiana nao katika mafunzo, mazoezi, ubadilishanaji wa wataalamu na taarifa za kiintelijensia na kufanya operesheni mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi hizo ni pamoja na Afrika Kusini, Angola, Algeria, Brazil, Bangladesh, Botswana, Burundi, Canada, Comoro, China, Cuba, DRC, Ethiopia, Falme za Kiarabu, Finland, Ghana, Hispania, India, Indonesia, Israel, Jamhuri ya Czech, Jordan, Kenya, Malawi, Marekani, Misri, Morocco, Msumbiji, Nigeria, Oman, Kuwait, Pakistan, Rwanda, Sri-Lanka, Sweden, Ufaransa, Uganda, Uholanzi, Uingereza, Ujerumani, Urusi, Uturuki, Uswisi, Zambia pamoja na wenzetu Zimbabwe. (Makofi)

19 MEI, 2026

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nijikite kwenye mafunzo ya usalama na stratejia; Wizara kupitia Chuo chetu cha Ulinzi cha NDC kwa maana ya *National Defence College* imeendelea kutoa mafunzo ya usalama na stratejia kwa maafisa waandamizi wa vyombo vya ulinzi na usalama pamoja na watumishi wa umma. Mafunzo yanayotolewa na chuo hiki ni ya uongozi katika ngazi ya kisera na kistratejia. Katika mafunzo hayo tunashirikiana na nchi mbalimbali ambazo ni pamoja na Afrika Kusini, Bangladesh, Botswana, Burundi, China, Ethiopia, India, Kenya, Malawi, Misri, Namibia, Nigeria, Rwanda, Sierra Leone, Uganda, Zambia na Zimbabwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo ya kina ya mafunzo ya usalama na stratejia yameainishwa katika aya ya 78 hadi 81 ukurasa wa 46 wa hotuba hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ushiriki wa JWTZ katika ulinzi wa amani; Wizara kupitia JWTZ imeendelea kushirikiana na jumuiya ya kimataifa na kikanda katika operesheni za ulinzi wa amani chini ya Umoja wa Mataifa na Umoja wa Afrika. Kwa sasa JWTZ ina vikundi vya ulinzi wa amani katika nchi ya DRC, Jamhuri ya Afrika ya Kati na Lebanoni. Kwa ujumla hali ya usalama ya vikundi hivyo vinavyoshiriki ulinzi wa amani ni shwari na vinaendelea kutekeleza majukumu yake kwa weledi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inaendelea kuboresha hali ya zana na vifaa kwa JWTZ na katika vikundi vinavyoshiriki katika majukumu ya ulinzi wa amani ili kuimarisha zaidi utendaji kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mpango na mwelekeo wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2026/2027; katika mwaka wa fedha 2026/2027 Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa imelenga kutekeleza mpango wa bajeti kwa kuzingatia Dira na Dhima ya Wizara; Dira ya Maendeleo ya Taifa ya 2050; Mpango wa Nne wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano yaani 2026/2030-2031 na Malengo ya Maendeleo Endelevu ya 2030; Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ya Uchaguzi Mkuu ya mwaka 2025 na Mpango Mkakati wa Wizara yaani Mpango wetu wa 2026 hadi 2030-2031

19 MEI, 2026

na taasisi zake na mwongozo wa maandalizi ya mpango wa bajeti ya Serikali ya mwaka huu wa fedha wa 2026/2027.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba uniruhusu kuwasilisha mpango wa makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka wa fedha 2026/2027 kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu makadirio ya makusanyo ya maduhuli; katika mwaka wa fedha 2026/2027 Wizara inatarajia kukusanya maduhuli ya jumla ya shilingi 90,603,000 kutoka katika mafungu yake matatu; Fungu 38 - NGOME linatarajia kukusanya kiasi cha shilingi milioni 22; Fungu 39 - JKT linatarajia kukusanya kiasi cha shilingi 67,403,000; na Fungu 57 - Wizara inatarajia kukusanya kiasi cha shilingi 1,200,000 kama ilivyoonyeshwa katika jedwali namba tano, ukurasa wa 50.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu matumizi ya kawaida na maendeleo; katika mwaka wa fedha 2026/2027 Serikali inatarajia kutenga fedha kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo jumla ya shilingi 4,286,489,324,427 ambapo kati ya fedha hizo shilingi 3,859,955,671,427 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 426,533,653,000 ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya fedha hizo Fungu 38 - NGOME linatarajia kutengewa shilingi 3,198,126,934,000 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 54,867,636,000 kwa ajili ya matumizi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu 39 - JKT linatarajiwa kutengewa shilingi 626,273,760,000 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 19,929,926,000 kwa ajili ya matumizi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu 57 - Wizara inatarajia kutengewa shilingi 35,554,768,000 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 351,736,091,000 kwa ajili ya matumizi ya maendeleo.

19 MEI, 2026

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchanganuo kwa kila fungu umeainishwa katika jedwali namba sita, ukurasa wa 51.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shughuli zinazokusudiwa kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2026/2027 zitazingatia maeneo ya kipaumbele kama ifuatavyo; kuimarisha jeshi kwa zana na vifaa vya kisasa kiteknolojia na mawasiliano, lakini pia na rasilimali watu; na kuendelea kuweka mazingira mazuri ya utendaji kazi kwa wanajeshi ikiwemo kutunza vifaa na zana, mazoezi, mafunzo, maslahi pamoja na huduma za afya na makazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha hizo zitatumika pia kuendelea kuimarisha uwezo wa Jeshi la Kujenga Taifa kwa kuboresha miundombinu ili liweze kuchukua vijana wengi zaidi watakaopata mafunzo ya awali ya kijeshi na stadi za kazi; kuendelea kuliimarisha Jeshi la Akiba, lakini pia kuendeleza na kulinda miradi ya kimkakati kwa maslahi mapana ya Taifa; kuimarisha mashirika na taasisi za utafiti kwa masuala ya kijeshi; kuanzisha viwanda vipya katika sekta ya ulinzi kwa maana ya *Defense Industries* vitakavyoweza kuzalisha bidhaa kwa matumizi ya kijeshi na kiraia; kuanzisha viwanda vipya kwa kushirikiana na sekta binafsi; kuimarisha ushirikiano na Umoja wa Mataifa, Umoja wa Afrika, Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika na Jumuiya ya Afrika Mashariki katika masuala ya ulinzi; na mwisho, kuendeleza kushirikiana na mamlaka za kiraia katika kukabiliana na majanga na dharura itakapohitajika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa shukrani, kabla ya kuhitimisha hotuba yangu, ninapenda kutumia fursa hii ili kuwashukuru viongozi na watendaji wa Wizara ninayoiongoza na taasisi zake kwa ushirikiano wanaonipatia katika kazi hii kubwa, lakini kwa michango yao madhubuti iliyowezesha kutekeleza mpango wa bajeti wa mwaka wa fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mafanikio na ushirikiano mkubwa katika kutayarisha makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2026/2027, ninapenda kumshukuru Katibu Mkuu Dkt. Faraji Kasidi Mnyepe; pia, ninamshukuru Mkuu wa Majeshi, Jenerali Jacob John Mkunda; pia, nitumie nafasi hii

19 MEI, 2026

kumshukuru Luteni Jenerali Salum Haji Othman, Mnadhimu wetu Mkuu wa Jeshi; Meja Jenerali Rajabu Ndiku Mabele, Mkuu wa Jeshi la Kujenga Taifa; Wakuu wa Kamandi, Wakuu wa Matawi, Makao Makuu ya Jeshi na JKT; Wakuu wa Mashirika, Wakuu wa Idara na Vitengo, Wakuu wa Vyuu, Shule na Vikosi vya Jeshi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, ninawashukuru maafisa askari na watumishi wa umma kwa ushirikiano wanaonipatia. Mafanikio tulioyapata yanatokana na bidii, nidhamu, uhodari na kujituma kwao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nitumie fursa hii kwa niaba ya Serikali kutoa shukrani kwa washirika wa maendeleo na Serikali za nchi mbalimbali kwa ushirikiano wanaoendelea kuipatia Wizara yetu. Washirika hao ni pamoja na Umoja wa Mataifa, Umoja wa Afrika, Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika, Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Nchi za Ukanda wa Maziwa Makuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tunazishukuru nchi rafiki katika shughuli zetu za ulinzi ambazo ni pamoja na Afrika Kusini, Algeria, Angola, Bangladesh, Burundi, Jamhuri ya Watu wa China, Cuba, Jamhuri ya Czech, Ethiopia, Finland, Ghana, Hispania, India, Indonesia, Israel, Jordan, Kenya, Msumbiji, Kuwait, Malawi, Marekani, Misri, Morocco, Nigeria, Oman, Pakistan, Rwanda, Serbia, Sri Lanka, Sweden, Uganda, Ufaransa, Ujerumani, Uingereza, Umoja wa Falme za Kiarabu, Urusi, Uturuki, Zambia na Zimbabwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba pia kuzishukuru Wizara na taasisi zote. Kwa Wizara yetu, hii ni Wizara ya kutoa huduma kwa maana kazi yetu ya msingi ni kutoa ulinzi. Kwa kazi yetu tunahitaji sana ushirika na wenzetu wa Wizara na taasisi zote, lakini pia na wananchi wote. Tunapenda kutumia nafasi hii kuwashukuru wananchi wote kwa ushirikiano wanaoutoa kwa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa pamoja na taasisi zake katika ulinzi wa nchi yetu. *(Makofi)*

19 MEI, 2026

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni matumaini yangu kuwa tutaendelea kushirikiana zaidi kwa manufaa ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kuishukuru familia yangu kwa maombi yao kwangu na Taifa letu. Pia ninapenda kukushukuru wewe binafsi, lakini pia Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, lakini bila kuwasahau Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ni maombi ya fedha; kwa mwaka wa fedha 2026/2027 Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na taasisi zilizo chini yake inaliomba Bunge lako Tukufu liidhinishhe jumla ya shilingi 4,286,489,115,000 ambazo kati ya fedha hizo shilingi 3,859,955,462,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 426,533,653,000 ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

HOTUBA YA MHESHIMIWA DKT. RHIMO S. NYANSAHO (MB), WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2026/27 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

A. UTANGULIZI

1. Mheshimiwa Spika, kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama (NUU) iliyochambua na kutoa ushauri ulioboresha Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, ninaomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likubali kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2025/26. Aidha, ninaomba Bunge lako Tukufu lijadili na kupitisha Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2026/27 kwa mafungu yote matatu (Fungu 57 - Wizara, Fungu 38 - NGOME na Fungu 39 - JKT).

2. Mheshimiwa Spika, awali ya yote nitumie fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema, kwa kujialia

19 MEI, 2026

Nchi yetu amani, utulivu na mshikamano na kutuwezesha kuendelea kutumikia Taifa letu kwa uaminifu na uadilifu tukiwa wenye afya njema.

3. Mheshimiwa Spika, napenda kuungana na waheshimiwa wabunge wenzangu waliotangulia, kuwapongeza viongozi wa kitaifa kwa kuchaguliwa kwenye nafasi mbalimbali katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025. Kipekee nitumie fursa hii kumpongeza kwa dhati **Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu na **Mhe. Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi**, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuchaguliwa kuiongoza Nchi yetu katika Serikali ya Awamu ya Sita. Ninamuomba mwenyezi Mungu azidi kuwapa maarifa, busara, hekima na nguvu katika kulingoza Taifa letu.

4. Mheshimiwa Spika, vilevile, napenda kumpongeza **Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi**, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuendelea kuaminiwa na wananchi kuiongoza Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa kipindi cha muhula wa pili. Pia, nampongeza **Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb.)**, Mbunge wa Iramba Magharibi kwa kuteuliwa kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

5. Mheshimiwa Spika, nikupongeze wewe binafsi **Mhe. Mussa Azzan Zungu (Mb.)**, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuchaguliwa kuiongoza Mhimili huu muhimu katika kusimamia maslahi ya Taifa letu. Vilevile, nimpongeze **Mhe. Daniel Baran Sillo (Mb.)**, kwa kuchaguliwa kuwa Naibu Spika.

6. Mheshimiwa Spika, ninawapongeza **Mhe. Deodatus Philip Mwanyika**, Mbunge wa Jimbo la Njombe Mjini; **Mhe. Najma Murtaza Giga**, Mbunge wa Viti Maalum; na **Mhe. Cecilia Daniel Pareso**, Mbunge wa Viti Maalum kwa kuchaguliwa kuwa Wenyeviti wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, ninawapongeza kwa jinsi mnavyoliongoza Bunge letu Tukufu kwa weledi na maarifa.

7. Mheshimiwa Spika, ninaomba nitumie fursa hii, kuwapongeza waheshimiwa mawaziri na naibu mawaziri

19 MEI, 2026

walioteuliwa kuongoza wizara mbalimbali. Aidha, nawapongeza waheshimiwa wabunge waliochaguliwa na walioteuliwa kulitumikia Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nawatakia kila la heri katika utekelezaji wa majukumu yao.

8. Mheshimiwa Spika, kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza kusimama katika Bunge lako Tukufu kuwasilisha Hotuba hii nikiwa Waziri wa Ulinzi na JKT, kwa namna ya kipekee namshukuru **Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu kwa kuniamini na kunitiua kuwa Mbunge na Waziri wa Wizara hii. Ninaomba niseme kuwa, uteuzi huu ni dhamana na heshima kubwa kwangu katika kusimamia na kuendeleza sekta ya ulinzi nchini ambayo ni kichocheo cha ukuaji wa sekta nyingine za kiuchumi, kijamii, maendeleo ya Taifa na wananchi kwa ujumla. Kwa kuzingatia miongozo na maelekezo ya Mhe. Rais na Amiri Jeshi Mkuu, na Dira 2050 ambayo msingi wake mkuu ni utawala bora, amani, usalama na utulivu, nitatekeleza majukumu yangu kwa weledi na uadilifu, kwa kushirikiana na Bunge lako Tukufu, ili kuhakikisha kuwa maono yake katika maendeleo ya Taifa yanafikiwa.

9. Mheshimiwa Spika, pia, nawashukuru mawaziri wenzangu na naibu mawaziri, **Dkt. Faraji Kasidi Mnyepe**, Katibu Mkuu Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, **Jenerali Jacob John Mkunda**, Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi, **Luteni Jenerali Salum Haji Othman**, Mnadhimu Mkuu wa Jeshi, na watendaji wote wa Wizara kwa ushirikiano wanaonipatia katika kutekeleza majukumu yangu.

10. Mheshimiwa Spika, nampongeza **Mhe. Najma Murtaza Giga (Mb.)**, kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, na **Mhe. Paschal Inyasi Chinyele (Mb.)**, kuwa Makamu Mwenyekiti pamoja na waheshimiwa wabunge wote walioteuliwa kuwa wajumbe wa Kamati hii. Wizara inaahidi kutoa ushirikiano kwa Kamati katika kuhakikisha mipaka, mamlaka na maslahi ya Taifa letu yanaendelea kulindwa kikamilifu.

11. Mheshimiwa Spika, napenda pia kutumia nafasi hii kuishukuru kwa dhati Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, kwa maoni na ushauri wa kukabiliwa na

19 MEI, 2026

changamoto katika Sekta ya Ulinzi. Vilevile, nawashukuru kwa ushauri waliotupatia katika maandalizi ya Bajeti hii. Maoni, ushauri na maelekezo ya Kamati wakati wakichambua Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2025/26, na mapendekezo ya Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2026/27, yamesaidia kuboresha makadirio ya mapato na matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2026/27, ninayowasilisha leo hapa Bungeni.

12. Mheshimiwa Spika, ninaungana na wenzangu waliotangulia kutoa salamu za pole kwako, Bunge lako Tukufu, familia, ndugu, jamaa, na watazania wote kwa ujumla kwa kuondokewa na **Mhe. Jenista Joakim Mhagama** aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Peramiho aliyefariki tarehe 11 Desemba, 2025, **Mhe. Halima Idd Nassor** aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum (wafanyakazi) aliyefariki tarehe 18 Januari, 2026 na **Mhe. William Vangimembe Lukuvi** aliyekuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu) na Mbunge wa Jimbo la Ismani aliyefariki tarehe 25 Machi, 2026. Ninamuomba Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi. Amina.

B. HALI YA ULINZI NA USALAMA WA MIPAKA YA NCHI

13. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2025/26, hali ya mipaka ya Nchi yetu yenye urefu wa jumla ya kilomita **5,923.41**, ambayo inahusisha eneo la Nchi kavu, anga na eneo la maji, vyombo vyetu vya ulinzi vimeendelea kuchukua hatua madhubuti kuhakikisha ulinzi na usalama katika mipaka hiyo. Mipaka ya Nchi kavu ni baina ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC), Kenya, Malawi, Msumbiji, Rwanda, Uganda, Zambia na mipaka ya Bahari ya Hindi inayojumuisha Nchi za Comoros na Shelisheli.

14. Mheshimiwa Spika, katika kipindi husika hapakuwa na matukio yaliyoashiria uvunjifu wa amani baina ya Nchi yetu na Nchi tunazopakana nazo. Hata hivyo, zimekuwepo changamoto kadhaa za kiulinzi na kiusalama katika baadhi ya mipaka ikiwemo uharibifu wa alama za mipakani, ukosefu wa barabara za ulinzi kwa baadhi ya mipaka na nyingine kuharibika pamoja na

19 MEI, 2026

migogoro ya ndani katika baadhi ya Nchi tunazopakana nazo. Taarifa kwa kila Mpaka ni kama ifuatavyo:

Mpaka wa Tanzania na Burundi

15. Mheshimiwa Spika, hali ya usalama wa Mpaka wa Tanzania na Burundi wenye urefu wa kilomita **468.85** ni shwari. Hakuna matukio yoyote yanayoashiria kuhatarisha usalama wa Nchi yetu yaliyotokea. Mpaka unakabiliwa na changamoto za uharibifu wa alama za Mpaka na barabara za ulinzi. Hali hii inaathiri shughuli mbalimbali za ulinzi katika Mpaka. Wizara kupitia JWTZ kwa kushirikiana na vyombo vingine vya usalama imeendelea kuimarisha ulinzi katika Mpaka huu.

Mpaka wa Tanzania na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo

16. **Mheshimiwa Spika**, hali ya usalama ya Mpaka wa Tanzania na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) wenye urefu wa kilomita **554** ni shwari. Hata hivyo, Mpaka unakabiliwa na changamoto za kiusalama kutokana na mapigano yanayoendelea Mashariki mwa DRC kati ya Jeshi la Nchi hiyo na makundi yenye silaha, hususan Kundi la M23. Hali hii inaathiri usalama wa Mpaka. Kundi la M23 linashikilia miji mbalimbali ya kimkakati katika majimbo ya Kivu Kaskazini na Kusini ikiwemo Goma na Bukavu na kudhibiti Mji wa Uvira. Kushikiliwa kwa miji hiyo kunaongeza changamoto za kiusalama katika Mpaka huu. Aidha, juhudi mbalimbali za kikanda na kimataifa zimeendelea kuchukuliwa kurejesha amani ya kudumu nchini DRC. Wizara kupitia JWTZ, imeendelea kufuatilia hali hiyo kwa ukaribu ikiwemo kufanya doria mara kwa mara katika Mpaka huu.

Mpaka wa Tanzania na Kenya

17. **Mheshimiwa Spika**, hali ya usalama wa Mpaka wa Tanzania na Kenya wenye urefu wa kilomita **1,187** ni shwari. Hakuna tukio lililojitokeza linaloashiria kuhatarisha usalama katika Nchi yetu. Kazi ya kuimarisha alama za Mpaka huu inayotekelezwa na Timu ya wataalam kutoka Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Jamhuri ya Kenya inaendelea.

Mpaka wa Tanzania na Malawi

18. Mheshimiwa Spika, hali ya usalama ya Mpaka wa Tanzania na Malawi wenye urefu wa kilomita **394**, ni shwari. Hakuna tukio lililotokea lenye viashiria vya kuhatarisha usalama wa Nchi yetu. Ushirikiano mzuri wa Jeshi letu na Jeshi la Malawi umeendelea kuimarisha usalama wa Mpaka huu. Changamoto katika Mpaka ni mgogoro wa kimpaka kati ya Nchi yetu na Nchi ya Malawi katika Ziwa Nyasa. Changamoto hii, imeendelea kufanyiwa kazi kupitia Tume Maalum ya Usuluhishi (High Level Mediation Team) chini ya Mhe. Joaquim Chissano, Rais Mstaafu wa Msumbiji. Serikali yetu kupitia Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, inaendelea kutumia njia za kidiplomasia ili kupata ufumbuzi wa changamoto hii. Aidha, Wizara kupitia JWTZ, imeendelea kuimarisha ulinzi katika Mpaka huu na kuhakikisha wananchi wanaoishi karibu na Ziwa Nyasa wanaendelea na shughuli zao kama kawaida.

Mpaka wa Tanzania na Msumbiji

19. Mheshimiwa Spika, hali ya usalama wa Mpaka wa Tanzania na Msumbiji wenye urefu wa kilomita **922.76**, ni shwari. Hata hivyo, Mpaka unakabiliwa na changamoto ya uwepo wa kikundi cha kigaidi cha **Ansar Al - Sunna Wal Jamaah (ASWJ) / Islamic State Mozambique Province** kilichopo Kaskazini mwa Msumbiji, katika Jimbo la Cabo Delgado linalopakana na Mkoa wa Mtwara kwa upande wa Tanzania. Pia, unakabiliwa na changamoto ya kuharibika kwa barabara za ulinzi ambazo zinaathiri shughuli za ulinzi wa Mpaka. Wizara kupitia JWTZ imeendelea kuimarisha ulinzi katika Mpaka huu kwa kuvijengea uwezo vikundi vyake kwa zana na vifaa kuhakikisha vinatekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Vilevile, Wizara imeendelea kuwasiliana na Wizara ya Ujenzi kuona namna bora ya kuimarisha barabara hizo ili kuimarisha shughuli za ulinzi katika Mpaka huu.

Mpaka wa Tanzania na Rwanda

20. Mheshimiwa Spika, hali ya usalama wa Mpaka wa Tanzania na Rwanda wenye urefu wa kilomita **230** ni shwari. Katika kipindi hiki, hakuna viashiria vyovyote vilivyoriipotiwa vyenye kuhatarisha

19 MEI, 2026

usalama wa Nchi yetu. Hata hivyo, unakabiliwa na changamoto ya kuharibika kwa alama za Mpaka na barabara za ulinzi. Hali hii inaathiri shughuli za ulinzi ikiwemo doria. Juhudi za pamoja za kuimarisha alama za Mpaka huu zinaendelea kufanyika kupitia Timu ya wataalam kutoka Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Jamhuri ya Rwanda.

Mpaka wa Tanzania na Uganda

21. Mheshimiwa Spika, hali ya usalama katika Mpaka wa Tanzania na Uganda wenye urefu wa kilomita **397.80** ni shwari. Hakuna tukio la kuhatarisha usalama wa Nchi yetu lililotokea katika kipindi hiki. Pamoja na hali hii, Mpaka unakabiliwa na changamoto inayotokana na kuharibika kwa alama za Mpaka na uingizaji haramu wa mifugo kwa ajili ya malisho hususan katika Wilaya ya Misenyi mkoani Kagera. Vilevile, unakabiliwa na changamoto ya kimpaka kutokana na Serikali ya Uganda kuibua hoja kuwa Mpaka wake na Tanzania unapita nyuzi moja (1°) Kusini mwa Ikweta, badala ya marundo ya mawe yaliyopo ambayo ndiyo Mpaka sahihi kihistoria.

22. Mheshimiwa Spika, changamoto hizi zimeendelea kushughulikiwa kidiplomasia na pande zote mbili kupitia Wizara zenye dhamana ya Ardhi na Mambo ya Nje. Aidha, Wizara kupitia JWTZ imeendelea kuimarisha ulinzi katika

Mpaka huu. Mpaka wa Tanzania na Zambia

23. Mheshimiwa Spika, hali ya usalama katika Mpaka wa Tanzania na Zambia wenye urefu wa kilomita **345**, ni shwari. Hakuna tukio lililojitokeza lenye kuhatarisha usalama wa Nchi yetu katika kipindi hiki. Changamoto zinazokabili Mpaka huu ni pamoja na uchakavu wa baadhi ya alama za Mpaka. Kukabiliana na changamoto hiyo, uimarishaji wa alama hizo umeendelea kufanyika kupitia Timu ya wataalam kutoka Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya Zambia.

Ulinzi na Usalama wa Anga la Juu

24. Mheshimiwa Spika, hali ya ulinzi na usalama wa Anga la Juu ni shwari, ingawa imekuwa isiyotabirika kutokana na kuongezeka kwa matumizi ya teknolojia ya kisasa. Aidha, Wizara ya Ulinzi na JKT kwa kushirikiana na Wizara na Taasisi nyingine inaendelea kujiimarisha kwa vifaa, zana, wataalam, mafunzo na semina, lengo ni kuhakikisha Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inakuwa salama dhidi ya matishio ya Anga la Juu.

Mpaka Katika Bahari ya Hindi

25. Mheshimiwa Spika, hali ya usalama katika Mpaka wa Bahari ya Hindi wenye urefu wa *Nautical Miles* **864.376** ni shwari. Katika Mpaka huu tumepakana na Nchi za Comoros na Shelisheli. Hakuna tukio lililoashiria kuhatarisha usalama dhidi ya Nchi yetu lililotokea katika kipindi hiki. Aidha, JWTZ imeendelea kufanya doria za mara kwa mara katika eneo la Bahari ya Hindi kwa kushirikiana na vyombo vingine vya usalama ili kubaini na kuzuia uharamia, wahamiaji haramu, uvuvi haramu, usafirishaji haramu wa binadamu, usafirishaji wa dawa za kulevya na matishio ya kigaidi.

C. UTEKELEZAJI WA MAAGIZO YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA

26. Mheshimiwa Spika, Wizara iliwasilisha Taarifa ya Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge yaliyotolewa katika Bunge la 12, Mkutano wa 19, Kikao cha 28 kilichofanyika tarehe 20 Mei, 2025 kwenye Kikao cha Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje Ulinzi na Usalama. Kamati iliridhika na hatua zilizofikiwa katika utekelezaji wa maazimio hayo. Aidha, tarehe 10 Machi, 2026, Kamati ilipokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2025/26 na tarehe 26 Machi, 2026 ilipokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2025/26 na Mapendekezo ya Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2026/27. Kamati ilitoa maoni, ushauri na maelekezo yaliyolenga kuboresha usimamizi wa miradi ya maendeleo. Napenda kuishukuru Kamati na kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa maoni, ushauri na maelekezo

19 MEI, 2026

yaliyotolewa yamezingatiwa na kufanyiwa kazi wakati wa kuandaa na kukamilisha Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2026/27 ninayowasilisha leo hapa Bungeni.

D. UTEKELEZAJI WA ILANI YA CHAMA CHA MAPINDUZI YA UCHAGUZI MKUU WA 2025 KWA MWAKA WA FEDHA 2025/26

27. Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2025/26, Wizara imeendelea kutekeleza Ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025 ambayo miongoni mwa malengo yake ni kudumisha muungano, amani, utulivu, usalama na diplomasia ya kimataifa. Kuhakikisha lengo hili linafikiwa, Wizara ya Ulinzi na JKT imeendelea kutekeleza ipasavyo masuala yaliyodainishwa kwenye **Sura ya Pili** Ibara ya 501 (vii-xii) na 51 (x) ya Ilani ambayo ni:

- a. *Kuimarisha ulinzi na usalama wa ndani ya Nchi hususan maeneo ya kimkakati kama vile bandari, viwanja vya ndege, na mipakani ili kudumisha amani, utulivu na usalama wa raia na mali zao;*
- b. *Kuimarisha vyombo vya ulinzi na usalama kwa kuboresha mazingira ya kazi ikiwemo makazi, vifaa, zana, mafunzo yanayoendana na teknolojia na mifumo ya intelijensia ya kisasa ili kutekeleza majukumu yao ipasavyo;*
- c. *Kuhamasisha na kutoa elimu kwa wananchi kuhusu masuala ya ulinzi, usalama, uzalendo wa kitaifa na umuhimu wa kushiriki katika ulinzi wa Taifa ikiwa ni pamoja na kujiunga na Jeshi la Akiba na vikundi vya ulinzi shirikishi ili kuimarisha ulinzi na usalama wa nchi yetu;*
- d. *Kuimarisha ushirikiano na jumuiya za kikanda, kimataifa, na Nchi nyingine katika nyanja za ulinzi na usalama;*
- e. *Kuimarisha kambi za Jeshi la Kujenga Taifa (Tanzania Bara) na Jeshi la Kujenga Uchumi (Zanzibar) ili kuwezesha wahitimu wa Kidato cha Sita na vijana wanaojitolea kwa hiyari kupata fursa ya mafunzo yanayolenga kujenga uzalendo kwa Taifa, moyo wa kujitolea na stadi za kazi; na*

19 MEI, 2026

f. Kuendelea kushiriki kikamilifu katika shughuli za kulinda amani kupitia misheni za kimataifa ikiwemo za Umoja wa Afrika na Umoja wa Mataifa ili kuleta utulivu katika Nchi jirani na rafiki zinazokumbwa na migogoro.

E. TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2025/26

Makusanyo ya Maduhuli

28. Mheshimiwa Spika, kwa Mwaka wa Fedha 2025/26, Wizara ilikadiria kukusanya maduhuli ya jumla ya **Shilingi 87,603,000.00** kutoka katika mafungu yake matatu, Fungu 38 - NGOME **Shilingi 22,000,000.00**, Fungu 39 - JKT **Shilingi 64,403,000.00** na Fungu 57 - Wizara **Shilingi 1,200,000.00**.

29. Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Mwezi Aprili 2026 Wizara imefanikiwa kukusanya maduhuli ya jumla ya **Shilingi 180,505,418.00** kutoka kwenye mafungu yake matatu, sawa na **asilimia 206.05** ya makadirio. Kwa upande wa Fungu 38 - NGOME limekusanya **Shilingi 22,349,954.00** ambazo zimetokana na mauzo ya nyaraka za zabuni (Sale of Tender Documents) na mapato yanayotokana na uwakala wa Bima zilizokatwa na wanajeshi kwa Shirika la Bima la Taifa.

30. Mheshimiwa Spika, Fungu 39 - JKT limekusanya **Shilingi 65,603,000.00** zilizotokana na mauzo ya nyaraka za zabuni na mauzo ya mazao ya kilimo, na Fungu 57 - Wizara, limekusanya jumla ya **Shilingi 92,552,464.00** zilizotokana na deni la ukodishaji wa simu za ZTE na ukodishaji wa minara ya mawasiliano kwa TTCL. Mchanganuo wa maduhuli kwa kila Fungu umeoneshwa kwenye **Jedwali Na. 1**

19 MEI, 2026

Jedwali Na. 1: Makadirio na Makusanyo ya Maduhuli kuanzia Julai 2025 hadi Aprili 2026.

| Fungu | Makadirio ya Maduhuli 2025/26 (Shs) | Makusanyo Julai 2025 hadi Aprili 2026 (Shs) | Asilimia ya Makusanyo |
|--------------|--|--|------------------------------|
| 38 – NGOME | 22,000,000.00 | 22,349,954.00 | 101.59 |
| 39 – JKT | 64,403,000.00 | 65,603,000.00 | 101.86 |
| 57 – Wizara | 1,200,000.00 | 92,552,464.00 | 7,712.71 |
| Jumla | 87,603,000.00 | 180,505,418.00 | 206.05 |

Bajeti ya Matumizi ya Kawaida na Maendeleo

Bajeti iliyoidhinishwa

31. Mheshimiwa Spika, katika Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2025/26, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa iliidhinishwa jumla ya **Shilingi 3,645,912,947,000.00**. Kati ya ya fedha hizo, **Shilingi 3,327,115,385,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 318,797,562,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi ya Maendeleo kwa mafungu yake matatu ambayo ni Fungu 57 - Wizara, Fungu 38 - NGOME na Fungu 39 - JKT. Mchanganuo wa Bajeti kwa kila fungu umeainishwa katika **Jedwali Na. 2**.

Jedwali Na. 2: Bajeti Iliyoidhinishwa kwa Mwaka wa Fedha 2025/26

| Na | Fungu | Matumizi ya Kawaida (Shs) | Matumizi ya Maendeleo (Shs) | Jumla (Shs) |
|-----------|------------------|----------------------------------|------------------------------------|-----------------------------|
| 1. | 38 - NGOME | 2,733,729,204,000.00 | 48,867,636,000.00 | 2,782,596,840,000.00 |
| 2. | 39 - JKT | 567,023,845,000.00 | 9,929,926,000.00 | 576,953,771,000.00 |
| 3. | 57 - Wizara | 26,362,336,000.00 | 260,000,000,000.00 | 286,362,336,000.00 |
| | Jumla Kuu | 3,327,115,385,000.00 | 318,797,562,000.00 | 3,645,912,947,000.00 |

Fedha zilizopokelewa kuanzia Mwezi Julai 2025 hadi Aprili 2026

32. Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Aprili, 2026 fedha zilizopokelewa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Maendeleo ni **Shilingi 3,122,326,357,215.44** sawa na **asilimia 85.64** ya Bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 3,011,737,307,354.91**

19 MEI, 2026

sawa na **asilimia 90.52** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 110,589,049,860.53** sawa na **asilimia 34.69** ni kwa ajili ya Matumizi ya Maendeleo.

33. Mheshimiwa Spika, kati ya Fedha hizo, Fungu 38: NGOME limepokea fedha za Matumizi ya Kawaida **Shilingi 2,516,758,703,569.18** sawa na **asilimia 92.06**, na Matumizi ya Maendeleo **Shilingi 9,309,160,031.00** sawa na **asilimia 19.05**; Fungu 39: JKT limepokea fedha za Matumizi ya Kawaida **Shilingi 470,874,925,482.33** sawa na **asilimia 83.04**, na Matumizi ya Maendeleo **Shilingi 9,929,926,000.00** sawa na **asilimia 100**; na Fungu 57: Wizara limepokea fedha za Matumizi ya Kawaida **Shilingi 24,103,678,303.40** sawa na **asilimia 91.44**, na Matumizi ya Maendeleo **Shilingi 91,349,963,829.53** sawa na **asilimia 35.13**. Muhtasari wa mchanganuo wa mapokezi ya fedha kwa mafungu yote umecainishwa katika **Jedwali Na. 3**.

Jedwali Na. 3: Mapokezi ya Fedha kuanzia Julai 2025 hadi Aprili 2026

| Fungu | Aina ya Matumizi | Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 | Mapokezi ya Fedha kuanzia Julai 2025 Aprili 2026 | Asilimia Bajeti vs Mapokezi |
|-------------------|-----------------------|-------------------------------------|--|-----------------------------|
| | | (Shs) | (Shs) | |
| 38 - NGOME | Mshahara | 2,201,453,296,000.00 | 1,959,480,540,054.58 | 89.01 |
| | Chakula | 297,424,825,000.00 | 253,587,020,749.31 | 85.26 |
| | Posho Msamaha wa kodi | 97,200,000,000.00 | 72,900,000,000.00 | 75.00 |
| | Matumizi Mengineyo | 137,651,083,000.00 | 230,791,142,765.29 | 167.66 |
| | Maendeleo | 48,867,636,000.00 | 9,309,160,031.00 | 19.05 |
| | Jumla ya Fungu | 2,782,596,840,000.00 | 2,526,067,863,600.18 | 90.78 |
| | | | | |
| 39 - JKT | Mshahara | 406,799,724,000.00 | 347,418,712,149.00 | 85.40 |
| | Chakula | 76,175,580,000.00 | 51,758,762,500.00 | 67.95 |
| | Posho Msamaha wa kodi | 12,015,600,000.00 | 8,100,000,000.00 | 67.41 |
| | Matumizi Mengineyo | 51,032,941,000.00 | 42,597,450,833.33 | 83.47 |
| | Mafunzo ya Vijana | 21,000,000,000.00 | 21,000,000,000.00 | 100.00 |
| | | | | |

19 MEI, 2026

| | | | | |
|--|---------------------------|-----------------------------|-----------------------------|--------------|
| | Mujibu | | | |
| | Maendeleo | 9,929,926,000.00 | 9,929,926,000.00 | 100.00 |
| | Jumla ya Fungu | 576,953,771,000.00 | 480,804,851,482.33 | 83.34 |
| | Mishahara | 10,782,457,000.00 | 9,963,772,420.00 | 92.41 |
| | Matumizi Mengineyo | 15,579,000,000.00 | 14,139,905,883.40 | 90.76 |
| | Maendeleo | 260,000,000,000.00 | 91,349,963,829.53 | 35.13 |
| | Jumla ya Fungu | 286,361,457,000.00 | 115,453,642,132.93 | 40.32 |
| | JUMLA KUU | 3,645,912,068,000.00 | 3,122,326,357,215.44 | 85.64 |

Uhamisho wa Fedha za Matumizi Mengineyo na Maendeleo Fungu 57 – Wizara

34. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha kuanzia Julai 2025 hadi Aprili 2026, Fungu 57 - Wizara limepokea uhamisho wa fedha za maendeleo kiasi cha **Shilingi 1,331,467,213,231.82** kwa ajili ya kugharamia shughuli mbalimbali. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 1,210,974,680,107.34** zimetolewa kugharamia mikataba ya ununuzi wa zana na vifaa kwa matumizi ya JWTZ kutoka kwa wazabuni mbalimbali. Vilevile, **Shilingi 117,692,467,011.00** kwa ajili ya kugharamia malipo ya deni la kimkataba na **Shilingi 2,980,066,113.12** zimepokelewa miundombinu wezeshi.

35. Mheshimiwa Spika, vilevile, Wizara imepokea uhamisho wa fedha kiasi cha **Shilingi 7,000,000,000.00** katika Bajeti ya Matumizi Mengineyo kwa ajili ya kugharamia malipo ya madeni ya huduma za matibabu kwa Hospitali ya Benjamin Mkapa Jijini Dodoma, *Muhimbili Orthopaedic Institute na Jakaya Kikwete Cardiac Institute* Jijini Dar es Salaam.

Fungu 38 - NGOME

36. Mheshimiwa Spika, Fungu 38 - NGOME limepokea uhamisho wa fedha za maendeleo wenye jumla ya **Shilingi 20,272,046,086.54** kugharamia ununuzi wa vifaa vya mawasiliano vya JWTZ na kugharamia Mradi wa ujenzi wa Jengo la mahafali, Mlango Mkuu na Uzio katika Chuo cha Taifa cha Ulinzi (National Defence College - NDC Tanzania). Vilevile, limepokea uhamisho wa fedha wenye jumla ya **Shilingi 56,132,873,378.00** za Matumizi

19 MEI, 2026

Mengineyo. Fedha hizo zimetumika kugharamia Operesheni maalumu.

Shughuli zilizotekelezwa kwa Fedha za Matumizi ya Kawaida

37. Mheshimiwa Spika, fedha zilizotolewa kwa ajili ya kutekeleza shughuli za kawaida katika Mwaka wa Fedha 2025/26, zimetumika katika maeneo yafuatayo:

Mafunzo na Mazoezi ya Kijeshi

38. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuratibu na kusimamia mafunzo mbalimbali ya kijeshi kwa maafisa na askari katika shule na vyo vya kijeshi ndani na nje ya Nchi. Katika Mwaka wa Fedha 2025/26, Wizara kupitia JWTZ imeendelea kufanya mazoezi na Nchi rafiki. Mwaka wa Fedha 2025/26 Jeshi lilifanya zoezi lililoshirikisha kamandi za anga za majeshi ya Nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC). Aidha, JWTZ ilifanya Zoezi la Ushirikiano Imara lililoshirikisha majeshi ya Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC). Mazoezi hayo yameimarisha ushirikiano, mshikamano na utayari kwa majeshi ya Nchi wanachama katika kukabiliana na changamoto za kiusalama ikiwemo ugaidi, uharamia na kukabiliana na majanga.

39. Mheshimiwa Spika, Mafunzo mbalimbali yanaendelea kutolewa kwa maafisa na askari ndani na nje ya Nchi, ili kuiwezesha JWTZ kutekeleza majukumu yake ya kulinda Nchi na mipaka yake kwa ufanisi, kulingana na kasi ya mabadiliko ya sayansi na teknolojia.

Matengenezo na Matunzo ya Zana na Vifaa vya Kijeshi

40. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia JWTZ imeendelea na programu za kuhakikisha mitambo, magari, zana na vifaa vya kijeshi vinakuwa katika hali nzuri ya kiutendaji, hii ni pamoja na kuvifanyia matengenezo pale inapohitajika. Aidha, kupitia TATC, kituo hicho kinaendelea na tafiti ambazo zimetumika kuwezesha kufanya maboresho ya mitambo, magari, zana na vifaa vilivyopo nchini.

19 MEI, 2026

Mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa

41. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) imeendelea kuwapatia vijana wa Kitanzania mafunzo ya awali ya Kijeshi na stadi za kazi kwa ajili ya kuwajengea uzalendo, umoja wa kitaifa, na uwezo wa kujitegemea. Mafunzo haya hufanyika katika makundi mawili ambayo ni Kundi la Kujitolea na Kundi la Lazima kwa vijana wanaohitimu Kidato cha Sita kwenye kambi mbalimbali za JKT.

42. Mheshimiwa Spika, Katika Mwaka wa Fedha 2025/26 mafunzo yamefanyika kupitia **Operesheni Nishati Safi**, ambapo jumla ya vijana **34,000** wa Kundi la Lazima walipatiwa mafunzo. Kati yao wavulana ni **25,469** na wasichana ni **8,531**. Vilevile, katika Mwaka wa Fedha 2024/25 yamefanyika mafunzo kwa Kundi la Kujitolea kupitia Operesheni **Miaka 60 ya Muungano** ambapo jumla ya vijana **12,000** wamepatiwa mafunzo. Kati yao wavulana ni **8,536** na wasichana ni **3,464**. Aidha, katika mwaka wa fedha 2025/26 jumla ya vijana 12,000 wa kujitolea **Operesheni Nishati Safi** wanaendelea na mafunzo ambapo kati yao wavulani ni **7,972** na wasichana ni **4,028**.

43. Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha wahitimu wote wa Kidato cha Sita wanapata fursa ya kujiunga na mafunzo ya JKT, miundombinu ya kambi imeendelea kuboreshwa, ambapo hadi kufikia Mwaka wa Fedha 2025/26 ina uwezo wa kuchukua vijana zaidi ya **60,000**. Mpango uliopo ni kuendelea kuboresha miundombinu na kufungua kambi mpya, ili kuiwezesha JKT kuchukua vijana **140,000** ifikapo Mwaka 2031, na hatimaye kuwezesha wahitimu wote wa Kidato cha Sita kupata fursa ya kujiunga na mafunzo ya JKT.

44. Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii kulitaarifu Bunge lako Tukufu pamoja na umma wa Tanzania kwamba, mafunzo yanayotolewa kwa vijana wa JKT yameendelea kuwajengea uzalendo, ukakamavu, umoja wa kitaifa, kuwapatia stadi za kazi katika nyanja mbalimbali na stadi za maisha, ili wakimaliza mafunzo ya JKT waweze kurejea katika jamii wakiwa raia wema wenye uwezo wa kujitegemea na kulilinda Taifa. Nitoe

rai kwa vijana wote wanaopata fursa ya mafunzo hayo, kuwa raia wema na kuzitumia stadi walizozipata kujijiri na kujitegemea.

Kilimo cha Kimkakati

45. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia JKT imeendelea kutekeleza Mpango Mkakati wa Mageuzi ya Kilimo Ndani ya JKT (2019/20 – 2027/28) unaolenga kuongeza uzalishaji wa mazao na kujitosheleza kwa chakula, ili kuipunguzia Serikali gharama za kulisha vijana wanaohudhuria mafunzo ya JKT na kuchangia katika usalama wa chakula kwa Taifa. Kupitia Mpango huo, JKT imeendeleza ujenzi wa skimu ya umwagiliaji Chita ambapo hadi sasa ekari 2,500 kati ya 12,000 zimejengewa miundombinu ya umwagiliaji. Aidha, katika Msimu wa Kilimo 2024/25, zimezalishwa tani 1,962.2 za Mpunga, tani 5,864 za Mahindi, tani 6.52 za Maharage na tani 48 za Alizeti.

Mafunzo kwa Jeshi la Akiba

46. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia JWTZ imeendelea kutoa mafunzo kwa Jeshi la Akiba katika mikoa yote ya Tanzania. Mafunzo haya husimamiwa na ofisi za washauri wa Jeshi la Akiba katika mikoa yote kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI. Lengo ni kuelimisha wananchi juu ya umuhimu wa masuala ya Ulinzi, na kuwajengea uwezo katika kulitumikia Taifa lao. Katika Mwaka wa Fedha 2025/26 jumla ya wananchi **14,899** walihitimu mafunzo, ambapo kati yao wanaume ni **12,280** na wanawake ni **2,619**. Niwapongeze wahitimu wote na kuwataka waendeleo kuviishi viapo vyao vya kulinda raia, kutetea uhuru na uchumi wa Nchi, pamoja na kutii sheria. Nitoe shukrani kwa Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI kwa ushirikiano wanaotupatia katika kuratibu mafunzo haya muhimu.

Huduma za Afya na Tiba

47. Mheshimiwa Spika, Katika kipindi husika, Wizara kupitia JWTZ imeendelea kutoa huduma za matibabu kwa maafisa, askari, watumishi wa umma, na familia zao pamoja na wananchi. Katika kuboresha huduma za afya, juhudi mbalimbali zimefanyika ikiwemo ujenzi wa Hospitali Kuu ya Rufaa ya Jeshi Dodoma

19 MEI, 2026

unaoendelea kwa awamu, ambapo Awamu ya Kwanza hadi ya Nne zimekamiliwa. Kwa sasa, Awamu ya Tano inaendelea kwa ujenzi wa *Diagnostic Radiology Centre* na ununuzi wa vifaa tiba ili Hospitali ianze kutoa huduma.

48. Mheshimiwa Spika, JWTZ imeboresha upatikanaji wa huduma muhimu katika Hospitali Kuu ya Jeshi Lugalo, zikiwemo za usafishaji wa figo, uchunguzi na matibabu ya magonjwa ya moyo. Hospitali zote za kanda za Jeshi zina vifaa vya kisasa vya kutolea huduma za kibingwa vikiwemo vya kuhudumia wagonjwa mahututi. Pia, zinatoa huduma ya vipimo vya *Advanced Ultrasound* na *Digitalized X – Ray*. Vilevile, huduma katika vituo vya tiba vikosini zinaendelea kuboreshwa, kwa vituo hivyo kupatiwa vifaa tiba, kuongezewa madaktari na kutumia mifumo ya TEHAMA.

Stahiki kwa Wanajeshi na Watumishi wa Umma

49. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kutoa stahiki mbalimbali kwa wanajeshi na watumishi wa umma, ikiwemo mishahara na malipo ya likizo. Vilevile, imeendelea kugharamia mafunzo mbalimbali ya kitaalam kuwawezesha watumishi kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu yao.

Ushirikiano na Mamlaka za Kiraia katika shughuli mbalimbali

50. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia JWTZ imeendelea kushirikiana na Mamlaka za Kiraia, kupitia huduma za moja kwa moja na miradi ya maendeleo. Mbali na jukumu la msingi la ulinzi wa mipaka ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, JWTZ ina jukumu la kisheria la kusaidia Mamlaka za Kiraia wakati wa majanga au uhitaji wa dharura. Katika Mwaka wa Fedha 2025/26, Jeshi limeimarisha utayari wa kukabiliana na dharura na limeshiriki katika usafirishaji wa chakula wakati wa mafuriko katika Nchi ya Msumbiji kuanzia tarehe 17 hadi 24 Machi, 2026. Vilevile, Wizara kupitia JWTZ imeendelea kushiriki katika ulinzi wa miradi ya kimkakati ikiwemo Reli ya kisasa (SGR), Mradi wa Kufua Umeme wa Maji wa Julius Nyerere (JNHPP), Mgodhi wa Tanzanite, Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP), Daraja la Kigongo - Busisi, Bandari, Mkongo wa Taifa, na maeneo ya

viwanja vya ndege. Jeshi lipo tayari kushirikiana na Mamlaka za Kiraia muda wote litakapohitajika.

Ushiriki katika Michezo Kitaifa na Kimataifa

51. Mheshimiwa Spika, Wizara ya Ulinzi na JKT inatambua vema mchango wa michezo kwa ustawi wa Wanajeshi wetu. Hivyo, katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2025/26, Wizara imeiwezesha JWTZ kushiriki kwa mafanikio katika michezo mbalimbali ikiwemo Mpira wa miguu, Riadha, Ngumi, Pool table na Kuogelea. Aidha, naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu japo kwa uchache baadhi ya mafanikio ambayo Wizara kupitia JWTZ imeyapata katika michezo hiyo.

52. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mpira wa miguu, Wizara ina timu mbili za wanaume zinazoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara (NBC Premier League). Timu hizo ni Mashujaa FC na JKT Tanzania ambazo zinamilikiwa na JWTZ na JKT mtawalia. Vilevile, JWTZ ina timu nne zinazoshiriki Ligi Daraja la Kwanza (Championship). Timu hizo ni TMA Stars, Mbuni Football Club, Transit Camp na Gunners, ambazo zinafanya vizuri katika Ligi hiyo, na ni matumaini yangu zitapanda daraja na hivyo kuongeza timu za Jeshi zinazoshiriki Ligi Kuu.

53. Mheshimiwa Spika, Wizara ina timu mbili za mpira wa miguu wa wanawake ambazo zinashiriki katika mashindano ya ligi kuu ya kitaifa. Timu hizo ni JKT Queens na Mashujaa Queens ambazo zinamilikiwa na JKT na JWTZ mtawalia. Aidha, nina furaha kuwajulisha kuwa JKT Queens ni mabingwa wa Council for East and Central Africa Football Associations (CECAFA) kwa mwaka 2025, ilitwaa ubingwa huo baada ya kuwafunga Rayon Sports ya Rwanda katika mchezo uliofanyika tarehe 16 Septemba, 2025. Ushindi huu uliwezesha Timu hiyo kufuzu kuwakilisha Ukanda wa Afrika Mashariki kwenye Klabu Bingwa ya Afrika Mwaka 2025.

54. Mheshimiwa Spika, Wizara katika mwaka wa Fedha 2025/26, imeshiriki katika mashindano ya Mei Mosi yaliyofanyika mkoani Njombe na kuwa mshindi wa kwanza wa jumla katika michezo mbalimbali. Aidha, Shirika la Mzinga limeshiriki katika Mashindano ya Shirikisho la Michezo la Mashirika ya Umma, Taasisi na

19 MEI, 2026

Makampuni Binafsi Tanzania (SHIMMUTA), yaliyofanyika mkoani Morogoro kuanzia tarehe 25 Novemba hadi 06 Desemba, 2025 na limeweza kushika nafasi ya kwanza kwa mshindi wa jumla katika michezo hiyo.

55. Mheshimiwa Spika, katika mchezo wa riadha, Sajini Taji Alphonse Felix Simbu amekuwa Bingwa wa Dunia wa mashindano ya Riadha ya Dunia (*World Athletics Championship 2025*) Tokyo Japan yaliyofanyika tarehe 15 Septemba, 2025 na kuwa Mtanzania wa kwanza kupata Medali ya Dhahabu katika mashindano hayo. Vilevile, katika mashindano ya Boston Mararthon yaliyofanyika nchini Marekani tarehe 20 Aprili, 2026 alishika nafasi ya pili na kupewa Medali ya Fedha. Aidha, wanariadha wengine walioshinda ni pamoja na **Sajini Secilia Ginoka Panga** mshindi wa kwanza katika mbio za kimataifa za Sao Silvester zilizofanyika nchini Brazil tarehe 31 Desemba, 2025 na kufanikiwa kupata Medali ya Dhahabu, **Koplo Magdalena Crispin Shauri** mshindi wa kwanza katika mbio za kimataifa za Al Shargiyal (Shargiyal International Half Marathon) zilizofanyika nchini Saudi Arabia tarehe 21 Januari, 2026 na kupata Medali ya Dhahabu, na **Praiveti Sinda Godfrey Sinda** mshindi wa pili katika mbio za kimataifa za CPC Loop Den Haag zilizofanyika nchini Uholanzi tarehe 15 Machi, 2026 na kufanikiwa kupata Medali ya Fedha.

56. Mheshimiwa Spika, katika mashindano ya Pool table Barani Afrika yaliyofanyika Durban nchini Afrika Kusini, Mwezi Februari 2026 Mtumishi wa Umma **Bi. Rosemary Deus Kazaura** alishiriki na kuwa mchezaji bora na kupata Medali ya Dhahabu. Aidha, ushiriki wa JWTZ katika mashindano mbalimbali umekuwa na mafanikio kutokana na maandalizi mazuri ya timu pamoja na uwezeshwaji unaofanywa na Wizara kupitia JWTZ. Mbali na kujenga ukakamavu kimwili kwa wanajeshi, michezo inasaidia kujenga mahusiano mazuri kwa wananchi na majeshi mengine.

57. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mchezo wa ngumi, mabondia wa JWTZ wanaume na wanawake wameendelea kufanya vizuri katika mashindano mbalimbali ya ndani na nje ya Nchi. Katika maadhimisho ya miaka 50 ya Uhuru wa Nchi ya Comoros yaliyofanyika tarehe 06 Julai, 2025, mabondia **Koplo Ezra**

19 MEI, 2026

Mwanjwango na **Praiveti Kassim Mbundikwa** walishinda Medali ya Dhahabu.

58. Mheshimiwa Spika, pia Wizara imeshiriki katika michezo mingine ndani na nje ya nchi ikiwemo mpira wa magongo, vishale (darts), mpira wa wavu (volleyball), mpira wa pete (netball), mpira wa kikapu (Basketball) na Golf. Katika michezo hiyo, timu zetu zilifanya vizuri. Ushiriki na ushindi wa wanamichezo wetu katika mashindano haya, umeweza kuliletea Taifa letu medali, heshima pamoja na kuimarisha mahusiano na ushirikiano na nchi rafiki. Napenda kutumia fursa hii, kuwapongeza washindi wote.

59. Mheshimiwa Spika, napenda kutumia nafasi hii kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu kwa kutunukiwa Nishani ya juu ya heshima ya Baraza la Michezo ya Majeshi Duniani (CISM) ijulikanayo kama *THE GRAND CORDON* tarehe 14 Agosti, 2025 kwa mchango mkubwa wa kufikia malengo ya CISM. Vilevile, nawapongeza viongozi wote wa JWTZ kwa kutoa uzito katika michezo na kuunga mkono maono ya Rais na Amiri Jeshi Mkuu kwa kuimarisha miundombinu ya michezo.

60. Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee, kupitia Bunge lako Tukufu napenda kumpongeza **Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu, kwa mchango wake ulioweza wanamichezo wetu kupata mafanikio makubwa ndani na nje ya Nchi na kuliletea sifa na heshima Taifa letu.

61. Mheshimiwa Spika, napenda pia, kutoa taarifa kuwa katika hafla ya utoaji wa Tuzo za Baraza la Michezo Tanzania 2026 iliyofanyika tarehe 09 Mei, 2026, **Sajini Taji Alphonse Felix Simbu** alitangazwa kuwa Mwanamichezo Bora wa Kiume, **Praiveti Stumai Abdallah** Mwanamichezo Bora wa Kike ambaye ni mchezaji wa JKT Queens na Timu ya Taifa ya Wanawake, **Mteule Daraja la Kwanza Anthony Mwingereza (Mstaafu)** Kocha Bora kwa upande wa wanaume na **Klabu ya JKT Queens** ilitangazwa kuwa Klabu Bora kwa upande wa wanawake kutokana na mafanikio makubwa iliyoyapata katika mashindano mbalimbali.

Masuala Mtambuka

62. Mheshimiwa Spika, Wizara pamoja na taasisi zilizo chini yake imeendelea kuzingatia masuala mtambuka katika utekelezaji wa shughuli zake kwa kutumia Bajeti ya Matumizi ya Kawaida. Masuala hayo yanajumuisha mapambano dhidi ya magonjwa ambukizi na sugu yasiyoambukiza, utawala bora na mazingira.

Mapambano dhidi ya magonjwa ambukizi na sugu yasiyoambukiza

63. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2025/26, Wizara imeendelea kutekeleza mikakati ya kupambana na maambukizi mapya ya Virusi vya UKIMWI na Magonjwa Sugu yasiyoambukiza. Mikakati hiyo inajumuisha kuhamasisha watumishi kupima ili kufahamu hali za afya zao. Aidha, Wizara imeendelea kutoa huduma ya lische kwa watumishi wanaoishi na Virusi vinavyosababisha Upungufu wa Kinga Mwilini. Hatua hizi zinachukuliwa kwa kuzingatia Mwongozo wa Udhhibiti VVU na UKIMWI mahali pa kazi.

Utawala Bora

64. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuimarisha Utawala Bora kwa kuzingatia miongozo ya kupambana na rushwa, sheria za matumizi ya fedha na ununuzi, ambapo taarifa za ukaguzi na ununuzi zimekuwa zikiandaliwa na kuwasilishwa kwenye mamlaka husika.

65. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2025/26 Wizara pamoja na taasisi zilizo chini yake imeendelea na jitihada mbalimbali ili kuimarisha Utawala Bora kwa kuzingatia sheria za matumizi ya fedha na ununuzi, kuhakikisha matumizi ya fedha na ununuzi yanafanyika kwa ufanisi, kuzingatia thamani ya fedha na kaguzi kufanyika ipasavyo. Katika taarifa ya Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya Mwaka wa Fedha 2024/25, Wizara na taasisi zilizo chini yake imeendelea kupata Hati Inayoridhisha (Safi) ya Ukaguzi.

66. Mheshimiwa Spika, taarifa za kila Robo Mwaka huwasilishwa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Vilevile, semina mbalimbali kuhusu jinsi ya kupambana na kuzuia rushwa mahala pa kazi zimeendelea kutolewa kwa watumishi. Wizara imekuwa ikishirikisha watumishi katika kutoa maoni na ushauri kupitia vikao mbalimbali, hususan Baraza la Wafanyakazi, Kamati ya Maadili na Kamati ya Ajira. Pia, Wizara inaendelea kutoa huduma bora kwa wateja kwa kuzingatia sheria, kanuni na miongozo mbalimbali.

Utunzaji wa Mazingira

67. Mheshimiwa Spika, Wizara imechukua hatua mahususi ili kutimiza Azma ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya utunzaji wa mazingira na matumizi ya nishati safi. Katika kipindi husika kupitia taasisi zilizo chini yake, imeendelea na utunzaji wa mazingira katika maeneo yake yenye miti ya asili, kwa kulinda maeneo hayo yasivamiwe kwa shughuli za kijamii, na kuendelea kupanda miti mipya. Katika Mwaka wa Fedha 2025/26 Wizara na taasisi zake imeweza kupanda miti mipya **209,794** katika kambi mbalimbali za Jeshi. Vilevile, Wizara imeendelea na upimaji na uwekaji wa alama za mipaka katika maeneo ya Jeshi yakiwemo yenye misitu na ardhi oevu. Hatua hii imepunguza uvamizi, uharibifu wa mazingira na migogoro ya ardhi inayotokana na shughuli za kibinadamu zikiwemo uchomaji mkaa, ukataji miti, uchimbaji madini, kilimo na ufugaji.

68. Mheshimiwa Spika, kuhusu matumizi ya nishati safi JWTZ na kambi zake zinazolisha zaidi ya watu 100 yamefikia asilimia 92 ya matumizi ya nishati safi ya kupikia, JKT imefikia asilimia 100, Shirika la Mzinga asilimia 98, na Shirika la *Tanzania Automotive Technology Center* (TATC) asilimia 98. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Wakala wa Nishati Vijijini (REA) imetekeleza mkakati wa matumizi ya nishati safi ya kupikia katika kambi zote za JKT. Vilevile, shughuli zilizotekelezwa hadi hivi sasa ni kutengeneza mashine za kuzalisha mkaa mbadala, utengenezaji wa miundombinu ya mitambo ya gesivunde (biogas plant) katika baadhi ya vikosi vya JKT na kufundisha vijana kutengeneza mkaa banifu katika kambi zote za JKT.

Shughuli zilizotekelezwa kwa kutumia Fedha za Maendeleo

69. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2025/26, Fungu 57 - Wizara imetumia fedha za maendeleo kutekeleza shughuli mbalimbali zifuatazo:

- a. Kugharamia malipo ya mikataba mbalimbali ya ununuzi wa zana na vifaa kwa matumizi ya JWTZ;
- b. Utafiti wa uhuishaji wa silaha, zana na vifaa kwa matumizi ya Jeshi;
- c. Ununuzi wa mitambo na malighafi za kuzalisha mazao ya msingi kwa Shirika la Mzinga;
- d. Kufanya maboresho ya vifaa vya ulinzi wa anga;
- e. Kutekeleza shughuli za utafiti na uhawilishaji wa teknolojia katika Shirika la TATC;
- f. Kugharamia maboresho, huduma ya ulinzi na malipo ya huduma ya umeme kwenye minara ya Mawasiliano Salama Jeshini;
- g. Kugharamia ufuatiliaji na tathmini wa miradi na shughuli mbalimbali za Wizara; na
- h. Kulipa fidia ya ardhi katika maeneo yaliyofanyiwa uthamini, kama inavyoonekana katika **Jedwali Na 4**.

Jedwali Na. 4: Maeneo Yaliyolipwa Fidia ya Ardhi kuanzia Julai 2025 hadi Aprili 2026

| Na | Eneo | Mkoa | Kiasi kilicholipwa (Shs) |
|-----------|--|-------------|---------------------------------|
| 1. | Fidia kwa wananchi 989 eneo la Mboghwe - Nzega. | Tabora | 4,869,631,375.08 |
| 2. | Fidia ya wananchi 121 eneo la Pongwekiona – Chalinze. | Pwani | 4,180,632,171.00 |
| 3. | Fidia ya wananchi 34 eneo la Buhale – Musoma. | Mara | 278,427,710.83 |
| 4. | Fidia ya mwananchi mmoja eneo la Buhongwa - Nyamagana. | Mwanza | 18,639,400.00 |

19 MEI, 2026

| | | | |
|--------------|--|---------|--------------------------|
| 5. | Fidia ya wananchi 10 eneo la Rasi Nondwa - Kasulu. | Kigoma | 733,602,415.00 |
| 6. | Fidia ya wananchi wawili eneo la Chungu – Ikungi. | Singida | 10,840,767.00 |
| 7. | Fidia ya mwananchi mmoja eneo la Bweni - Pangani | Tanga | 2,000,000,000.00 |
| Jumla | | | 12,091,773,838.91 |

70. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2025/26, Fungu 38: NGOME limetumia fedha za maendeleo kutekeleza shughuli mbalimbali zifuatazo:

- a. Kugharamia ununuzi wa risasi, mabomu na milipuko kwa ajili ya mafunzo, oparesheni na mazoezi;
- b. Kuendeleza ujenzi wa Shule ya Polisi Jeshi Mafinga mkoani Iringa;
- c. Kuendeleza ujenzi wa Makao Makuu ya Kamandi ya Jeshi la Anga;
- d. Umaliziaji wa Ujenzi wa Ukumbi SKUA – Tanga;
- e. Ujenzi wa Makao Makuu ya Kamandi ya Jeshi la Akiba; na
- f. Kugharamia uboreshaji wa miundombinu ya vyuo, shule na vikosi.

71. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2025/26, Fungu 39: JKT limetumia fedha za maendeleo kutekeleza miradi ifuatayo:

- a. Kuendeleza ujenzi wa Kikosi kipya cha Tanganyika;
- b. Kumalizia ujenzi wa majengo ya Makao Makuu ya JKT;
- c. Ujenzi wa mahanga katika Kiteule cha Chenene - Kikosi cha Makutupora JKT; na
- d. Kuendeleza ujenzi wa Skimu ya umwagiliaji Chita, Morogoro na kuanzisha ujenzi wa Skimu ya umwagiliaji katika Kiteule cha Chenene - Kikosi cha Makutupora JKT- Dodoma.

72. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia mashirika yake ya Tanzania Automotive Technology Centre (TATC), Mzinga, na

19 MEI, 2026

Shirika la Uzalishaji Mali la Jeshi la Kujenga Taifa (SUMAJKT) imeendelea kutekeleza majukumu yake ifuatavyo:

Tanzania Automotive Technology Centre

73. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2025/26, Shirika la *Tanzania Automotive Technology Centre* (TATC) liliidhinishiwa fedha kiasi cha **Shilingi 15,000,000,000.00** kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Hadi kufikia Mwezi Aprili 2026, limepokea **Shilingi 5,500,000,000.00** sawa na **asilimia 36.67**. Fedha hizo zimetumika kugharamia: ukamilishaji wa miundombinu ya Jengo, ununuzi wa mashine na mitambo kwa ajili ya Karakana ya *Grey and ductile Iron*; ununuzi wa malighafi na mitambo kwa ajili ya kukamilisha Mradi wa *Cupola Furnace*; ukarabati wa miundombinu ya milki; na kuendeleza tafiti za teknolojia ya magari na bidhaa za viwandani.

74. Mheshimiwa Spika, aidha, Shirika la TATC limekamilisha taratibu za kuingia ubia kwa ajili ya kuanzisha kiwanda cha kuunganisha magari na kampuni ya *STREIT Group* kutoka Umoja wa Nchi za Falme za Kiarabu (UAE). Manufaa yatakayopatikana kutokana na ubia huu ni kuongeza mtaji, kuongeza ajira, kupata teknolojia na kuimarisha uwezo wa kuunda magari ya Deraya na kiraia.

Shirika la Mzinga

75. Mheshimiwa Spika, katika Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2025/26, Shirika la Mzinga liliidhinishiwa fedha kiasi cha **Shilingi 6,000,000,000.00** kwa ajili ya kutekeleza shughuli za maendeleo. Hadi kufikia mwezi Aprili 2026, Shirika limepokea **Shilingi 4,674,582,595.94** sawa na **asilimia 77.91**. Fedha hizo zimetumika kugharamia ununuzi wa mashine na malighafi kwa ajili ya uzalishaji wa mazao ya msingi. Aidha Shirika katika kuongeza uzalishaji wa mazao ya msingi kwa ajili ya JWTZ na vyombo vingine vya ulinzi na usalama lipo katika mchakato wa kuanzisha kiwanda kipywa (Mzinga II) ambapo hatua iliyofikiwa sasa ni kuandaliwa kwa Mkataba kati Shirika na Mzabuni.

19 MEI, 2026

Shirika la Uzalishaji Mali la Jeshi la Kujenga Taifa

76. Mheshimiwa Spika, katika Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2025/26, Shirika la Uzalishaji Mali la Jeshi la Kujenga Taifa (SUMAJKT) liliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 2,000,000,000.00** kwa ajili ya kugharamia ununuzi wa mitambo. Hadi kufikia mwezi Aprili 2026 Shirika limepokea kiasi kilichoidhinishwa, ambacho kimetumika kugharamia ununuzi wa mitambo na zana za kilimo kwa ajili ya kuongeza uzalishaji wa mazao mbalimbali.

77. Mheshimiwa Spika, kwa kutumia vyanzo vya ndani vya mapato, Shirika limeendelea na shughuli za uzalishaji mali kupitia kampuni tanzu na viwanda vyake, ili kuchangia katika uchumi wa Nchi na kuipunguzia Serikali gharama za malezi ya vijana wanaojiunga na mafunzo ya JKT. Shughuli hizo zinatekelezwa kupitia sekta za ujenzi, viwanda, biashara na huduma, kilimo, mifugo na uvuvi pamoja na elimu.

F. USHIRIKIANO WA KIULINZI KIKANDA NA KIMATAIFA

Ushirikiano na Nchi nyingine

78. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuimarisha ushirikiano wa kikanda na kimataifa, kwa kushiriki vikao vya kikanda na kimataifa katika kuimarisha ulinzi na usalama duniani.

79. Mheshimiwa Spika, vilevile, Wizara kupitia JWTZ imeendelea kushirikiana na Nchi rafiki katika masuala ya ulinzi na usalama kwenye maeneo mbalimbali, ikiwemo mafunzo, mazoezi na misaada ya kitaalamu. Pia, tumeendelea kushirikiana na Umoja wa Mataifa (UN), Umoja wa Afrika (AU), Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), na Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) katika mafunzo, mazoezi, ubadilishanaji wataalamu na taarifa, na kufanya operesheni mbalimbali. Nchi hizo ni pamoja na Afrika Kusini, Angola, Algeria, Brazil, Bangladesh, Botswana, Burundi, Canada, Comoros, China, Cuba, DRC, Ethiopia, Falme za Kiarabu, Finland, Ghana, Hispania, India, Indonesia, Israel, Jamhuri ya Czech, Jordan, Kenya, Malawi, Marekani, Misri, Morocco, Msumbiji, Nigeria, Oman, Kuwait, Pakistan, Rwanda, Sri Lanka,

19 MEI, 2026

Sweden, Ufaransa, Uganda, Uholanzi, Uingereza, Ujerumani, Urusi, Uturuki, Uswisi, Zambia na Zimbabwe.

Mafunzo ya Usalama na Stratejia

80. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Chuo cha Taifa cha Ulinzi - Tanzania (NDC - Tanzania) imeendelea kutoa mafunzo ya Usalama na Stratejia kwa maafisa waandamizi wa vyombo vya ulinzi na usalama pamoja na Utumishi wa Umma. Mafunzo yanayotolewa na Chuo hiki ni ya uongozi katika ngazi ya Kisera na Kistratejia. Katika mafunzo hayo tunashirikiana na Nchi mbalimbali ambazo ni pamoja na Afrika Kusini, Bangladeshi, Botswana, Burundi, China, Ethiopia, India, Kenya, Malawi, Misri, Namibia, Nigeria, Rwanda, Sierra Leone, Uganda, Zambia na Zimbabwe.

81. Mheshimiwa Spika, Nchi rafiki zinazoleta viongozi wake kupata Mafunzo Chuo cha Taifa cha Ulinzi – Tanzania inaonesha ubora na viwango vya kimataifa vya Mtaala, uhusiano mzuri na mataifa hayo, na mchango wa Tanzania katika kuandaa viongozi katika Usalama na Stratejia kitaifa, kikanda na kimataifa. Kupitia Mafunzo haya, Wizara inashiriki moja kwa moja katika utekelezaji wa Diplomasia ya Ulinzi na ujenzi wa Ushirikiano wa Kimataifa wenye tija na Nchi rafiki; masuala ambayo yanaendelea kuimarishwa na Serikali ya Awamu ya Sita.

82. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2025/26, Chuo kimeendesha mafunzo kwa viongozi waandamizi wa Serikali na Sekta Binafsi kuanzia tarehe 09 - 13 Machi, 2026. Mada kuu ya Kozi hii ilikuwa “**Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi katika Kuchochea Maendeleo Endelevu ya Taifa,**” (Public Private Partnership (PPP) for Sustainable National Development). Washiriki wa Kozi hii walikuwa ni baadhi ya makatibu wakuu na naibu makatibu wakuu wa wizara, watendaji wakuu wa taasisi za umma, watendaji wakuu wa taasisi za binafsi, viongozi kutoka Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, na maafisa kutoka vyombo vya ulinzi na usalama.

83. Mheshimiwa Spika, pia, Chuo cha Ukamanda na Unadhimu (CSC) na Chuo cha Mafunzo ya Kijeshi Monduli (TMA) Arusha

19 MEI, 2026

vimeendelea kuendesha mafunzo kwa kushirikiana na Nchi mbalimbali. Mafunzo hayo yameendelea kuimarisha uhusiano na diplomasia ya ulinzi.

Ushiriki wa JWTZ katika Ulinzi wa Amani

84. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia JWTZ imeendelea kushirikiana na Jumuiya za Kimataifa na Kikanda katika operesheni za ulinzi wa amani chini ya Umoja wa Mataifa na Umoja wa Afrika. Kwa sasa JWTZ ina vikundi vya ulinzi wa Amani katika Nchi za DRC (MONUSCO), Jamhuri ya Afrika ya Kati (MINUSCA) na Lebanoni (UNIFIL). Kwa ujumla hali ya usalama wa vikundi hivyo vinavyoshiriki Ulinzi wa Amani ni shwari na vinaendelea kutekeleza majukumu yake kwa weledi. Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inaendelea kuboresha hali ya zana na vifaa kwa JWTZ na katika vikundi vinavyoshiriki katika majukumu ya Ulinzi wa Amani ili kuimarisha zaidi utendaji kazi.

G. MPANGO NA MWELEKEO WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2026/27

85. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2026/27, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa imelenga kutekeleza Mpango na Bajeti kwa kuzingatia Dira na Dhima ya Wizara, Dira ya Maendeleo ya Taifa 2050, Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2026/27 – 2030/31), Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030 (SDGs), Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025, Mpango Mkakati wa Wizara (2026/27 – 2030/31) na Taasisi zake na Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2026/27.

86. Mheshimiwa Spika, naomba uniruhusu kuwasilisha Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2026/27 ifuatavyo:

Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli

87. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2026/27, Wizara inatarajia kukusanya maduhuli ya jumla ya **Shilingi 90,603,000.00** kutoka katika mafungu yake matatu. Fungu 38 - NGOME

19 MEI, 2026

linatarajia kukusanya kiasi cha **Shilingi 22,000,000.00**, Fungu 39 - JKT linatarajia kukusanya kiasi cha **Shilingi 67,403,000.00** na Fungu 57 - Wizara inatarajia kukusanya kiasi cha **Shilingi 1,200,000.00** kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 5**.

Jedwali Na. 5: Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2026/27

| Na. | Fungu | Makadirio ya Maduhuli 2026/27 (Shs) |
|--------------|--------------|--|
| 1. | 38 – NGOME | 22,000,000.00 |
| 2. | 39 – JKT | 67,403,000.00 |
| 3. | 57 – Wizara | 1,200,000.00 |
| Jumla | | 90,603,000.00 |

Matumizi ya Kawaida na Maendeleo

88. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2026/27, Serikali inatarajia kutenga fedha kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Maendeleo jumla ya **Shilingi 4,286,489,324,427.00** ambapo kati ya fedha hizo, **Shilingi 3,859,955,671,427.00** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida, na **Shilingi 426,533,653,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi ya Maendeleo.

89. Mheshimiwa Spika, kati ya Fedha hizo, Fungu 38 - NGOME linatarajia kutengewa **Shilingi 3,198,126,934,000.00** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 54,867,636,000.00** kwa ajili ya Matumizi ya Maendeleo. Fungu 39 - JKT linatarajia kutengewa **Shilingi 626,273,760,000.00** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 19,929,926,000.00** kwa ajili ya Matumizi ya Maendeleo. Fungu 57 - Wizara linatarajia kutengewa **Shilingi 35,554,768,000.00** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 351,736,091,000.00** kwa ajili ya Matumizi ya Maendeleo. Mchanganuo kwa kila Fungu ni kama ilivyoainishwa katika **Jedwali Na. 6**.

19 MEI, 2026

Jedwali Na. 6: Mchanganuo wa Bajeti kwa kila Fungu kwa Mwaka wa Fedha 2026/27

| Na | Fungu | Matumizi ya Kawaida (Shs) | Matumizi ya Maendeleo (Shs) | Jumla ya Fedha zitakazotengwa (Shs) |
|----|--------------|-----------------------------|-----------------------------|-------------------------------------|
| 1. | 38 – NGOME | 3,198,126,934,000.00 | 54,867,636,000.00 | 3,252,994,570,000.00 |
| 2. | 39 – JKT | 626,273,760,000.00 | 19,929,926,000.00 | 646,203,686,000.00 |
| 3. | 57 – Wizara | 35,554,768,000.00 | 351,736,091,000.00 | 387,290,859,000.00 |
| | Jumla | 3,859,955,462,000.00 | 426,533,653,000.00 | 4,286,489,115,000.00 |

90. Mheshimiwa Spika, shughuli zinazokusudiwa kutekelezwa katika Mwaka wa Fedha 2026/27 zitazingatia maeneo ya kipaumbele yafuatayo:

- a. Kuliimarisha Jeshi kwa zana na vifaa vya kisasa, kiteknolojia, mawasiliano na rasilimali watu;
- b. Kuendelea kuweka mazingira mazuri ya utendaji kazi kwa wanajeshi ikiwemo kutunza vifaa na zana, mazoezi, mafunzo, maslahi, huduma za afya na makazi;
- c. Kuendelea kuimarisha uwezo wa Jeshi la Kujenga Taifa kwa kuboresha miundombinu, ili liweze kuchukua vijana wengi zaidi watakaopata mafunzo ya awali ya kijeshi na stadi za kazi;
- d. Kuendelea kuliimarisha Jeshi la Akiba;
- e. Kuendeleza na kulinda miradi ya kimkakati kwa maslahi mapana ya Taifa;
- f. Kuimarisha mashirika na taasisi za utafiti wa masuala ya kijeshi, kuanzisha viwanda vipya katika Sekta ya Ulinzi (Defence industries) vitakavyozalisha bidhaa kwa matumizi ya Kijeshi na Kiraia. Pia, kuanzisha viwanda vipya kwa kushirikiana na Sekta Binafsi;
- g. Kuimarisha ushirikiano na Umoja wa Mataifa, Umoja wa Afrika, Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika, Jumuiya ya Afrika Mashariki na kati ya Nchi na Nchi katika masuala ya ulinzi; na
- h. Kuendelea kushirikiana na Mamlaka za kiraia katika kukabiliana na majanga na dharura inapohitajika.

H. SHUKRANI

91. Mheshimiwa Spika, kabla ya kuhitimisha Hotuba yangu, napenda kutumia fursa hii kuwashukuru viongozi na watendaji wa Wizara ninayoiongoza na taasisi zake kwa ushirikiano wanayoifanya, na wanaonipatia, michango kazi yao kubwa madhubuti iliyoweza kutekeleza Mpango na Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2025/26 kwa mafanikio na ushirikiano mkubwa katika kutayarisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2026/27 ninayoyawasilisha. Napenda kumshukuru **Dkt. Faraji Kasidi Mnyepe**, Katibu Mkuu wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, **Jenerali Jacob John Mkunda**, Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi, **Luteni Jenerali Salum Haji Othman**, Mnadhimu Mkuu wa Jeshi, **Meja Jenerali Rajabu Nduku Mabele**, Mkuu wa Jeshi la Kujenga Taifa, Wakuu wa Kamandi, Wakuu wa Matawi Makao Makuu ya Jeshi na JKT, Wakuu wa Mashirika, Wakuu wa Idara na Vitengo, Wakuu wa Vyuu, Shule na Vikosi vya Jeshi. Vilevile, nawashukuru maafisa, askari na watumishi wa umma kwa ushirikiano wanaonipatia. Mafanikio tuliyopata ni kutokana na bidii, nidhamu, uhodari na kujituma kwao.

92. Mheshimiwa Spika, naomba nitumie fursa hii, kwa niaba ya Serikali kutoa shukrani kwa washirika wa maendeleo na serikali za Nchi mbalimbali kwa ushirikiano wanaoendelea kuipatia Wizara ninayoiongoza. Washirika hao ni pamoja na Umoja wa Mataifa, Umoja wa Afrika, Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika, Jumuiya ya Afrika Mashariki, na Jumuiya ya Nchi za Ukanda wa Maziwa Makuu. Pia, tunazishukuru Nchi rafiki katika shughuli zetu za ulinzi ambazo ni pamoja na Afrika Kusini, Algeria, Angola, Bangladesh, Burundi, Jamhuri ya Watu wa China, Cuba, Jamhuri ya Czech, Ethiopia, Finland, Ghana, Hispania, India, Indonesia, Israel, Jordan, Kenya, Msumbiji, Kuwait, Malawi, Marekani, Misri, Morocco, Nigeria, Oman, Pakistan, Rwanda, Serbia, Sri Lanka, Sweden, Uganda, Ufaransa, Ujerumani, Uholanzi, Uingereza, Umoja wa Falme za Kiarabu, Urusi, Uswisi, Uturuki, Zambia na Zimbabwe.

93. Mheshimiwa Spika, naomba pia kuzishukuru wizara na taasisi zote, na wananchi wote kwa ushirikiano wanaoutoa kwa Wizara ya Ulinzi na JKT na taasisi zake katika ulinzi wa Nchi yetu. Ni

19 MEI, 2026

matumaini yangu kuwa tutaendelea kushirikiana zaidi kwa manufaa ya Taifa letu.

94. Mheshimiwa Spika, napenda kuishukuru familia yangu kwa uvumilivu na upendo wao mkubwa kwangu unaoniwezesha kutekeleza majukumu yangu kwa utulivu.

95. Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru wewe binafsi, Mawaziri wenzangu na Wabunge wote kwa kunisikiliza. Hotuba hii, inapatikana pia katika tovuti ya Wizara ya Ulinzi na JKT ambayo ni www.modans.go.tz

I. HITIMISHO

96. Mheshimiwa Spika, kwa Mwaka wa Fedha 2026/27, Wizara ya Ulinzi na JKT na taasisi zilizo chini yake inaliomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya **Shilingi 4,286,489,115, 000.00** kati ya fedha hizo, **Shilingi 3,859,955,462,000.00** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **Shilingi 426,533,653,000.00** ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo.

97. Mheshimiwa Spika, naomba kutoa Hoja.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaafiki.

(Hoja ilitolewa lamuliwe)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, hoja imetolewa na imeungwa mkono, tunakushukuru Mheshimiwa Waziri.

Sasa ninamwita Mheshimiwa Mwenyekiti, wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, Mheshimiwa Najma Giga.

MHE. NAJMA MURTAZA GIGA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa fursa hii. Kwanza kabisa sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ndiye muweza wa kila jambo katika ulimwengu wetu.

19 MEI, 2026

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaanza kusoma Taarifa yangu, ninaomba Taarifa yote ya Kamati kama ilivyoletwa na Kamati iweze kuingia kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 121 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2025, ninaomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2025/2026, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2026/2027 na pia kuliomba Bunge lako Tukufu liipokee taarifa hii na kuikubali, kisha kuidhinisha bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, msingi wa taarifa hii ni majukumu ya Kamati kwa mujibu wa Kifungu cha 6(3) na Kifungu cha 7(1)(a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge pamoja na masharti ya Kanuni ya 121(4) ya Kanuni za Bunge, kuwa kabla ya Taarifa ya Utekelezaji na Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kujadiliwa Bungeni, inapaswa kuchambuliwa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa, uchambuzi huo ulifanyika tarehe 26 Machi, 2026 baada ya ziara za ukaguzi wa miradi ya maendeleo inayotekelezwa chini ya Wizara hii kama ilivyoelekeza Kanuni ya 120(1) na 121(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuliwezesha Bunge lako Tukufu kufuatilia kikamilifu utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2025/2026, pamoja na kuishauri vyema Serikali kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka wa fedha 2026/2027, Taarifa hii imegawanyika katika sehemu kuu tano kama ifuatavyo: -

- (i) Sehemu ya kwanza; ni utangulizi ambao unaeleza kwa ujumla kuhusu msingi na muundo wa taarifa;

19 MEI, 2026

- (ii) Sehemu ya pili; ambayo inafafanua matokeo ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo uliofanyika kwa mujibu wa Kanuni ya 120(1) ya Kanuni za Bunge;
- (iii) Sehemu ya tatu hadi ya nne ambazo zinachambua utekelezaji wa mipango na Bajeti kwa mwaka wa fedha 2025/2026 pamoja na kuchanganua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2026/2027; na
- (iv) Sehemu ya tano inaonesha Maoni na Ushauri wa Kamati kutokana na matokeo ya uchambuzi. Aidha, sehemu hii inahitimisha Taarifa kwa shukurani na kubainisha msimamo wa jumla wa Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukaguzi wa miradi ya maendeleo; kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 121(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ilitembelea na kukagua Miradi ya Maendeleo katika Shirika la Mzinga, mkoani Morogoro. Fedha iliyoombwa kwa miradi iliyo chini ya Shirika la Mzinga inahusu ununuzi wa mashine za kisasa, vipuri na malighafi ili kuboresha mkondo wa uzalishaji wa mazao ya msingi. Fedha hiyo imeelekezwa pia kwenye ujenzi wa karakana na ukarabati wa majengo ya zamani na miundobinu yake, na vilevile kufanya utafiti na kutengeneza kifaa maalum yaani *portable launcher* kitakachotumika kurusha bomu baridi na kufukuza wanyama waharibifu kwenye makazi ya binadamu. Kamati ilitaarifiwa kuwa miradi hii yote imetekelezwa kwa utaratibu wa *Force Account*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jumla ya shilingi bilioni sita zilitolewa na hadi kufikia mwezi Machi, 2026 Wizara ilikuwa imepokea shilingi 4,674,582,594.94 sawa na 77.9% ya fedha iliyotengwa. Aidha, ilielezwa kwamba miradi hiyo inatarajiwa kukamilika kabla ya Juni, 2026 iwapo fedha zilizosalia zitapatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa taarifa za miradi wakati wa ziara ulionesha yafuatayo; hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa miradi ni wastani wa 90% ingawa fedha

19 MEI, 2026

zilizopokewa ni 77.9%. Matumizi ya fedha iliyopokelewa yalikuwa ni 100% ya fedha iliyopokelewa na 77.9% ya bajeti iliyotengwa, na sehemu ya matumizi ya fedha iliyopokelewa ilihusisha masuala ya ununuzi ikiwemo ununuzi wa mashine, vipuri na zana za ujenzi pamoja na ukarabati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla matokeo ya uchambuzi wa utekelezaji wa miradi hiyo yanaonesha dhamira thabiti ya Serikali katika kuhakikisha miradi ya maendeleo ya sekta hii muhimu inatekelezwa kwa ufanisi. Aidha, kasi ya utekelezaji iliyofikiwa pamoja na matumizi kamili ya fedha zilizopokelewa, vinaonesha uwezo mzuri na usimamizi, uratibu na utekelezaji wa miradi hiyo. Wataalamu wa sekta hii wameendelea kutumia weledi na uzalendo wao mkubwa katika kutekeleza majukumu yao ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ina maoni kuwa uwekezaji unaoendelea ni uamuzi mzuri unaohitaji kuungwa mkono. Vilevile Kamati inapongeza juhudi, weledi na hatua zote hizi na kushawishi kuwa bado mwelekeo huu unahitaji kuendelea kuzingatiwa ipasavyo. Maelezo zaidi kuhusu utekelezaji wa miradi ya maendeleo yanapatikana katika ukurasa wa 4 hadi 6 wa Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji wa mpango wa bajeti na uzingatiaji wa maoni ya Kamati kwa mwaka wa fedha 2025/2026; uchambuzi wa Kamati katika mapitio ya utekelezaji wa mpango wa bajeti wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka wa fedha 2025/2026 ulilenga kulinganisha makusanyo ya maduhuli na lengo la makusanyo hayo upatikanaji wa fedha za matumizi kwa ajili ya shughuli zilizopangwa kutekelezwa hususani fedha za matumizi mengineyo na upatikanaji wa fedha za maendeleo ikilinganishwa na bajeti iliyoidhinishwa na Bunge kwa mwaka wa fedha 2025/2026 kwa Mafungu yote matatu ya Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu hii ya taarifa inahusu uchambuzi wa Kamati kwa mambo yafuatayo; kwanza, mapitio ya utekelezaji na ushauri wa Kamati; pili, ukusanyaji wa maduhuli; na tatu, upatikanaji wa fedha kutoka Hazina.

19 MEI, 2026

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mapitio ya utekelezaji wa ushauri wa Kamati; wakati wa kuchambua mpango wa makadirio na mapato ya matumizi ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Kamati ilishauri masuala mbalimbali yaliyopaswa kuzingatiwa na kufanyiwa kazi na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Ninapenda kuliarifu Bunge lako kuwa taarifa ya mtoa hoja ilieleza bayana namna ambavyo Serikali imezingatia kwa sehemu kubwa ushauri uliotolewa na Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia Madaraka ya Bunge yaliyoainishwa katika Ibara ya 63(2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, Kamati inaendelea kusesitiza kwamba sehemu ya ushauri ambao haujatekelezwa kikamilifu inapaswa kufanyiwa kazi kamilifu na kuwa sehemu ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha ujao 2026/2027.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwenendo wa ukusanyaji wa maduhuli; kwa mwaka wa fedha 2025/2026 Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ilikadiria kukusanya maduhuli yenye jumla ya shilingi 87,603,00 kwa Mafungu yote matatu. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2026 kiasi cha fedha za maduhuri kilichokuwa kimekusanywa kilikuwa ni shilingi 180,505,418 sawa na 206.5% ya lengo. Aidha, Kamati ilibaini kuwa kiasi kilichokusanywa kimeongezeka kwa shilingi 1,746,314.98 sawa na 0.98% ikilinganishwa na kiwango kilichokusanywa katika kipindi kama hicho kwa mwaka wa fedha 2024/2025 ambacho kilikuwa ni shilingi 178,759,103.8.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa makusanyo hayo yamechangiwa na Mafungu yote matatu ya Wizara ambapo Fungu 38 – NGAME limekusanya 101.59% ya lengo lililowekwa; Fungu 39 la JKT limekusanya 101.86% ya lengo lilowekwa na Fungu 57 ambayo ni Wizara limekusanya 7.712% ya lengo iliowekwa. Ongezeko kwa Fungu 57 la Wizara kwa mwaka huu wa fedha 2025/2026 limetokana na malipo ya deni la ukodishaji wa simu kama ilivyokuwa katika mwaka uliopita wa fedha. Hata hivyo ongezeko la mwaka huu ni kubwa zaidi kwa 199.04%.

19 MEI, 2026

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Kamati ilifanya uchambuzi kwa kila Fungu na kubainisha mchanganuo wa makusanyo ya maduhuri kwa mwaka wa fedha 2025/2026 kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 01.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa mwenendo wa makusanyo umeonesha matokeo ya kuridhisha katika Mafungu yote. Kwa ujumla makusanyo yamevuka lengo lilowekwa kabla ya mwaka wa fedha kukamilika. Hali hii inaakisi usimamizi imara wa mapato na jitihada madhubuti ya kuongeza ufanisi wa ukusanyaji wa mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upatikanaji wa fedha kutoka Hazina; Kamati ilipokea na kuchambua Taarifa ya Wizara kuhusu utekelezaji wa bajeti kwa mwaka 2025/2026 kwa lengo la kujiridhisha kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa kufanya ulinganisho wa bajeti iliyoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya matumizi yote ya Wizara na kiasi cha fedha kilichokuwa kimetolewa hadi kufikia mwezi Aprili, 2026 Kamati ililinganisha uwiano wa bajeti na Mafungu hayo kwa uwiano wa fedha ilizopokelewa kwa Mafungu hayo na ulinganisho huo unaonekana katika Jedwali Na. 02 na Na. 03 kwenye Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na uchambuzi huu wa Kamati, mambo yafuatayo yalibainika kuhusiana na mwenendo wa upatikanaji wa fedha:-

- (i) Hadi kufikia mwezi Aprili, 2026 Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kupitia Mafungu yote matatu ilikuwa imepokea shilingi 3,122,326,357,205.44 sawa na 85.64% ya fedha zilizoidhinishwa.
- (ii) Kati ya fedha zilizopokelewa Fungu 38 - NGOME ilikuwa limepokea 90.78% ya fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya Fungu hilo na Fungu 39 – JKT lilikuwa limepokea 83.34% ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya Fungu hilo, na Fungu 57 lilikuwa limepokea 40.32% ya fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya fungu hilo.

19 MEI, 2026

- (iii) Serikali ilizingatia vyema uzito uliotolewa na Bunge wakati wa kuidhinisha bajeti ya Wizara hii. Mfano, bajeti ya Fungu 38 la NGOME iliyoidhinishwa na Bunge ilikuwa ni 76.32% ya bajeti yote ya Wizara na kiasi kilichopokelewa na fungu hilo ni 80.9% ya fedha zote zilizopokelewa na Wizara hadi kufikia mwezi Aprili, 2026.
- (iv) Fungu 39 lilitengewa 15.8% ya bajeti yote ya Wizara na kiasi kilichopokelewa na fungu hilo hadi kufikia mwezi Aprili, 2026 ni 15.4% ya fedha zote zilizopokelewa na Wizara.
- (v) Fungu 57 liliidhinishwa 7.9% ya bajeti yote ya Wizara na hadi kufikia mwezi Aprili, 2026 kiasi kilichopokelewa ni 3.7% ya fedha zote zilizopokelewa na Wizara katika kipindi hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwenendo huu unatoa mwelekeo mzuri wa kuendelea kuimarisha sekta ya ulinzi nchini kwa kutoa kipaumbele kwa Wizara hii. Kwa juhudi hizo, Taifa litaendelea kuimarika na Serikali itaendelea kuwezesha ustawi wa shughuli za kijamii na kiuchumi nchini. Maelezo zaidi ya Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2025/2026 yapo katika ukurasa wa 7 hadi 14 wa Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa mpango wa bajeti na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2026/2027; ninaanza na mpango wa utekelezaji wa majukumu ya wizara kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kujiridhisha na makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2026/2027, Kamati ilipitia majukumu makuu ya Wizara na kubaini kuwa makadirio ya mapato na matumizi yanayopendekezwa yanalenga kuendelea kuimarisha utendaji wa kazi na ufanisi wa Wizara katika utekelezaji wa majukumu hayo kulingana na Dira na Dhima ya Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, utekelezaji wa bajeti ya Wizara unalenga kuchangia katika nguzo za usalama na amani

19 MEI, 2026

ambao ni msingi wa utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2050 ambayo utekelezaji wake kamili unaanza katika mwaka ujao wa fedha. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2026/2027; katika mwaka wa fedha 2026/2027, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kupitia Mafungu yote matatu 38, 39 na 57 inatarajia kukusanya mapato ya jumla ya shilingi 90,603,300. Kiasi hiki kimeongezeka kwa 3.4% ikilinganishwa na kiasi kilichopangwa kukusanywa katika mwaka wa fedha 2025/2026 ambacho kilikuwa ni shilingi 87,603,00. Mchanganuo wa makusanyo ni kama unavyoonekana katika Jedwali Na. 04 na Chati Na. 01 kwenye Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na uchambuzi uliofanyika, Kamati imebaini mambo yafuatayo: -

- (i) Lengo la makusanyo kwa Mafungu yote ya Wizara hii imeongezeka kwa 3.4% ikilinganishwa na lengo lilowekwa katika mwaka wa fedha unaomalizika wa 2025/2026.
- (ii) Fungu namba 39 ambalo ni JKT linatarajiwa kuchangia katika makusanyo ya Wizara kwa kiasi cha 74.4%. Fungu 38% ambayo ni NGOME linatarajiwa kuchangia katika makusanyo kwa kiwango cha 24.3% na Fungu la 57 Wizara linatarajiwa kuwa litachangia katika makusanyo kwa kiwango cha 1.3%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tathmini ya Kamati imebaini kuwa mwenendo wa makusanyo wa mafungu yote matatu unaridhisha kwani katika mwaka huu wa fedha 2025/2026, mafungu yote yamevuka lengo na makusanyo hadi kufikia mwezi Aprili 26 ambapo kiwango kilipaswa kuwa 75%. Ni matarajio ya Kamati kwamba usimamizi mzuri wa ukusanyaji wa mapato na weledi uliotumika katika mwaka wa fedha 2025/2026 utaendelea kuzingatiwa ipasavyo.

19 MEI, 2026

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa makadirio ya matumizi; maelezo ya Wizara yaliyowasilishwa kwenye Kamati yalibainisha kuwa, katika mwaka wa fedha 2026/2027 Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa katika mafungu yote matatu, inaomba kuidhinishwa shilingi 4,286,489,324,427; kati ya fedha hizo zilizoidhinishwa shilingi 3,859,955,671,427 sawa na 90.05% ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 426,583,653,000 sawa na 9.95% ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo, na katika uchambuzi wake, Kamati imebaini mambo yafuatayo:-

- (i) Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka wa fedha 2026/2027 imeongezeka kwa shilingi 640,577,256,427 sawa na 17.59 ikilinganishwa na bajeti ya mwaka wa fedha 2025/2026. Aidha ongezeko hilo ni sawa na mara mbili ya ongezeko lililopita ambalo lilikuwa ni 8.8%;
- (ii) Kiasi cha fedha kinachoombwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida kimeongezeka kwa shilingi 582,840,077,000 ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2025/2026 ambacho ni sawa na 16.02%;
- (iii) Fedha zinazoomba kwa ajili ya miradi ya maendeleo zimeongezeka kwa shilingi 107,739,091,000 ambapo ni ongezeko la 33.78% ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2025/2026%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ongezeko la makadirio ya matumizi ya aina zote katika Wizara hii limezingatia umuhimu wa kuendelea kuimarisha hali ya ulinzi na usalama pamoja na mipaka ya nchi yetu. Aidha kuongezeka kwa bajeti kutakuwa na tija iwapo fedha zinazoombwa kutoka Hazina zitapatikana kwa wakati na kwa ukamilifu. Maelezo zaidi ya uchambuzi wa mpango wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2026/2027 yanapatikana katika ukurasa wa 15 hadi 20 wa Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni ya Kamati; kwa kuzingatia maelezo ya uchambuzi niliyoyatoa, Kamati ina mtazamo na maoni ambayo yamejenga msingi na ushauri unaotolewa na Kamati kwa Wizara. Mtazamo na maoni hayo ni kama ifuatavyo: -

19 MEI, 2026

- (i) Upatikanaji wa fedha za maendeleo kwa wakati na kwa kiwango stahiki ni muhimu uendelee kupewa kipaumbele ili kuhakikisha malengo yaliyokusudiwa yanafikiwa;
- (ii) Mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa JKT ni muhimu kwa vijana kwani huwajengea uzalendo, ukakamavu, umoja wa Kitaifa na stadi za maisha na kazi. Ni vyema fursa za mafunzo hayo zikaongezwa kwa vijana nchini;
- (iii) Ulipaji wa fidia kwa maeneo yaliyofanyiwa uthamini kwa lengo la kutwaliwa kwa shughuli za ulinzi ni muhimu ili wananchi wanaohamishwa wawezeshe kuanzisha au kuendeleza shughuli za kiuchumi na kijamii katika maeneo mengine;
- (iv) Upatikanaji wa fedha za kulipa fidia kwa wananchi wanaohamishwa kupisha shughuli za kiulinzi na malipo ya fidia stahiki kwa wakati unapunguza adha kwa wananchi kuendelea kusubiri fidia na au kuwepo katika maeneo hayo yasiyopaswa kuyaendeleza;
- (v) Usimamizi bora wa matumizi ya nishati safi utaongeza juhudi za kulinda mazingira na hatua ya taasisi za ulinzi kuongeza matumizi ya nishati safi, kuzalisha mkaa wa banifu na kutengeneza mitambo ya gesi vunge (*biogas*) ni ya kupongezwa kwani inasaidia kupunguza matumizi ya nishati chafu, kulinda mazingira na kuwapa ujuzi vijana walio katika mafunzo ya JKT;
- (vi) JKT ikiendelea kutoa mafunzo ya mkaa mbadala na teknolojia ya mitambo ya *biogas* kwa vijana, jamii itanufaika kutokana na ujuzi huo wa wahitimu wa mafunzo ya JKT na kuchangia mafanikio ya mkakati wa Taifa wa Nishati Safi ya Kupikia 2024/2034 unaolenga angalau asilimia 80 ya Watanzania ya kutumia nishati safi ifikapo mwaka 2034;

19 MEI, 2026

- (vii) Hatua ya SUMA-JKT kutumia vyanzo vya ndani ya mapato ili kuongeza uzalishaji mali inachangia kuiwezesha JKT kugharamia malezi ya vijana wanaojiunga na mafunzo na hivyo kuipunguzia Serikali mzigo. Hata hivyo, uwiano baina ya shughuli za uzalishaji na malezi ya vijana lazima vizingatiwe; na
- (viii) Uendelezaji wa Mashirika ya Kimkakati ya Mzinga na Nyumbu katika tasnia ya ulinzi (*Defense Industry*) unapaswa kupewa kipaumbele kupitia utoaji wa bajeti stahiki ya maendeleo na usasishaji wa teknolojia kwa maana usasishaji Waheshimiwa Wabunge ni kwa kutumia teknolojia za kisasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wa Kamati, kutokana na mtazamo wa maoni na maoni ya hapo juu Kamati inashauri yafuatayo:-

- (i) Serikali iendelee kuimarisha upatikanaji wa fedha za maendeleo kwa wakati na kwa kiwango stahiki ili kuendelea kufanikisha utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa maendeleo yaliyokusudiwa.
- (ii) Serikali iongeze nafasi za vijana kujiunga na JKT kwa kuongeza uwezo wa kambi na kuboresha miundombinu ya mafunzo. Aidha, mafunzo ya stadi za kazi yaendane na mahitaji halisi ya soko la ajira. Sambamba na kuanzisha mfumo wa ufuatiliaji wa wahitimu ili kupata mrejesho wa matokeo ya mafunzi hayo.
- (iii) Serikali iendelee kutenga fedha katika bajeti kila mwaka ili kulipa fidia kwa wananchi wanaohamishwa kupisha shughuli za kiulinzi kwa wakati ili kuepuka malimbikizo ya madeni.
- (iv) Wizara ya Ulinzi iendelee kuiwezesha kifedha na kiujuzi SUMA-JKT ili iendelee uzalishaji na kuchangia uwezo wa JKT katika kugharamia malezi ya vijana, shughuli za uzalishaji kama kilimo, viwanda, biashara, ufugaji, uvuvi

19 MEI, 2026

na ujenzi zitumike kikamilifu kuongeza ujuzi wa vijana bila kuathiri lengo kuu la malezi ya JKT.

- (v) Wizara isimamie matumizi ya nishati safi katika taasisi zake zote ili kulinda mazingira huku JKT ikiendelea kutoa mafunzo ya mkaa mbadala na teknolojia ya mitambo ya gesi vunde (*biogas*) kwa vijana ili iwanufaishe jamii wanaporejea uraiani.
- (vi) Serikali iendelee kuyaimarisha mashirika ya kimkakati ya Mzinga na Nyumbu katika tasnia ya ulinzi kwa kuyapatia bajeti stahiki na usafishaji wa teknolojia ili kuyaongezea ufanisi na uwezo wa kujiendesha na hivyo kuwezesha kufikiwa kwa tija tarajiwa.
- (vii) Wizara iendelee na utekelezaji maoni na mapendekezo ya Kamati yaliyotolewa katika vipindi mbalimbali vilivyopita ambayo haijatekelezwa kwa lengo la kuendelea kuboresha utendaji wa shughuli za Wizara na Taasisi zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho; napenda kukushukuru tena kwa kunipa fursa hii kwa ajili ya kuwasilisha taarifa hii. Aidha, kwa namna ya pekee nawashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kwa kutoa maoni, ushauri na ushirikiano ambavyo vimewezesha kukamilisha maandilizi ya taarifa hii. Ninaomba majina yao kama yalivyo katika taarifa yaingie kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati, napenda kutumia fursa hii kumshukuru Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimiwa Dkt. Rhimo Nyansaho (Mb), kwa kushirikiana na Kamati kwa vizuri zaidi katika kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu ya Kikanuni ya Kamati. Aidha, namshukuru Katibu Mkuu, Dkt. Faraji Mnyepe pamoja na watendaji wote wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa ushirikiano wao kwa Kamati.

19 MEI, 2026

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru Katibu wa Bunge, Ndugu Baraka Leonard kwa uratibu mzuri wa shughuli za Kamati na Bunge. Aidha, naishukuru Sekretarieti ya Kamati kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati na kuhakikisha taarifa hii inakamilika kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu lipokee taarifa hii na likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka wa fedha 2026/2027 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na ninaomba kuwasilisha, ahsanteni sana. *(Makofi)*

TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA (FUNGU 38, 39, 57) KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026; PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

SEHEMU YA KWANZA

1.0 UTANGULIZI

1.1 Maelezo ya Jumla

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 121 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, 2025, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka wa fedha 2025/2026, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2026/2027 na kuliomba Bunge lako Tukufu liipokee Taarifa hii na kuikubali, kisha kuidhinisha Bajeti ya Wizara hiyo.

1.2 Msingi wa Taarifa

Mheshimiwa Spika, msingi wa taarifa hii ni majukumu ya Kamati kwa mujibu wa Kifungu cha 6 (3) na Kifungu cha 7 (1) (a), cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge pamoja na masharti ya Kanuni ya 121 (4) ya Kanuni za Bunge, kuwa kabla ya Taarifa ya Utekelezaji na Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na JKT kujadiliwa Bungeni, zilipaswa kuchambuliwa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama. Naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa, uchambuzi huo ulifanyika tarehe 26 Machi, 2026 baada ya ziara za ukaguzi wa miradi ya maendeleo inayotekelezwa chini ya Wizara hii kama inavyoelekeza Kanuni ya 120(1) na 121(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge.

Mheshimiwa Spika, kwa madhumuni ya kubainisha mawanda ya Taarifa hii, ni vyema nilikumbushe Bunge hili kwamba, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) inayo jumla ya Mafungu Matatu (3) ya Kibajeti ambayo ni:-

- (i) Fungu 38 - Ngome;
- (ii) Fungu 39 - Jeshi la Kujenga Taifa; na
- (iii) Fungu 57 – Wizara.

1.3 Muundo wa Taarifa

Mheshimiwa Spika, ili kuliwezesha Bunge lako Tukufu kufuatilia kikamilifu utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2025/2026, pamoja na kuishauri vema Serikali kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka wa fedha 2026/2027, Taarifa hii imegawanyika katika Sehemu Kuu tano (5) kama ifuatavyo: -

- (i) Sehemu ya Kwanza; ni utangulizi ambao unaeleza kwa ujumla kuhusu msingi na muundo wa Taarifa.
- (ii) Sehemu ya Pili; ambayo inafafanua matokeo ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo uliofanyika kwa mujibu wa Kanuni ya 120 (1) ya Kanuni za Bunge.
- (iii) Sehemu ya Tatu hadi ya Nne ambazo zinachambua utekelezaji wa mipango na Bajeti kwa mwaka wa fedha

19 MEI, 2026

2025/2026 pamoja na kuchanganua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

(iv) Sehemu ya Tano inaonesha Maoni na Ushauri wa Kamati kutokana na matokeo ya uchambuzi. Aidha, sehemu hii inahitimisha taarifa kwa shukurani na kubainisha msimamo wa jumla wa Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

SEHEMU YA PILI

2.0 MATOKEO YA UKAGUZI WA MIRADI YA MAENDELEO

2.1 Maelezo ya Jumla

Mheshimiwa Spika, ili kuzingatia masharti ya Kanuni ya 121 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ilitembelea na kukagua Mradi wa Ujenzi wa Bweni la Askari Kapera Wanawake TMA Mzinga - Morogoro.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Taarifa hii inaeleza mambo makuu mawili yafuatayo: -

- (i) Muhtasari wa maelezo ya miradi iliyotembelewa na kukaguliwa katika mwaka wa fedha 2025/2026; na
- (ii) Uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji wa miradi hiyo.

Mheshimiwa Spika, sehemu hii inalenga kuliwezesha Bunge kufuatilia hali ya utekelezaji na upatikanaji wa fedha ambazo ziliidhinishwa na hivyo kupata mantiki ya uamuzi wake wakati wa kujadili makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

2.2 Muhtasari wa Maelezo kuhusu Miradi ya Maendeleo iliyokaguliwa

Mheshimiwa Spika, ili kuzingatia masharti ya Kanuni ya 121 (1) ya Kanuni za Bunge, Kamati ilikagua utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ya Shirika la Mzinga, Morogoro. Madhumuni ya miradi hiyo ni kufanya ununuzi wa mashine, vipuri na malighafi ili kuboresha mkondo wa uzalishaji

19 MEI, 2026

wa mazao ya msingi; kukamilisha ujenzi wa karakana na ukarabati wa majengo na miundombinu, na kufanya utafiti na kutengeneza kifaa (portable launcher) kitakachotumika kurusha bomu baridi na kufukuza wanyama waharibifu kwenye makazi ya binadamu. Miradi hii yote inatekelezwa kwa utaratibu wa *Force Account*.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa kuwa utekelezaji wa miradi hiyo ulitengewa jumla ya **shilingi 6,000,000,000.00** na hadi kufikia mwezi Machi, 2026, Wizara ilikuwa imepokea kiasi cha **shilingi 4,674,582,595.94** ambacho ni sawa na **asilimia 77.9** ya fedha iliyotengwa. Aidha, ilielezwa kwamba utekelezaji wa miradi hiyo unatarajiwa kukamilika kabla ya juni, 2026 iwapo kiasi cha fedha kilichosalia kitapatikana.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa taarifa za mradi wakati wa ziara ulionyesha yafuatayo:-

- (i) Hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa miradi ni wastani wa **asilimia 90**, ingawaje fedha zilizopokewa ni **asilimia 77.9**;
- (ii) Matumizi ya fedha iliyopokelewa yalikuwa ni **asilimia 100** ya fedha iliyopokelewa na **asilimia 77.9** ya bajeti iliyotengwa; na
- (iii) Sehemu ya matumizi ya fedha iliyopokelewa ilihusisha masuala ya ununuzi ikiwemo ununuzi wa mashine, vipuli na zana; na ujenzi na ukarabati.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla, matokeo ya uchambuzi wa utekelezaji wa miradi hiyo yanaonesha dhamira thabiti ya Serikali katika kuhakikisha miradi ya maendeleo ya sekta hii muhimu inatekelezwa kwa ufanisi.

Aidha, kasi ya utekelezaji iliyofikiwa pamoja na matumizi kamili ya fedha zilizopokelewa vinaonesha uwezo mzuri wa usimamizi, uratibu na utekelezaji wa miradi hiyo. Kamati ina maoni kuwa, uwekezaji unaoendelea ni uamuzi mzuri unaohitaji kuungwa mkona. Kamati inapongeza juhudi, weledi na hatua hizi na kushawishi kuwa, bado mwelekeo huu unahitaji kuendelea kuzingatiwa inavyostahili.

19 MEI, 2026

2.3 Maoni ya Jumla kuhusu Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026

Mheshimiwa Spika, kutokana na uchambuzi wa taarifa za utekelezaji wa miradi, ni dhahiri kuwa sekta ya ulinzi imeendelea kupewa kipaumbele kupitia utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Aidha, wataalamu wa sekta hiyo wameendelea kutumia weledi na uzalendo wao mkubwa kutekeleza majukumu yao inavyostahili.

Kamati ina maoni kuwa pamoja na juhudi hizo za Serikali kuhakikisha kuwa sekta ya ulinzi inatekeleza vema miradi yake, bado kuna umuhimu wa kuendelea kupeleka pesa zinazoidhishwa kwa ajili ya sekta hii.

SEHEMU YA TATU

3.0 UCHAMBUZI WA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA BAJETI NA UZINGATIAJI WA MAONI YA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026

3.1 Maelezo ya Jumla

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati katika Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka wa fedha 2025/2026, ulilenga kulinganisha makusanyo ya maduhuli na lengo la makusanyo hayo, upatikanaji wa fedha za matumizi kwa ajili ya shughuli zilizopangwa kutekelezwa, hususan fedha za matumizi mengineyo na upatikanaji wa fedha za maendeleo ikilinganishwa na bajeti iliyoidhinishwa na Bunge kwa mwaka wa fedha 2025/2026, kwa mafungu yote Matatu ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, aidha, Kamati ilizingatia taarifa mbalimbali zilizowasilishwa mbele ya Kamati kwa kipindi cha mwezi Januari na mwezi Aprili, 2026 pamoja na majadiliano yaliyochangia upatikanaji wa taarifa muhimu, na za ziada wakati wa vikao vya Kamati. Sehemu hii ya taarifa inahusu uchambuzi wa Kamati wa mambo yafuatayo: -

- (i) Mapitio ya utekelezaji wa ushauri wa Kamati;
- (ii) Ukusanyaji wa Maduhuli; na

19 MEI, 2026

(iii) Upatikanaji wa Fedha kutoka Hazina.

3.2 Mapitio ya Utekelezaji wa Ushauri wa Kamati

Mheshimiwa Spika, wakati wa kuchambua Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Kamati ilishauri masuala mbalimbali yanayopaswa kuzingatiwa na kufanyiwa kazi na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Napenda kuliarifu Bunge lako kuwa, taarifa ya Mtoa Hoja ilieleza bayana kwamba, Serikali imezingatia kwa sehemu kubwa ushauri uliotolewa na Kamati.

Kwa kuzingatia Madaraka ya Bunge yaliyoainishwa katika Ibara ya 63 (2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, Kamati inaendelea kusisitiza kwamba, sehemu ya ushauri ambao haujatekelezwa kikamilifu inapaswa kufanyiwa kazi kikamilifu na kuwa sehemu ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha ujao, 2026/2027.

3.3 Mwenendo wa Ukusanyaji wa Maduhuli

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2025/2026, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ilikadiria kukusanya maduhuli yenye jumla ya **Shilingi 87,603,000.00** kwa Mafungu yote matatu (3)

Kwa mujibu wa maelezo ya Wizara, hadi kufikia mwezi Aprili, 2026 kiasi cha fedha za maduhuli kilichokuwa kimekusanywa kilikuwa **Shilingi 180,505,418.00** sawa na **asilimia 206.05** ya lengo. Aidha, Kamati ilibaini kuwa kiasi kilichokusanywa kimeongezeka kwa **Shilingi 1,746,314.92** sawa na **asilimia 0.98** ikilinganishwa na kiwango kilichokusanywa katika kipindi kama hicho kwa mwaka wa fedha 2024/2025 ambacho kilikuwa ni **Shilingi 178,759,103.08**

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa, makusanyo hayo yamechangiwa na Mafungu yote matatu ya Wizara ambapo; Fungu 38 (Ngome) limekusanya **asilimia 101.59** ya lengo lililowekwa na Fungu 39 (JKT) limekusanya **asilimia 101.86** ya lengo lililowekwa na Fungu 57 (Wizara) limekusanya **asilimia 7,712** ya lengo lililowekwa.

Ongezeko kwa Fungu 57 (Wizara) kwa mwaka huu wa fedha 2025/2026 limetokana na malipo ya deni la ukodishaji wa simu, kama ilivyokuwa katika mwaka uliopita wa fedha. Hata hivyo, ongezeko la

19 MEI, 2026

mwaka huu ni kubwa zaidi kwa **asilimia 196.04** ikilinganishwa na ongezeko la **asilimia 7,517** katika mwaka uliopita wa fedha, 2024/2025.

Mheshimiwa Spika, vilevile Kamati ilifanya uchambuzi kwa kila Fungu na kubainisha mchanganuo wa makusanyo ya maduhuli kwa mwaka wa fedha 2025/2026 kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 01**

Jedwali Na. 1: Mchanganuo wa Makadirio na Makusanyo ya Maduhuli

| FUNGU | MAKADIRIO | MAKUSANYO | % YA JUMLA YA MAKUSANYO |
|--------------|-------------------|-----------------------|--------------------------------|
| 38 - Ngome | 22,000,000.00 | 22,349,954.00 | 101.59 |
| 39 - JKT | 64,403,000.00 | 65,603,000.00 | 101.86 |
| 57 - Wizara | 1,200,000.00 | 92,552,464.00 | 7,712.71 |
| Jumla | 87,603,000 | 180,505,418.00 | 206.05 |

Chanzo: Randama ya Wizara 2026/2027

Mheshimiwa Spika, vilevile, Kamati ilifanya uchambuzi na ulinganisho wa makusanyo yaliyopatikana kwa kila Fungu hadi kufikia mwezi Aprili, 2026 na makusanyo yaliyopatikana katika kipindi kama hicho katika mwaka wa fedha 2024/2025 na kubaini yafuatayo: -

(i) **Makusanyo katika Fungu 38 – Ngome;** hadi kufikia mwezi Aprili, 2026 ilikusudiwa makusanyo yawe angalau **asilimia 75** ya lengo lililowekwa lakini katika utekelezaji Fungu hilo lilikuwa limekusanya **asilimia 101.59** ya lengo la mwaka.

(ii) **Makusanyo ya Fungu 39 –JKT;** hadi kufikia mwezi Aprili, 2026 ilikusudiwa makusanyo yawe angalau **asilimia 75** ya lengo lililowekwa, lakini katika utekelezaji Fungu hilo lilikuwa limekusanya **asilimia 101.86** ya lengo la mwaka;

(iii) **Makusanyo ya Fungu 57 – Wizara;** hadi kufikia mwezi Aprili, 2026 ilikusudiwa makusanyo yawe angalau **asilimia 75** ya lengo lililowekwa lakini katika utekelezaji Fungu hilo lilikuwa limekusanya **asilimia 7,712.71** ya lengo la mwaka;

19 MEI, 2026

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa mwenendo wa makusanyo umeonesha matokeo ya kuridhisha katika mafungu yote. Kwa ujumla makusanyo yamevuka lengo lililowekwa kabla ya mwaka wa fedha kukamilika. Hali hii inaakisi usimamizi imara wa mapato na jitihada madhubuti za kuongeza ufanisi wa ukusanyaji wa mapato.

3.4 Upatikanaji wa Fedha kutoka Hazina

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipokea na kuchambua Taarifa ya Wizara kuhusu utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka 2025/2026, kwa lengo la kujiridhisha kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa kufanya ulinganisho wa bajeti iliyoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya matumizi yote ya Wizara na kiasi cha fedha kilichokuwa kimetolewa hadi kufikia mwezi Aprili, 2026.

Aidha, katika kujiridhisha kuhusu uzito uliowekwa wakati wa utoaji wa fedha kutoka Hazina kama ulielekeana na uzito uliokusudiwa na Bunge wakati wa kuidhinisha Bajeti ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Kamati ililinganisha uwiano wa Bajeti za Mafungu hayo na uwiano wa fedha zilizopokelewa kwa Mafungu hayo. Ulinganisho huo unaonekana katika **Jedwali Na. 02** na **Jedwali Na. 03** hapa chini.

Jedwali Na. 2: Ulinganisho wa Fedha zilizoidhinishwa na zilizopokelewa kwa Fungu 38, Fungu 39 na Fungu 57
Chanzo: Randama ya Wizara 2026/2027

| Fungu | Fedha zilizoidhinishwa kwa mwaka 2025/2026 | Asilimia ya fedha zilizoidhinishwa Kiuwiano | Fedha zilizopokelewa kufikia Aprili, 2026 | Asilimia ya fedha zilizopokelewa | Asilimia ya fedha zilizopokelewa |
|-------|--|---|---|----------------------------------|----------------------------------|
| 38 | 2,782,596,840,000.00 | 76.3 | 2,526,067,863,600.18 | 90.78 | 80.9 |
| 39 | 576,953,771,000.00 | 15.8 | 480,804,851,482.33 | 83.34 | 15.4 |
| 57 | 286,361,457,000.00 | 7.9 | 115,453,642,132.93 | 40.32 | 3.7 |
| | 3,645,912,068,000.00 | 100 | 3,122,326,357,215.44 | 85.64 | 100 |

Chanzo: Randama ya Wizara 2026/2027

19 MEI, 2026

Mheshimiwa Spika, kutokana na uchambuzi huo wa Kamati, mambo yafuatayo yalibainika kuhusiana na mwenendo wa upatikanaji wa fedha:-

(i) Hadi kufikia mwezi Aprili, 2026 Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kupitia mafungu yote matatu ilikuwa imepokea **Shilingi 3,122,326,357,215.44** sawa na **asilimia 85.64** ya fedha zilizoidhinishwa;

(ii) Kati ya fedha zilizopokelewa, Fungu 38 (Ngome) lilikuwa limepokea **asilimia 90.78** ya fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya Fungu hilo, Fungu 39 (JKT) lilikuwa limepokea **asilimia 83.34** ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya Fungu hilo na Fungu 57 (Wizara) lilikuwa limepokea **asilimia 40.32** ya fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya fungu hilo;

(iii) Serikali ilizingatia vyema uzito uliotolewa na Bunge wakati wa kuidhinisha Bajeti ya Wizara hii. Mfano; Bajeti ya Fungu 38 (Ngome) iliyoidhinishwa na Bunge ilikuwa ni **asilimia 76.32** ya Bajeti yote ya Wizara na kiasi kilichopokelewa na Fungu hilo ni **asilimia 80.9** ya fedha zote zilizopokelewa na Wizara hadi kufikia mwezi Aprili, 2026;

(iv) Fungu 39 lilitengewa **asilimia 15.8** ya bajeti yote ya Wizara na kiasi kilichopokelewa na Fungu hilo hadi kufikia mwezi Aprili, 2026 ni **asilimia 15.4** ya fedha zote zilizopokelewa na Wizara; na

(v) Fungu 57 liliidhinishwa **asilimia 7.9** ya bajeti yote ya Wizara, na hadi kufikia mwezi Aprili, 2026 kiasi kilichopokelewa ni **asilimia 3.7** ya fedha zote zilizopokelewa na Wizara katika kipindi hicho.

Mheshimiwa Spika, Mwenendo huu unatoa mwelekeo mzuri wa kuendelea kuimarisha sekta ya Ulinzi nchini kwa kutoa kipaumbele kwa wizara hii. Kwa juhudi hizo, taifa litaendelea kuimarika na serikali itaendelea kuwezesha ustawi wa shughuli za kijamii na kiuchumi nchini.

19 MEI, 2026

**Jedwali Na. 3: Ulinganisho wa Fedha za Maendeleo
zilizoidhinishwa na zilizopokelewa kwa
Fungu 38, Fungu 39 na Fungu 57**

| Fungu | Fedha za maendeleo zilizoidhinishwa kwa mwaka 2025/2026 | Asilimia ya fedha zilizoidhinishwa | Fedha za maendeleo zilizopokelewa kufikia Aprili, 2026 | Asilimia ya fedha zilizopokelewa | Asilimia ya fedha zilizopokelewa |
|--------------|--|---|---|---|---|
| 38 | 48,867,636,000.00 | 15.33 | 9,309,160,031.00 | 19.05 | 8.42 |
| 39 | 9,929,926,000.00 | 3.11 | 9,929,926,000.00 | 100 | 8.98 |
| 57 | 260,000,000,000.00 | 81.56 | 91,349,963,829.00 | 35 | 82.6 |
| | 318,797,562,000.00 | 100 | 110,589,049,860.00 | 34.69 | 100 |

(i) Hadi kufikia mwezi Aprili, 2026 Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kupitia mafungu yote matatu ilikuwa imepokea fedha za maendeleo kiasi cha **Shilingi 110,589,049,860.00** sawa na **asilimia 34.69** ya fedha zilizoidhinishwa;

(ii) Kati ya fedha za maendeleo zilizopokelewa na Wizara katika mafungu yote matatu, Fungu 38 (Ngome) lilipokea **asilimia 8.42**; Fungu 39 (JKT) **asilimia 8.98** na Fungu 57 (Wizara) **asilimia 82.6**;

(iii) Serikali inajitahidi kuzingatia uzito uliotolewa na Bunge wakati wa kuidhinisha Bajeti ya Wizara hii. Jitihada za kuhakikisha fedha zinapokelewa kwa kiwango stahiki zinadhahirika. Mfano; bajeti iliyoidhinishwa kwa ajili ya maendeleo kwa Fungu 39 – JKT ilipatikana kwa **asilimia 100** hadi kufikia Aprili, 2026; na

(iv) Jitihada zinahitajika katika kusaidia kuongeza kiasi cha fedha zinazopokelewa kwa Fungu 38 – Ngome na Fungu 57 – Wizara ambazo kwa wastani zilipokea fedha za maendeleo kwa wastani wa asilimia **27**;

19 MEI, 2026

SEHEMU YA NNE

4.0 UCHAMBUZI WA MPANGO WA BAJETI NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027

4.1 Mpango wa Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027

Mheshimiwa Spika, ili kujiridhisha na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2026/2027, Kamati ilipitia majukumu makuu ya Wizara na Kubaini kuwa makadirio ya mapato na matumizi yanayopendekezwa yanalenga kuendelea kuimarisha utendaji kazi na ufanisi wa Wizara katika utekelezaji wa majukumu hayo kulingana na Dira na Dhima ya Wizara. Aidha, utekelezaji wa bajeti ya Wizara unalenga kuchangia katika nguzo za amani, usalama, na ujuzi na amani, ambazo ni msingi wa utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2050 ambayo utekelezaji wake kamili unaanza katika mwaka ujao wa fedha.

Mheshimiwa Spika, lengo hili limepangwa kufikiwa kwa kutekeleza majukumu nane ambayo ni pamoja na kuliongezea uwezo wa kimedani Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania kwa kulipatia vifaa vya kisasa, zana bora na raslimaliwatu; kuboresha mazingira ya kufanyia kazi, makazi na kuimarisha upatikanaji wa huduma stahiki na mahitaji ya msingi kwa wanajeshi na watumishi wa umma; kutoa fursa kwa vijana wa kitanzania kupata mafunzo ya awali ya kijeshi na stadi za kazi ili kuwajengea ukakamavu, uzalendo, umoja wa kitaifa na uwezo wa kujitegemea; kuendeleza tafiti na uhawilishaji wa teknolojia kwa ajili ya kuzalisha bidhaa na huduma kwa matumizi ya kijeshi na kiraia; kuendelea kuimarisha Jeshi la Akiba kwa kutoa mafunzo stahiki; kuimarisha ushirikiano na nchi nyingine katika nyanja za kijeshi na kiulinzi; na kuendelea kushirikiana na mamlaka za kiraia katika kukabiliana na dharura pale inapohitajika.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati umeonesha kuwa, majukumu yaliyopangwa yatawezesha kufikiwa kwa malengo Nane (8) ya Wizara hii kwa ufanisi zaidi iwapo Serikali itazingatia kikamilifu Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara

19 MEI, 2026

kwa kutoa kikamlifu na kwa wakati fedha zitakazoidhinishwa na Bunge ili kutekeleza mpango kazi ulioandaliwa.

4.2 Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027


Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2026/2027, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kupitia mafungu yote matatu (38, 39 na 57) inatarajia kukusanya mapato ya jumla ya **Shilingi 90,603,000.00**. Kiasi hiki kimeongezeka kwa **asilimia 3.4** ikilinganishwa na kiasi kilichopangwa kukusanywa katika mwaka wa fedha 2025/2026 ambacho kilikuwa **shilingi 87,603,000.00**. Mchanganuo wa Makusanyo ni kama unavyoonekana katika **Jedwali Na. 04.** na **Chati Na. 01** hapa chini: -

Jedwali Na. 4: Mchanganuo wa Makadirio ya Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027

| Fungu | Makadirio | Asilimia ya lengo la Wizara |
|-------------------|----------------------|-----------------------------|
| Fungu 38 - Ngome | 22,000,000.00 | 24.3 |
| Fungu 39 – JKT | 67,403,000.00 | 74.4 |
| Fungu 57 - Wizara | 1,200,000.00 | 1.3 |
| JUMLA | 90,603,000.00 | 100 |

Chanzo: Randama ya Wizara 2026/2027

CHATI 1: Mchanganuo wa asilimia ya Makadirio ya Maduhuli kwa mwaka 2026/2027



Chanzo: Randama ya Wizara 2026/2027

19 MEI, 2026

Mheshimiwa Spika, kutokana na uchambuzi uliofanyika, Kamati imebaini mambo yafuatayo: -

(i) Lengo la makusanyo kwa mafungu yote ya Wizara hii limeongezeka kwa **asilimia 3.4** ikilinganishwa na lengo lililowekwa katika mwaka wa fedha unaomalizika 2025/2026);

(ii) Fungu 39 – JKT linatarajiwa kuchangia katika makusanyo ya Wizara kwa kiwa cha **asilimia 74.4**;

(iii) Fungu 38 – Ngome linatarajiwa kuchangia katika makusanyo kwa kiwango cha **asilimia 24.3**;

(iv) Fungu 57 – Wizara inatarajiwa kuwa litachangia katika makusanyo kwa kiwango cha **asilimia 1.3**

(v) Tathmini ya Kamati imebaini kuwa mwenendo wa makusanyo kwa mafungu yote matatu unaridhisha kwani katika mwaka huu wa fedha 2025/2026 mafungu yote yamevuka lengo la makusanyo hadi kufikia mwezi Aprili, 2026 ambapo kiwango kilipaswa kuwa asilimia 75.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi huo unaonesha kuwa uhalisia umeendelea kuzingatiwa. Kamati ina maoni kwamba, usimamizi mzuri wa ukusanyaji wa mapato na weledi uliotumika kwa mwaka wa fedha 2025/2026 utaendelea kuzingatiwa inavyostahili.

4.3 Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi

Mheshimiwa Spika, maelezo ya Wizara yaliyowasilishwa kwenye Kamati, yalibainisha kwamba katika mwaka wa fedha 2026/2027, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa katika Mafungu yote matatu inaomba kuidhinishwa **Shilingi 4,286,489,324,427.00**. Kati ya fedha hizo zilizoidhinishwa, **Shilingi 3,859,955,671,427.00** sawa na **asilimia 90.05** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **Shilingi 426,533,653,000.00** sawa na **asilimia 9.95** ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, ili kukidhi mantiki ya sharti la Kanuni ya 120 (2) ya Kanuni za Bunge, Kamati ilifanya uchambuzi wa makadirio hayo

19 MEI, 2026

kwa kupitia Kasma (*Items*), Vifungu (*Subvotes*) na Mafungu (*Votes*) yote kwa kulinganisha na bajeti iliyoidhinishwa na kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2025/2026. Katika uchambuzi wake, Kamati imebaini mambo yafuatayo: -

(i) Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka wa fedha 2026/2027 imeongezeka kwa **shilingi 640,577,256,427.00**, sawa na **asilimia 17.57** ikilinganishwa na bajeti ya mwaka wa fedha 2025/2026. Aidha, ongezeko hilo ni sawa na mara mbili ya ongezeko lililopita ambalo lilikuwa ni **asilimia 8.8**;

(ii) Kiasi cha fedha kinachoombwa kwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida kimeongezeka kwa **shilingi 532,840,077,000.00** ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2025/2026, ambacho ni sawa na **asilimia 16.02**

(iii) Fedha zinazoombwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo zimeongezeka kwa **Shilingi 107,736,091,000.00**, ongezeko la **asilimia 33.78** ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2025/2026.

(iv) Katika **Shilingi 426,533,653,000.00** zinazoombwa kwa ajili ya maendeleo, sehemu kubwa ambayo ni **asilimia 82.4** ni kwa ajili ya Fungu 57 – Wizara. Aidha, kati ya sehemu iliyosalia **asilimia 4.7** ni kwa ajili ya Fungu 39 – JKT na **asilimia 12.9** ni kwa ajili ya Fungu 38 - Ngome;

(v) Ongezeko la makadirio ya matumizi ya aina zote katika Wizara hii limezingatia umuhimu wa kuendelea kuimarishaji hali ya ulinzi na usalama pamoja na mipaka ya nchi yetu; na

(vi) Kuongezeka kwa bajeti ya Wizara katika mafungu yake matatu na katika maeneo yote ya matumizi, kutakuwa na tija iwapo fedha zitaombwa kutoka hazina na kupatikana kwa wakati na kwa ukamilifu.

SEHEMU YA TANO

5.0 MAONI, USHAURI WA KAMATI NA HITIMISHO

5.1 Maoni ya Kamati

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia maelezo ya uchambuzi niliyo yatoa, Kamati ina mtazamo na maoni ambayo yanajenga msingi wa ushauri utakaotolewa na Kamati kwa Wizara. Mtazamo na maoni hayo ni kama ifuatavyo: -

(i) Upatikanaji wa fedha za maendeleo kwa wakati na kwa kiwango stahiki, ni muhimu uendelee kupewa kipaumbele ili kuhakikisha malengo yaliyokusudiwa yanafikiwa.

(ii) Mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) ni muhimu kwa vijana kwani huwajengea uzalendo, ukakamavu, umoja wa kitaifa, na stadi za maisha na kazi. Ni vyema fursa za mafunzo hayo zikaongezwa kwa vijana nchini.

(iii) Ulipaji wa fidia kwa maeneo yaliyofanyiwa uthamini kwa lengo la kutwaliwa kwa shughuli za ulinzi ni muhimu ili wananchi wanaohamishwa wawezeshe kuanzisha au kuendeleza shughuli za kiuchumi na kijamii katika maeneo mengine.

(iv) Upatikanaji wa fedha za kulipa fidia kwa wananchi wanaohamishwa kupisha shughuli za kiulinzi na malipo ya fidia stahiki kwa wakati unapunguza adha kwa wananchi kuendelea kusubiri fidia, au kuwepo katika maeneo hayo wasiyopaswa kuyaendeleza.

(v) Usimamizi bora wa matumizi ya nishati safi utaongeza juhudu za kulinda mazingira.

(vi) Hatua ya taasisi za ulinzi kuongeza matumizi ya nishati safi, kuzalisha mkaa banifu na kutengeneza mitambo ya gesi vunde (bio gas), ni ya kupongezwa kwani inasaidia kupunguza matumizi ya nishati chafu, kulinda mazingira na kuwapa ujuzi vijana walio katika mafunzo ya JKT.

(vii) JKT ikiendelea kutoa mafunzo ya mkaa mbadala na teknolojia ya mitambo ya gesi vunde (bio gas) kwa vijana, Jamii itanufaika kutokana na ujuzi huo wa wahitimu wa mafunzo ya JKT na kuchangia mafanikio ya Mkakati wa Taifa wa Nishati Safi ya Kupikia 2024 – 2034 unaolenga angalau asilimia 80 ya Watanzania kutumia nishati safi ifikapo mwaka 2034.

(viii) Hatua ya SUMA JKT kutumia vyanzo vya ndani vya mapato ili kuongeza uzalishaji mali, inachangia kuiwezesha JKT kugharamia malezi ya vijana wanaojiunga na mafunzo, na hivyo kuipunguzia Serikali mzigo. Hata hivyo, uwiano baina ya shughuli za uzalishaji na malezi ya vijana lazima vizingatiwe.

(ix) Uendelezaji wa mashirika ya kimkakati ya MZINGA na NYUMBU katika tasnia ya ulinzi (defence industry) unapaswa kupewa kipaumbele kupitia utoaji wa bajeti stahiki ya maendeleo na usasishaji wa teknolojia.

5.2 Ushauri wa Kamati

Mheshimiwa Spika, kutokana na mtazamo na maoni hapo juu, Kamati inashauri yafuatayo: -

(i) Serikali iendelee kuimarisha upatikanaji wa fedha za maendeleo kwa wakati na kwa kiwango stahiki, ili kuendelea kufanikisha utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa malengo yaliyokusudiwa.

(ii) Serikali iongeze nafasi za vijana kujiunga na JKT kwa kuongeza uwezo wa kambi na kuboresha miundombinu ya mafunzo. Aidha, mafunzo ya stadi za kazi yaendane na mahitaji halisi ya soko la ajira, sambamba na kuanzisha mfumo wa ufuatiliaji kwa wahitimu ili kupata mrejesho wa matokeo ya mafunzo hayo.

(iii) Serikali iendelee kutenga fedha katika bajeti ya kila mwaka ili kulipa fidia kwa wananchi wanaohamishwa kupisha shughuli za kiulinzi, kwa wakati na kuepuka malimbikizo ya madeni.

(iv) Wizara ya Ulinzi iendelee kuiwezesha kifedha na kiujuzi SUMA JKT ili iendelee uzalishaji na kuchangia uwezo wa JKT katika kugharamia malezi ya vijana. Shughuli za uzalishaji kama kilimo, viwanda, biashara, ufugaji, uvuvi na ujenzi zitumiwe kikamilifu kuongeza ujuzi kwa vijana, bila kuathiri lengo kuu la malezi ya JKT.

(v) Wizara isimamie matumizi ya nishati safi katika taasisi zake zote ili kulinda mazingira, huku JKT ikiendelea kutoa mafunzo ya mkaa mbadala na teknolojia ya mitambo ya gesi vunde (bio gas) kwa vijana ili wanufaishe jamii wanaporejea uraiiani.

(vi) Serikali iendelee kuyaimarisha mashirika ya kimkakati ya MZINGA na NYUMBU katika tasnia ya ulinzi kwa kuyapatia bajeti stahiki, na usasishaji wa teknolojia ili kuyaongezea ufanisi, na uwezo wa kujiendesha na hivyo kuwezesha kufikiwa kwa tija tarajiwa.

(vii) Wizara iendelee na utekelezaji wa Maoni na Mapendekezo ya Kamati yaliyotolewa katika vipindi mbalimbali vilivyopita ambayo hayajatekelezwa kwa lengo la kuendelea kuboresha utendaji wa shughuli za Wizara na taasisi zake.

5.3 Hitimisho

Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi kwa ajili ya kuwasilisha Taarifa hii. Aidha, kwa namna ya pekee nawashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, kwa kutoa maoni, ushauri na ushirikiano ambavyo vimewezesha kukamilisha maandalizi ya taarifa hii. Ninaomba majina yao kama yalivyo katika Taarifa hii yaingie kwenye Kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge (Hansard): -

1. Mhe. Najma Murtaza Giga, Mb - Mwenyekiti
2. Mhe. Paschal Inyasi Chinyele, Mb - M/Mwenyekiti
3. Mhe. Dkt. Tulia Ackson, Mb - Mjumbe
4. Mhe. Mary Pius Chatanda, Mb - Mjumbe
5. Mhe. Daniel Tlemai Awack, Mb - Mjumbe
6. Mhe. Nape Moses Nnauye, Mb - Mjumbe
7. Mhe. Zainab Rashid Kawawa, Mb - Mjumbe
8. Mhe. Dkt. Seleman Saidi Jafo, Mb - Mjumbe

19 MEI, 2026

9. Mhe. Christina Solomon Mndeme, Mb - Mjumbe
10. Mhe. Fadhili Ally Liwaka, Mb - Mjumbe
11. Mhe. Salum Khamis Haji, Mb - Mjumbe
12. Mhe. Abdul Yussuf Maalim, Mb - Mjumbe
13. Mhe. Ramadhan Muhidin Ramadhan, Mb - Mjumbe
14. Mhe. Asya Ali Khamis, Mb - Mjumbe
15. Mhe. Agnes Elias Hokororo, Mb - Mjumbe
16. Mhe. Elibariki Immanuel Kingu, Mb - Mjumbe
17. Mhe. Zainab Abdallah Issa, Mb - Mjumbe
18. Mhe. Juma Omari Kipanga, Mb - Mjumbe
19. Mhe. Dkt. David Mathayo David, Mb - Mjumbe
20. Mhe. Angela Charles Kizigha, Mb - Mjumbe
21. Mhe. Dkt. Lazaro Killian Komba, Mb - Mjumbe

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati napenda kutumia fursa hii kumshukuru Waziri wa Ulinzi na JKT Mhe. Dkt. Rhimo Simeon Nyansaho (Mb) kwa ushirikiano wake mzuri kwa Kamati katika kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu ya Kikanuni ya Kamati. Aidha, namshukuru Katibu Mkuu Dkt. Faraji Kasidi Mnyepe pamoja na Watendaji wote wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, kwa ushirikiano wao kwa kamati.

Mheshimiwa Spika, ninamshukuru Katibu wa Bunge, Ndg. Baraka Idelphonice Leornad, kwa uratibu mzuri wa shughuli za Kamati na Bunge. Aidha, naishukuru Sekretariat ya Kamati kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati na kuhakikisha Taarifa hii inakamilika kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu liipokee Taarifa hii na likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka wa fedha 2026/2027 kama yalivyowasilishwa na Mtoa Hoja.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono Hoja na naomba kuwasilisha.

Najma Murtaza Giga, (Mb)
**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE
YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA**

19 Mei, 2026

19 MEI, 2026

MWENYEKITI: Mheshimiwa ahsante. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, naomba tuwatambue pia wageni waliopo ukumbini ni wageni watano wa Mheshimiwa Profesa Pius Yanda ambao ni wapiga kura wake kutoka Kata ya Munanila, Buhigwe Mkoani Kigoma, karibuni sana wageni wetu. *(Makofi)*

Waheshimiwa sasa tunaingia kwenye uchangiaji, namwita mchangiaji wetu wa kwanza atakuwa Mheshimiwa Dkt. Selemani Saidi Jafo, ajiandae Mheshimiwa Elibariki Immanuel Kingu.

MHE. DKT. SELEMANI S. JAFO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza awali ya yote naomba kuchukua fursa hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu, Mola ambaye ametuwezesha siku hii tunakuja kujadili bajeti ya Wizara ya Ulinzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu kwa kazi kubwa anayoifanya, lakini kubwa hasa katika suala zima la kusimamia masuala ya amani, ulinzi na usalama katika nchi yetu. Mheshimiwa Rais, amejipambanua katika utawala wake unaona ameweka nguvu kubwa sana kuhakikisha Wizara hii inaendelea kufanya vizuri katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumpongeza sana Waziri, Mheshimiwa Dkt. Rhimo kwa kazi kubwa ambayo ameanza kuifanya ndani ya muda mfupi, lakini ameonyesha *leadership* nzuri, yenye hekima kubwa sana katika Wizara hili, lakini sambamba na hilo Katibu Mkuu, Dkt. Faraji Mnyepe ambaye nasema huyu ni *encyclopedia* ya Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni muda mrefu sana Katibu Mkuu huyu ameendelea kufanya kazi kubwa sana tumpongeza sana, Dkt. Mnyepe unaisimamia vizuri katika upande wa utendaji wa Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nimpongeze sana Mkuu wetu wa Majeshi Jenerali Jacob John Mkunda kwa kazi kubwa

19 MEI, 2026

unayoifanya katika suala zima kusimamia Jeshi letu, tunaimani kubwa, tuna heshima kubwa kama nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania inapozungumza, *East Africa*, Afrika, SADC tunaheshimika sana kwa sababu Jeshi letu liko imara na limekuwa saidizi kwa kiwango kikubwa sana katika suala zima kusimamia amani na migogoro Barani Afrika na maeneo mbalimbali, hakika Mkuu wa Majeshi hongera sana, sana, sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumpongeze Mnadhimu Mkuu wa Jeshi letu ambaye kwa kweli hekima yake naye ni kubwa Ndugu Salum Haji Othman, sisi Wajumbe wa Kamati tunamfahamu kwa hekima yake, weledi wake unaona kweli huyu ni Mnadhimu Mkuu wa Jeshi letu, hakika hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini niwapongeze sana Mameja Jenerali wote, tukianza na ndugu yangu Rajabu Mabele wa JKT, hakika umefanya kazi kubwa. Leo hii tunaona JKT inavyofanya kazi kubwa katika Taifa letu hili na taasisi yetu ya SUMA-JKT ambayo hii tuna kila sababu sisi kama Wabunge tuwapongeze. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Wakuu wote wa Kamandi mbalimbali na Vikosi na Wanajeshi wote katika Taifa letu.

Ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge, mimi ni Mjumbe wa Kamati, naomba niwaambie, katika Wizara hizi tuna kitu kinaitwa *untold stories*, lakini tukija kusema ni kwamba naomba tuwaaminishe Waheshimiwa Wabunge katika sehemu tunafanya kazi kubwa Wizara hii inafanya kazi kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kwa kazi kubwa ni suala zima tu la itifaki wa kawaida, lakini hapa alivyomaliza Mwenyekiti wetu wa Kamati tunasema ahsante basi Waziri njoo tumalize kumaliza hoja hii. Kwa sababu hii ni Wizara ya aina yake na kazi kubwa sana imeendelea kufanyika. *(Makofi)*

19 MEI, 2026

Mheshimiwa Mwenyekiti, kubwa zaidi niombe Wizara ya Fedha na hasa tunapopitisha bajeti niombe sana, hii Wizara tunasema ile *first charge*, tihakikishe kwamba tunaiwezesha amani yetu, utulivu wetu na nchi yetu na heshima yetu ni suala zima la usalama. Nchi yoyote inapokosa kuwa na chombo chenye kusimamia usalama wa nchi, hakika nchi hiyo inaondoa heshima yake kama Taifa hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo sisi tushukuru sana Wizara hii na Jeshi letu, limeendelea kuwa imara kusimamia kwamba suala zima la amani na utulivu nchi yetu inaendelea kuwa vizuri. Kwa hiyo, niombe Wizara ya Fedha tunapopitisha bajeti hapa na hususan bajeti ya maendeleo, tunaomba sana bajeti hii iende vizuri zaidi kama ilivyopangwa kusaidia vyombo hivi, chombo hiki kifanye kazi vizuri kazi yake ni kubwa sana. Kama nilivyosema kazi yake ni kubwa sana, naomba tuishie hapo kwanza kusema kazi yake ni kubwa sana, niombe Wizara ya Fedha ihakikishe isaidie sana upelekaji wa fedha katika Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika upande mwingine niombe sana katika uwezeshaji wa fedha kuangalia katika mfano Jeshi letu, Mwenyekiti wa Kamati amezungumza hapa, kuna maeneo mengine yametwaliwa, kuna wakati mwingine kuna maneno mengi sana ya wananchi na migogoro mingi sana, tuiheshimisha Jeshi letu, tuiheshimisha Wizara, twende tukalipe fidia kuondoa ile hali kidogo wakati mwingine wananchi wanalitazama Jeshi katika sura siyo nzuri zaidi, niombe jambo hilo tulifanye vizuri na hasa Wizara ya Fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikiwezekana twendeni tukaanzie pale Kisarawe tuna *2.5 billion* pale kwa wale wananchi ambao wametoa eneo lao kwa Kikosi cha Jeshi Kisarawe twendeni tukatoe zile fedha, huu ndiyo utaratibu mzuri hivi tutakuwa tumeenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *otherwise* mimi nishukuru sana na niwaombe Waheshimiwa Wabunge wenzangu tuunge mkono hoja hii kwa 100% basi kazi yetu iendelee na kazi na utu tunasonga mbele. *(Makofi)*

19 MEI, 2026

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa ahsante kwa mchango wako. Nilimtaja Mheshimiwa Elibariki Immanuel Kingu, wajiandae Mheshimiwa Christina Solomon Mndeme, Mheshimiwa Fadhili Ally Liwaka na Mheshimiwa Juma Mustafa Kawamba.

MHE. ELIBARIKI I. KINGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa heshima ya kuwa mchangiaji wa Wizara hii muhimu kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nitaanza kwa kusoma Kitabu cha Waraka wa Kwanza wa Mtume Petro, mstari wa tano anasema: "Vivyo hivyo ninyi vijana watiini wazee, naam ninyi nyote jifungeni unyenyekevu mpate kuhudumia kwa sababu Mungu huwapinga wote wenye kiburi, lakini huwapa wanyenyevu neema yake."

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa dhati ya moyo wangu niseme nimesoma fungu hili nikiwa nimeanza na neno la bwana nikiamini kabisa ya kwamba kwanza Mungu wetu ni Mungu wa Majeshi, Mungu wetu ni Mungu wa Majeshi na nimesoma fungu hili kwanza nikimtanguliza Mungu katika bajeti hii muhimu sana katika masuala mazima ya ulinzi wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiri kwamba mimi nimekuwa Serikalini maisha yangu yote toka nimealiza chuo, nimefanya kazi Serikalini na Mheshimiwa Jafo ametoka kuzungumza hapa ni Mjumbe mwenzangu kwenye Kamati hii na uzuri Mheshimiwa Jafo pia nimefanyanae kazi nikiwa kama Mkuu wa Wilaya ya Kisarawe miaka hiyo ya nyuma kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme kwa dhati ya moyo wangu Jeshi letu la Wananchi kwa kiwango kikubwa tungeweza kusema katika bajeti hii Wabunge wote kwa uzalendo ambao Jeshi letu limeendelea kuonesha kwa nchi yetu ninaweza nikasema kabisa na wanajeshi wote wanaotusikiliza sisi Wabunge na viongozi wa Jeshi wote walioko hapa wakiongozwa na Waziri

19 MEI, 2026

wetu kaka yangu mnyenyekevu sana ambaye fungu hili pia linamuhusu, kitendo cha kuona Wabunge, Bunge hili wanawasemea vizuri wanajeshi ni kwa sababu kubwa moja na ninaomba m-note na siku mkiondoka kwenye misingi hiyo mnaweza msizone sauti za Wabunge na Watanzania wakionesha mapenzi mema kwa Jeshi la Wananchi wa Tanzania. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nataka niwaambie mimi ni Mjumbe wa Kamati hii ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama. Nimemfahamu Waziri huyu Mheshimiwa Dkt. Nyansaho toka akiwa mtumishi wa umma pale Benki ya Azania, nataka tuweke rekodi sawa na fungu la unyenyevu nililolisoma linabeba maudhui ya Waziri wetu huyu wa Ulinzi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kuna jambo ambalo Mungu analithamini sana katika *leadership* ya mwanadamu, cha kwanza Mungu anachokithamini sana kwa binadamu *it's humbleness*, unyenyekevu na unyenyekevu huu wa Waziri wetu ameurithi kutoka kwa unyenyevu wa Amiri Jeshi Mkuu, Rais Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamsema Waziri huyu utakumbuka mimi nimefanya kazi katika shirika la umma linaitwa *Fair Competition Commission* nikiwa kama *inspector*, lakini nikiwa kama *Senior Human Resource Officer*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nikwambie wakati nafanya kazi *Fair Competition* nilifanya kazi kwa karibu na Mheshimiwa Dkt. Nyansaho, Waziri huyu alipokwenda pale TANESCO kama Mwenyekiti wa Bodi nchi yetu ilikuwa inapita katika misukosuko mingi sana ya kukatika umeme, nenda-rudi, lakini kwa unyenyevu wake aliacha alama, akaondoka ameacha alama, Taifa letu likawa limetulia. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Rais wetu amempa heshima Waziri huyu amekuja kwenye Wizara hii ya Ulinzi tunaona utulivu, nidhamu ya Jeshi letu vikiendelea kushamiri katika Taifa letu. Mheshimiwa Waziri, mimi kaka yako na mpakwa mafuta wa bwana ninakutia moyo, endelea na unyenyevu huo kwa sababu

19 MEI, 2026

ahadi ya unyenyekevu iko katika neno la bwana ambalo nimekusomea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nilitie moyo Jeshi letu la Wananchi wa Tanzania katika bajeti hii sisi tumepita tumeangalia miradi. Kwanza kabisa nataka niwaambie Mkuu wa Majeshi nafikiri uko hapa ndani, wewe na Katibu wako Mkuu kaka yangu ambaye ametajwa kwa sifa nyingi na majenerali wote walioko hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti nataka nikwambie uzalendo wa Jeshi letu katika kulinda tunu za amani na kulinda Katiba unawafanya Watanzania waendeleo kulipenda Jeshi hili na kulisemea bila aibu mahali popote. Ninataka nikwambie nidhamu iliyooneshwa na Jeshi letu la Wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taifa letu lilipokuwa linapita katika nyakati ngumu, Taifa letu wakati linapita katika nyakati za kujaribiwa, kitendo cha Jeshi la Wananchi wa Tanzania kusimama katika kutii mamlaka ya nchi na kulinda mipaka na uhuru wa Taifa letu sisi Wabunge tuliotumwa na wananchi kuja katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa dhati ya moyo wetu tunasema nembo ya Uhuru wa Taifa letu ni uadilifu ni pamoja na uadilifu wa kazi za Jeshi la Wananchi wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jenerali Mkunda na majenerali wako wote, kwa niaba ya Wabunge wenzangu na Wajumbe wa Kamati ambao sisi tunawasimamia kwa dhati ya moyo wangu Mungu wa Isaka, Ibrahim na Yacobo aendeleo kuwaimarisha muendeleo kulinda tunu za amani, mshikamano na umoja wa Taifa letu, kwa sababu ninyi mmekuwa chachu ya kukataa chokocho za mapandikizi yote ambazo zinataka kuvuruga umoja, amani na mshikamo wa Taifa langu Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatambua hata Rais Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan alipokuwa akiwahutubia nilisikiliza hotuba zake nyingi aliendeleo kulisisitiza jeshi letu muendeleo kulinda nidhamu ya hali ya juu, kwa sababu toka historia ya Taifa hili lilivyopata uhuru, mataifa mawili yalipoungana nchi yetu

19 MEI, 2026

imeendelea kuamini katika mambo ya kwamba uongozi wa Taifa letu ukishapewa ridhaa, hakuna kuangalia mipaka huyu ametoka Ruvuma, huyu ametoka Zanzibar, huyu ametoka Bara, Taifa hili ni moja, kila kiongozi anapopata ridhaa ya kuongoza Taifa hili, sisi kama Watanzania tunajukumu na wajibu wa kumuunga mkono, ndivyo mlivyofanya Jeshi la Wananchi wa Tanzania, Mungu awabariki sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi kwa sababu bajeti hii sina mengi ya kusema, neno langu la mwisho ninalotaka kuwaomba, endeleeni kuwa wazalendo kwa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, endeleeni kuwa wazalendo kwa Amiri Jeshi Mkuu na Rais wetu, na endeleeni kulinda uhuru na mipaka ya Taifa letu. Sisi Wabunge tulioko hapa tutaendelea kuwasemea, tutaendelea kuwaunga mkono, na tutaendelea kuwa mabalozi wenu wema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikibidi bajeti hii tuiptishe tu leo mchana, watu hawa wakaendeleo kujenga Taifa na kulinda uhuru wa Taifa letu. Ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako.

MHE. ELIBARIKI I. KINGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja kwa 100%. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako. Nilimtaja Mheshimiwa Christina Solomon Mndeme, ajiandae Mheshimiwa Ado Shaibu Ado, ajiandae Mheshimiwa Fadhili Ally Liwaka.

MHE. CHRISTINA S. MNDEME: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii niweze nami kutoa mchango wangu kwa Wizara hii ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehema, ambaye kwa uwezo wake ametuwezesha kuona leo, siku hii iitwayo leo.

19 MEI, 2026

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile ninachukua fursa hii kuwashukuru wanawake wa Mkoa wa Tabora ambao wameendelea kuniamini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya kipekee ninatoa pongezi nyingi kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu wa Majeshi yetu ya Ulinzi na Usalama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatoa pongezi nyingi kwa Waziri Mheshimiwa Dkt. Rhimo Nyansaho na Katibu Mkuu Dkt. Faraji Mnyepe na watumishi wote wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. *(Makofi)*

Vilevile, pongezi kwa Mkuu wa Majeshi Jenerali Jacob Mkunda na wasaidizi wake wote wakiwemo Mkuu wa Jeshi la Kujenga Taifa Meja Jenerali Rajabu Mabele na wasaidizi wake wote, wakiwemo Wakuu wa Taasisi za Mzinga, SUMA-JKT, Nyumbu na wakuu wa vikosi mbalimbali, makamanda na askari wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, ninawapongeza watumishi na makamanda wote wa Fungu 38, Fungu 39 pamoja na Fungu 57 la Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti na Waheshimiwa Wabunge, ni ukweli usiofichika jeshi letu linafanya kazi kubwa sana, sana, sana. Ninawiwa kuwashauri, kuwasihi na kuwashawishi. Kwa umoja wetu tuiptishe bajeti hii iliyowasilishwa katika Bunge hili Tukufu, ili kazi nzuri ya utekelezaji wa bajeti iliyofanywa na inayofanywa, sisi wote ni mashahidi, tunashuhudia kazi nzuri ambazo zinafanywa na Wizara hii na majeshi yetu na makamanda wetu. Kazi hizi ziendeele kufanyika katika nchi yetu, kwani ulinzi ndiyo kichocheo cha ukuaji wa uchumi, ulinzi ndiyo kichocheo pia cha shughuli za kijamii, lakini ulinzi ndiyo kichocheo cha kufikia malengo ya Dira yetu ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2050. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania kwa kipindi kirefu imekuwa ni kisima cha amani na utulivu, Afrika na dunia, hii ni kwa

19 MEI, 2026

sababu ya kazi nzuri inayofanywa na Majeshi yetu ya Ulinzi na Usalama nchini. Kuna watu wanakesha sisi tunalala, tunapata usingizi mnono. Kuna watu wanafanya kazi kubwa za kulinda mipaka yetu ya nchi kavu, ya anga na majini ili Taifa letu liendeleo kuwa salama. Tunalipongeza sana jeshi letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kazi kubwa ambazo zinafanywa na Jeshi letu na bidii, na nidhamu, na uhodari walionao wanajeshi wetu, sisi tumeshuhudia miradi ikitekelezwa kwa vizuri sana. Miradi ambayo tumetembelea sisi Wanakamati nikiwa ni sehemu ya Kamati, ninaunga mkono taarifa yote iliyotolewa na Mwenyekiti wetu wa Kamati. Kazi nzuri tumeziona zikitekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Hospitali yetu ya Shirika la Mzinga iliyopo Morogoro, nami ninatumia nafasi hii kuwaambia wananchi waitumie hospitali hii. Serikali imewekeza fedha nyingi ili kuboresha huduma katika hospitali hii iliyopo pale Mzinga, Morogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watumishi waliopo pale wanafanya kazi nyingi kwa weledi, kwa kujituma, na kwa nidhamu ya hali ya juu. Hatuna shaka na Jeshi letu, hatuna shaka na watumishi wote wa Wizara, hatuna shaka na makamanda wetu. Tuna kila sababu ya kuipitisha bajeti hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kazi nzuri inayofanywa na Majeshi yetu na askari wetu, tunaishauri Serikali na tunaipongeza Serikali kwa juhudi zake za kuendelea kutoa kipaumbele kwa bajeti kwa Wizara hii kwa kutenga na kuhakikisha fedha zilizotengwa zinapatikana ili kuendelea kuboresha ufanisi na utendaji wa Wizara na kuimarisha ulinzi na usalama wa mipaka yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashauri tu kwa uchache yafuatayo; kwanza, tunaiomba Serikali iendeleo kutoa fedha. Upatikanaji wa fedha za maendeleo ukifanyika kwa wakati na kwa viwango husika, na kwa stahiki ambazo zinahitajika, kwani mchango mkubwa unaofikiwa, unaofanywa na Jeshi letu ni

19 MEI, 2026

mkubwa. Tunaiomba Serikali yetu iendelee kutoa fedha za maendeleo jinsi ambavyo zinavyohitajika na kwa wakati na kwa muda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, kuongezwa kwa fursa za vijana wa kujiunga na mafunzo ya JKT. Tunahitaji vijana wetu wengi waendeleo kupata mafunzo ya ukakamavu, wapate kuwajengea umoja wa Kitaifa, lakini wapate stadi za maisha na kazi ambazo zitawasaidia kujijiri wanapomaliza mafunzo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ulipaji wa fidia kwa maeneo yaliyotwaliwa na jeshi ufanyike kwa uharaka bila ucheleweshaji. Ninachukua fursa hii kuishukuru Serikali ambayo kwa namna ya pekee imeweza kulipa fidia wananchi wa Mbogwe waliopo Nzega Mkoa wa Tabora, jumla ya shilingi 4,869,631,375. Jumla ya wananchi 989 wameweza kulipwa fidia zao. Hongera sana kwa Wizara yetu ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri mwingine, pale inapowezekana, vijana wetu waendeleo kupewa mafunzo ya kutengeneza teknolojia ya vifaa vya nishati safi, ikiwemo mitambo ya biogas, majiko banifu, majiko ya umeme na gesi ili yaweze kutumika nchini na kulinda mazingira yetu, kuinua uchumi na kulinda afya za watumiaji. Ni wakati sahihi sasa vijana wetu tunapoenda kutekeleza ajenda ya nishati safi ya kupikia, vijana wetu wafundishwe teknolojia hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumaliza ninaendelea kulipongeza jeshi letu na tunaendelea kuwatia moyo askari wetu na tunawaomba kwa Mwenyezi Mungu aendeleo kuwatunza na kuwalinda. Aendeleo kuibariki nchi yetu ikiongozwa na Amiri Jeshi Mkuu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja na ahsanteni kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

19 MEI, 2026

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako. Sasa ninampisha Mheshimiwa Spika aweze kuendelea. *(Makofi)*

Hapa Spika (Mhe. Mussa Azzan Zungu) Alikalia Kiti

SPIKA: Mheshimiwa Fadhili Ally Liwaka.

MHE. FADHILI A. LIWAKA: Mheshimiwa Spika, na mimi ninaungana na Wabunge wenzangu kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa rehema kubwa hii ya uzima, lakini ninatumia fursa hii adhimu sana kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Spika, leo tuko hapa kama Taifa tukiwa na matumaini makubwa wakati ambapo Bunge letu linakwenda kupitisha bajeti hii ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

Mheshimiwa Spika, niruhusu kwa unyenyekevu mkubwa sana na heshima kubwa, kumpongeza sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ambaye ndiyo amekuwa askari wa mstari wa mbele mwenye kupambania, kuyaishi, kuyainua na kuyahuisha maisha yetu Watanzania kwenye eneo hili la ulinzi na usalama, hususan katika eneo la majeshi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wewe utakuwa shuhuda na Wabunge wenzangu watakubaliana nami kwamba Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan amekuwa na kipaumbele kisichotia shaka juu ya usimamizi wa ulinzi katika maeneo ya mipaka na jamii zetu zinazozunguka. Amekuwa akitumia sera na maono yake katika kuhakikisha kwamba tunakuwa na Jeshi imara lililojikita katika masuala yenye ubobezi kwenye eneo la ulinzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba uniruhusu pia nimpongeze sana kaka yangu na ndugu yangu Waziri wa Ulinzi, Mheshimiwa Dkt. Rhimo Nyansaho kwa kazi kubwa ambayo anaifanya na hapa ametoka kuzungumza Mheshimiwa Kingu kwamba sambamba na kubeba jukumu zito la kuihudumia Wizara hii, lakini bado amebeba sura na taswira inayoakisi namna ambavyo

19 MEI, 2026

kiongozi anayesimamia vyombo vya ulinzi anavyopaswa kuwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na amefika mbali akachukua maandiko yaliyobeba unyenyekevu ndani yake na kubeba nia ya mtu sahihi anayepaswa kuwapigania na kuwapambania wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Dkt. Nyansaho si mgeni kwetu, kwa sisi vijana wa rika yetu tumemsoma sana alipokuwa *PSSSF*, tumemsoma alipokuwa Azania, tumemsoma alipokuwa *TIC*, lakini tumemsoma alipokuwa *TANESCO* alipofanya kazi kubwa ya kurudisha matumaini kwenye eneo la umeme, na leo hii sishangai, sipati bumbuwazi nikimwona akiwa anatekeleza wajibu wake vizuri kwenye eneo hili nyeti na uti wa mgongo wa Taifa letu katika nyanja zote za kiuchumi, jamii na suala zima la kiusalama lenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, toka Jeshi letu limeundwa tangu kuvunjwawunjwa kwa jeshi la wakoloni na nchi yetu kupata uhuru na kuamua kujisimamia wenyewe na kuunda Jeshi la Wananchi wa Tanzania, jeshi hili halijawahi kutuanguka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama yako mataifa duniani yanaweza kufikia mwisho wa dunia, yakawekwa mbele ya hukumu, yakaulizwa tuambieni katika nchi na ardhi niliyowapa, mbele za Mungu, nini mliwahi kujivunia? Ukiacha ardhi, ukiacha maji, ukiacha uoto wa asili na mimea tuliyopewa pamoja na wanyama, jambo pekee tunalojivunia Watanzania ni kuwa na Jeshi imara, lenye nguvu, uzalendo na uwezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika namna ya kibinadamu unaweza ukajiliza, je, kama mimi nisingezaliwa Tanzania, neno amani na utulivu unaojengwa na jeshi imara ningeweza kuuona wapi?

Mheshimiwa Spika, ninataka nikiri mbele ya Bunge lako Tukufu kuwa, sisi Watanzania, sisi Wabunge, kama vile jeshi linavyotulinda kwa silaha, kwa akili na maarifa, ndivyo sisi

19 MEI, 2026

wananchi na Wabunge tunavyowalinda wao kwa maombi, imani na maarifa yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jeshi letu limefanya kazi kubwa sana, limepambana katika maeneo ya ndani na nje ya nchi. Limejenga hehsima katika diplomasia ya Ulinzi, limejenga heshima katika uzalishaji mali, limejenga heshima katika masuala ya usalama. Kwa unyenyekevu mkubwa sana na heshima, ninaomba niwapongeze sana wasimamizi wa vyombo hivi. Ninampongeza sana Afande CDF Jacob Mkunda kwa kazi kubwa ya usimamizi anayoifanya na utulivu alioutengeneza kwenye jeshi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia ninampongeza Jenerali wa JKT kwa kazi kubwa anayoifanya ya ku-recruit vijana wetu, kuwatengeneza, hatimaye leo tunapoliona Jeshi la Tanzania tunaiona JKT iliyoandaliwa vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa, mimi nina maeneo machache sana ya kuweza kuchangia na kutengeneza ushauri wangu. Eneo la kwanza, ukiachana na shughuli za ulinzi wa mipaka, uzalishaji mali, lakini sisi sote tutakuwa mashahidi, tumeliona jeshi letu likishiriki katika masuala ya kijamii, masuala ya kuokoa, masuala ya kutengeneza *comfort* kwa watu na masuala yote yanayohusu majanga.

Mheshimiwa Spika, jeshi hili limefanya kazi kubwa pale Hanang, ndugu zangu wa Hanang watakuwa mashahidi namna jeshi lilivyofanya kazi yake vizuri. Jeshi hili limefanya kazi kubwa tulipopata majanga Kariakoo, watu wote wanajua na tunafahamu. Jeshi hili limesimamia ujenzi pale Msomera kwa nguvu kubwa, uwezo mkubwa na weledi mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ndiyo kusema kwamba mashaka yetu juu ya matumizi ya maarifa ya kijeshi hayaishii kwenye medani ya vita. Bado tunayapeleka kwenye medani ya maisha ya kijamii. Sasa tuna maeneo mawili ambayo niliomba kuchangia.

19 MEI, 2026

Mheshimiwa Spika, jambo la kwanza ni juu ya vijana wa Tanzania ambao wanamaliza kidato cha sita. Kwa sasa utaratibu tulionao ni wa kuwachukua vijana waliomaliza kidato cha sita kwenda kujitolea kwa mujibu wa sheria, lakini tunawaacha vijana wengi sana huko mtaani. Kwa kadri tunavyoona uwezo wa jeshi na namna wanajeshi wanavyokuwa, basi ni ombi langu na ninaamini Serikali yangu sikivu itaweka bajeti ya kutosha kupitia Wizara ya Fedha, ili vijana wote wanaomaliza kidato cha sita wasiende kwa mafungu, waende wote wanapokuwa wamemaliza, ili tukajenge Taifa la wasomi wenye uzalendo, ili tukajenge wataalamu wenye kuijua nchi hii, ili tukajenge wataalamu wasomi watakaokuja kulipigania Taifa hili kwa jasho, damu na nyama yao yote. Hilo ni eneo langu la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo la pili, amezungumza vizuri Mheshimiwa Dkt. Jafo na nilimpenda aliposema jeshi letu limebeba heshima na matumaini. Kama kuna jambo la mwisho na ni tumaini kwa Watanzania, pale wanapomwona mwanajeshi kwenye jambo gumu, hapo wanakuwa wamemaliza matatizo yao yote.

Mheshimiwa Spika, wako wazee wetu wamepigana Vita vya Kagera, wako katika maeneo mbalimbali nchini. Wako kila wilaya na kila jimbo la Mbunge hapa. Ninaiomba sasa Wizara, ninashauri namna ya kufanyia kazi hili jambo.

Mheshimiwa Spika, kwenye kila wilaya kuna Kamati za Usalama, ninaomba tuwatumie Wakuu wa Wilaya waliopo na Wakuu wa Vikosi vya Mgambo walioko kule, kuwabaini wazee waliobakia ambao wamepigana kulipigania Taifa hili katika kuliokoa dhidi ya mashambulizi ya Idi Amin. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pale Kagera walifanya kazi kubwa sana. Sasa hawa wazee wanadai madai yao, na mimi sina mashaka Mheshimiwa Waziri katika jambo hili, tukilichukua vizuri tukaliweka kwenye utaratibu, wazee wetu hawa tutapata manufaa, tutajua namba yao na tutasaidia kuwaokoa sana. *(Makofi)*

19 MEI, 2026

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo ninaunga mkono hoja na ninashukuru sana kwa nafasi. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Zainab Issa Abdallah, ajiandae Mheshimiwa Ado, ajiandae mtoa hoja.

MHE. ZAINAB ABDALLAH ISSA: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii nami nichangie bajeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nami ninakushukuru kwa kunipa nafasi hii kuchangia bajeti ya Wizara ya Ulinzi. Ninachukua fursa hii kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uhai na uzima, lakini kwa namna ya kipekee kabisa ninachukua fursa hii kumpongeza na kumshukuru sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuimarisha ulinzi na usalama wa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya kipekee kabisa tunampongeza Mheshimiwa Rais, mwaka huu Februari kwa kuzindua Makao Makuu ya Usalama wa Taifa, kwa ajili ya kuhakikisha kwamba viongozi wetu na wafanyakazi na taasisi za Wizara hii wanakuwa na mazingira bora ya kiutendaji na ya kufanyia kazi kwa ufanisi. Tunampongeza sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa sababu mradi ule wa makao makuu umeweza kugharimu zaidi ya shilingi bilioni 120. Haya ni maendeleo makubwa sana ndani ya Wizara hii. Tunampongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya kipekee tunampongeza Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kutuamini vijana na kutupa nafasi za juu kabisa za uongozi wa Taifa letu. Leo tunashuhudia kwenye historia ya Wizara hii tumepata Waziri kijana, mnyenyekevu, mchapa kazi, Mheshimiwa Dkt. Rhimo Nyansaho ambaye huyu ni mbobezi na mzamivu wa masuala ya uchumi. Tunampongeza sana kwa kuaminiwa na Mheshimiwa Rais kuwa Mbunge, lakini pia kuwa Waziri wa Wizara hii ya Ulinzi. Hakika anaitendea haki Wizara hii. *(Makofi)*

19 MEI, 2026

Mheshimiwa Spika, mimi kama Mjumbe wa Kamati ninataka niwaambie Wabunge wenzangu, mara ya kwanza Mheshimiwa Waziri alipokuja kwenye Kamati alikuwa anaweza kuitafsiri Wizara hii kichwani mwake bila kusoma popote. Kwa hiyo, tumeona kabisa jicho la mama limemwona huyu kijana mwenzetu, mchapakazi, mnyenyekevu, na ninaamini kwa weledi aliokuwa nao, na kwa namna anavyoishi na watu, na uwezo wa kusikiliza na kupambanua mambo, hakika atafika mbali. Tunamwomba sana kwa Mwenyezi Mungu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunampongeza sana Katibu Mkuu wa Wizara hii, yeye ndiyo *encyclopedia* ya Wizara hii. Kijana mnyenyekevu, mchapakazi, kwa kweli anafanya kazi kubwa sana na kazi nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini kwa namna ya kipekee ninaomba tumpongeze sana Mkuu wa Majeshi yetu, CDF Jenerali Jacob John Mkunda pamoja na Kamandi zote za vikosi vyetu vya ulinzi na usalama kwa kazi kubwa na nzuri ambayo wanaendelea kuifanya kuhakikisha nchi yetu inaendelea kuwa salama.

Mheshimiwa Spika, pia bila ya kumsahau mnadhimu wa jeshi ndugu yetu luteni jenerali Salum Haji Othumani, wanafanya kazi kubwa na kazi nzuri sana kumsaidia CDF, tunakupongeza sana, lakini pia tunampongeza Mkuu wetu wa JKT, Meja Jenerali Rajabu Mabele pamoja na Mkuu wa SUMA-JKT wanafanya kazi kubwa na kazi nzuri sana, tunawapongezeni sana.

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizo tunaomba tuwatie moyo wanajeshi wote na vikosi vyote vya usalama, kwamba kazi wanayoifanya ya kulinda amani na usalama wa nchi yetu, sisi kama Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tunawapongeza sana na tunawatia moyo na tunathamini kwamba sisi muda tukiwa tunalala wao wapo macho kupambania usalama wa Taifa letu. Tunawapongezeni sana na Mwenyezi Mungu azidi kuwalinda na kuwabariki kwa kuendelea kuimarisha usalama wa Taifa letu. *(Makofi)*

19 MEI, 2026

Mheshimiwa Spika, mimi ninaomba nitume salamu kwa Wizara ya Fedha. Suala la amani halina *compromise*, tunaweza ku-*compromise* mambo mengine yote, lakini siyo suala la usalama wan chi yetu. Ninaomba sana Wizara ya Fedha itusaidie kwenye suala zima la kutoa bajeti ya kutosha kwenye Wizara hii ili Wizara hii waendeleo kufanya kazi kwa ufanisi wa hali ya juu sana. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa mfano Fungu 57 la Wizara, fedha ambazo zimetoka ni 43.6% lakini pia kwenye fedha za miradi ya maendeleo, kwenye fedha shilingi bilioni 318, fedha zilizotoka ni shilingi bilioni 110 sawa na 34.6%, lakini pia Shirika la Nyumbu fedha ambazo zimetoka ni 32%, Shirika la Mzinga fedha zilizotoka ni 33%.

Mheshimiwa Spika, tunaomba sana Wizara ya Fedha, kuhakikisha kwamba wanatoa fedha hizi ili taasisi hizi zilizopo chini ya Wizara ziweze kufanya kazi kwa ufanisi wa hali ya juu sana, kwa sababu bila ya kuwawezesha, maana yake tunawafanya wafanye kazi katika mazingira magumu ya kulinda amani na usalama wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, la pili, niipongeze sana JKT (Jeshi la Kujenga Taifa), wamefanya kazi kubwa na kazi nzuri sana na kupitia SUMA-JKT mwaka huu tumeona wametoa gaio la shilingi bilioni moja kwenye Mfuko wa Hazina, haya ni mafanikio makubwa sana na mimi niungane na Mbunge mwenzangu Mheshimiwa Fadhili Liwaka, kuwaomba sana waone uwezekano wa vijana wetu wanaohitimu kidato cha sita kuhakikisha kwamba hawa vijana wanapata fursa ya kwenda kupata mafunzo haya. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa sasa hivi *capacity* ya JKT wanauwezo wa kuchukua vijana 60,000 lakini vijana wanaohitimu kidato cha sita ni 125,000. Niiombe sana Wizara ya Fedha iwape ushirikiano wenzetu wa Wizara ya Ulinzi kupitia JKT, kwa sababu tunaandaa Taifa la kesho na bila kuwaandaa vijana ambao ni wazalendo, tutakuwa tunatwanga maji kwenye kinu, hatuwezi kupata matokeo tunayoyatarajia. Ninajua mpango wa Wizara ni

19 MEI, 2026

kuhakikisha mpaka ifikapo mwaka 2031 wanaweza kuwa na *capacity* ya vijana 120,000; lakini niwaombe Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha kupitia SUMA-JKT wauone uwezekano wa kimkakati kabisa kuwezesha hili shirika letu la SUMA-JKT kuweza kufanya miradi ya kimkakati.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi tunaona SUMA-JKT wanafanya shughuli za ulinzi kwenye makampuni mbalimbali na kwenye miradi ya kimkakati ikiwemo *SGR*, wanafanya kazi kubwa sana kwenye Bwawa la *Hydropower* la Mwalimu Julius Nyerere, wanafanya kazi nzuri sana kwenye miradi ya kimkakati. Tunaomba sana pamoja na hii kazi nzuri wanayoifanya kwenye ulinzi, lakini pia kwenye ujenzi wa miradi mbalimbali tuone uwezekano wa kutanua wigo kwenye sekta za kimkakati kwa mfano uwezekano wa kuwa na kongani za viwanda, lakini pia kwenye sekta ya madini ili tuendelee kulinda rasilimali za Taifa letu lakini kupitia wao tuweze kupata fedha zakuwezesha JKT iweze kuendesha mafunzo mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini tunatambua sasa hivi kupitia JKT kuna skimu mbalimbali za umwagiliaji kama pale Chita kuna skimu ya umwagiliaji. Pale Chita tuna hekari 12,000 lakini tuna kilimo cha umwagiliaji hekari 2,500. Niiombe sana Wizara ya Kilimo...

(hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Mheshimiwa muda wako umekwisha.

MHE. ZAINAB ABDALLAH ISSA: Mheshimiwa Spika, niiombe sana Wizara ya Kilimo iweze kuwa-*support* wenzetu...

SPIKA: Nikuombe ...

MHE. ZAINAB ABDALLAH ISSA: Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo ninaunga mkono hoja, ahsante sana.

SPIKA: Nikuombe baada ya hapa umuone Katibu Mkuu wa Wizara ya Ulinzi akupe mtiririko wa pesa zinavyoingia kwenye

19 MEI, 2026

Wizara hiyo. Kuna pesa nyingine haziingii kwenye vitabu vyenu. Umenielewa?

Nilimuacha Mheshimiwa Juma Mustafa badala ya yeye atakuja Mheshimiwa Ado, halafu mtoa hoja.

MHE. JUMA M. KAWAMBA: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa ninaanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye amejaalia asubuhi hii tumekutana hapa ukumbini Bungeni, lakini Mwenyezi Mungu huyo huyo ambaye amejaalia amani na utulivu ndani ya Taifa letu limeendelea kuimarika.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kumpongeza Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan na Amiri Jeshi Mkuu wa Taifa hili kwa juhudi zake ameendelea kuhakikisha Tanzania yetu amani na utulivu imeendelea kuimarika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninapenda kumpongeza Waziri wa Wizara hii na viongozi wote wa vyombo vya ulinzi na usalama ambao wanahakikisha mipaka yetu ya nchi imeendelea kuwa na amani na amani na utulivu wa nchi yetu umeendelea kuimarika.

Mheshimiwa Spika, sisi sote tunakubaliana hapa hakuna maendeleo bila amani na hakuna amani bila ya kuwa na jeshi imara. Jeshi letu limekuwa ni mfano wa kuigwa Afrika Mashariki na Kusini mwa Jangwa la Sahara kutokana na uwekezaji wa muda mrefu ambao umeendelea kufanywa ndani ya jeshi letu. Hii inatuonesha nini sisi kama Waheshimiwa Wabunge, inabidi tuendeleo kulipa ushirikiano jeshi letu ili liendeleo kukabiliana na changamoto za ulinzi na usalama za kisasa. Kwani changamoto za ulinzi na usalama za kisasa ni ugaidi, uhalifu wa kimitandao, uzaji wa haramu wa binadamu, lakini hii inatuonesha nini; sisi kama Wabunge inabidi tuendeleo kulipa *support* jeshi letu kwa kulisemea na kuishauri Serikali, ihakikishe bajeti tutakayoipitisha hapa, fedha hizi zinakuja kwa wakati, kusudi jeshi letu liendeleo kufanya kazi kwa weledi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio haya, lakini bado kuna changamoto mbalimbali ambazo tunatakiwa tuziangalie

19 MEI, 2026

ndani ya jeshi letu. Sisi kama Waheshimiwa Wabunge inabidi tuendelee kuiomba Serikali, iendelee kuboresha makazi ya askari wetu, maeneo ya kufanyia kazi, maeneo ya maisha yao maaskari wetu, lakini matibabu ya askari wetu pamoja na kununua dhana za kisasa za kijeshi. Kwa sababu tunafahamu bila kuiomba Serikali iongeze bajeti na bajeti itakayopangwa iletwe kwa wakati, isipoletwa wanajeshi wetu hawa hawawezi kufanya kazi kwa weledi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi ninaiomba Serikali bajeti hii ambayo tutaipitisha hapa siku ya leo Serikali ijitahidi bajeti yote ije kwa ajili ya kuweza kuimarisha weledi na ufanisi wa jeshi letu. Kuna Jeshi la Kujenga Taifa, jeshi hili ni jeshi ambalo linafundisha uzalendo, linafundisha nidhamu, lakini pia linawawezesha vijana kuweza kuwafundisha mbinu mbalimbali za kuweza kujitegemea.

Mheshimiwa Spika, mimi ninaiomba Serikali iongezee bajeti Wizara hii, kusudi tuweze kuwa-*accommodate* vijana wengi waweze kujiunga na jeshi hili. Ikiwa ni pamoja na kurekebisha makambi, kuweza kuongeza makambi yawe na uwezo mkubwa wa kuweza kuchukua vijana wengi na mimi vijana wangu wa Jimbo la Igalula wawe pamoja ambao watakaochukuliwa kwa wingi na kuweza kujiunga na Jeshi la Kujenga Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Jeshi hili la JKT tukilitumia vizuri linaweza likatusaidia kupunguza upungufu wa ajira kwa vijana...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Mheshimiwa Juma, muda wako umekwisha, ahsante.

MHE. JUMA M. KAWAMBA: Mheshimiwa Spika, ninaunga hoja kwa 100%, ahsante ninashukuru sana.

SPIKA: Ahsante.

Mheshimiwa Ado, jiandae mtoa hoja.

19 MEI, 2026

MHE. ADO S. ADO: Mheshimiwa Spika, awali ya yote niseme kwamba ninafahamu kwamba mjadala wa Wizara ya Ulinzi, siyo mjadala wa kawaida, ninafahamu. Ni mjadala nyeti wenye maslahi mapana kwa Taifa, kwa hiyo nitazungumza kwa ufupi na nitazungumza kwa mipaka inayohitajika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la kwanza jambo la kwanza ni juu ya maslahi ya maveterani wa vita ya Kagera. Kama inavyofahamika na nimesoma *Hansard* za Bunge lililopita katika mwaka wa fedha huu tulionao; Serikali ilitoa ahadi ndani ya Bunge kupitia Waziri aliyepita Dkt. Tax, kwamba kuanzia mwezi Julai maveterani wa vita ya Kagera ambao hawapati posho wataanza kulipwa rasmi posho na Serikali. Hiyo ilikuwa ni ahadi ya Serikali kwa mashujaa wetu...

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, ninaongeza muda mpaka tumalize kazi yetu. *(Makofi)*

MHE. ADO S. ADO: Mheshimiwa Spika, hiyo ilikuwa ni ahadi ya Serikali kwa wapiganaji wetu, ahadi ambayo inajenga msingi kwa wapiganaji wa sasa kwamba wakienda mstari wa mbele wakapambana, watapewa tuzo, watatazamwa. *(Makofi)*

Mimi jimboni kwangu wazee hawa wapo, wengi wao umri wao ni baina ya miaka 70 mpaka 90, vikongwe lakini taarifa nilizonazo wanasema hawajaanza kulipwa.

Mheshimiwa Spika, sasa mimi ninataka Waziri atakapokuja kwenye majumuisho kwa kweli ninasita sana kuzungumza lugha ya kushika shilingi ila aje atoe maelezo kwamba Serikali ahadi ile kwa maveterani wa vita ya Kagera ilikuwa ni siasa ya maneno matupu na tunaweza kufanya siasa kwenye Wizara ya Ulinzi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nina mapendekezo ya ziada, ninapendekeza ukiacha ahadi ile ya posho tufanye kama mtindo ambao baadhi ya nchi zinafanya, tuwe na mfuko maalum wa maveterani wa vita ya Kagera. Mimi ninapendekeza tuwe na mtindo kama wa *The Kagera War Veteran Fund* na nchi nyingine

19 MEI, 2026

wanafanya, Marekani wanafanya, Afrika ya Kusini wanafanya, Uingereza wanafanya kwa mtindo tofauti tofauti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili ninakubaliana na Mheshimiwa Liwaka kwamba ni lazima tufanye sensa sio sensa ya kubaini idadi yao tu, tuangalie na hali yao, wanaendeleaje wazee wetu hawa waliopigana katika vita ya Kagera.

Mheshimiwa Spika, la pili na la mwisho; Jeshi la Wananchi ni jeshi la ukombozi wa Afrika, ni Jeshi la haki. Haikuwa kwa bahati mbaya jeshi hili lilipokelewa Uganda kwa shangwe, haikuwa kwa bahati mbaya jeshi hili lilipokelewa Kariakoo kwa shangwe, haikuwa kwa bahati mbaya Oktoba kwa yale yaliyotokea jeshi hili lilipokelewa kwa shangwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninatoa changamoto kwa jeshi, kuna kitu kimoja wakilinde kwa nguvu zote, kitu hiko ndio roho ya thamani yao; jeshi lijitenge na siasa, hicho ndio kitu wakilinde kwa nguvu zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni vimekuwepo vidole na huwa wanasema kwa sababu jeshi bado ni chombo hata katika zama hizi ambazo tunasema utumishi wa umma umekuwa *politicized* bado imani ipo...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Mheshimiwa Ado, muda wako umekwisha. Aah! Mara mwisho utaanza kusema vitu nitakuuliza ushahidi utashindwa, kaa chini. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa mtoa hoja. *(Makofi)*

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA: Mheshimiwa Spika, kwanza ninaomba kutumia nafasi hii kukushukuru wewe binafsi, lakini pia kumshukuru Naibu Spika, pamoja na Wenyeviti wote watatu wa Bunge letu na ni imani yangu kwamba wote leo wamo humu ndani. *(Makofi)*

19 MEI, 2026

Mheshimiwa Spika, tunakushukuru wewe binafsi kwa kutupa heshima kama Wizara yetu ya Ulinzi na kuja kuongoza sasa hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii pia kuishukuru Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama. Wamekuwa ni watu wanaojua nini maana ya ulinzi na usalama ndani ya nchi yetu, lakini pia nitumie nafasi hii pia kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia, lakini na wale ambao hawajachangia. Kwa wale waliochangia wapo Waheshimiwa Wabunge saba, michango yao yote tumeichukua, lakini tumeichukua kwa ukamilifu na tutaifanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nijikite katika yale mambo ambayo yamejirudia ili niweze kutoa ufafanuzi; cha kwanza, nimshukuru ndugu yangu Mheshimiwa Ado, na nimekushukuru kwamba pamoja na ulivyozungumza kulingana na unapotoka, lakini umeamini kwamba tahadhari juu ya ulinzi ni nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hii ndio nchi ambayo tunapenda tuijenge, nchi ambayo tuna dini tofauti, nchi ambayo tuna vyama tofauti, lakini inapofika suala la ulinzi na usalama tunakuwa kitu kimoja. Kwa hiyo, ninakushukuru ndugu yangu Mheshimiwa Ado. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nijielekeze kutoa ufafanuzi juu ya maveterani wale wazee wetu waliopigana, wengine wamelala mauti, lakini wengine wapo hai wa vita ya Kagera. Cha kwanza, ni vyema Bunge lako Tukufu lijue kwamba Amiri Jeshi Mkuu kwa maana ya Mheshimiwa Rais, amewapa hawa maveterani wa Kagera heshima kubwa kwa sababu tangu walipomaliza vita ile, vita ya Kagera ilikuwa ina makundi matatu; kundi la kwanza lilikuwa ni wanajeshi waliokuwa jeshini, lakini kundi la pili ni watu kwa maana ya wenzetu ambao walijitoa wakasema kwa sababu tumevamiwa sasa tujitoe, wakaji-*mobilize* wenyewe hawana mafunzo ili waende kwa ajili ya kuikomboa nchi na kupambana na Nduli Idi Amin.

Mheshimiwa Spika, lakini kundi la tatu lilikuwa ni Jeshi la Akiba. Sasa katika hili baada ya vita ya Kagera, wale wazee wetu walivyorudi, vyombo vingine vya ulinzi na usalama vilitoa nafasi kwa watu kwenda kuajiriwa kwenye vile vyombo vingine tofauti na jeshi kwa sababu wapo walioenda kwa ajili ya lile zoezi tu la vita. Sasa wapo waliokosa sifa za kuajiriwa na vyombo vingine tofauti na jeshi kwa sababu wapo walioenda kwa ajili ya lile zoezi tu. Sasa wapo waliokosa sifa za kuajiriwa na vyombo vingine vya ulinzi na usalama kwa wakati ule kwa sababu walikuwa wamepata majeraha hawana sifa. Hawa ndio ambao sasa tunawazungumzia.

Mheshimiwa Spika, kwa huruma ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia, pamoja na kwamba wakati ule walilipwa kifutajasho shilingi 5,000 kwa wakati ule iliyokuwa inaitwa Ahsante Nyerere. Baada ya kulipwa, pamoja na mambo yote yaliyopita, Mheshimiwa Rais mwaka jana akatoa maelekezo kwetu sisi Wizara ya Ulinzi kwamba wale wazee wetu ambao waliipambania nchi sasa ni vizuri Wizara ikaangalia namna ili waingizwe kwenye daftari la pensheni. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, sasa mwezi Juni kuna taratibu kidogo zinatokea kwamba hili ilikuwa ni mwezi Juni, kwa hiyo lazima zile taratibu za kiserikali kutangaza liwe *gazetted* ili sisi kwenye Wizara ya Ulinzi tuweze kukaa kwenye halmashauri ya majeshi, tubadilishe baadhi ya vipengele ambavyo vitaruhusu sasa wale wazee wetu waweze kuingizwa kwenye daftari la kulipwa pensheni, kazi hiyo mpaka sasa ninavyozungumza tumeshaifanya na imeshakamilika. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kazi ya pili ilikuwa sasa ni namna ya kuwatambua wako wapi hawa. Kazi hii naomba Waheshimiwa Wabunge watatusaidia ili kwa namna moja au nyingine waweze kufikiwa kila mmoja. Tukawasiliana kupitia Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa sababu kila wilaya sisi tuna Mshauri wa Jeshi la Akiba au Mshauri wa Mgambo. Kupitia ofisi ya Mkuu wa Wilaya tumeshabatambua zaidi ya wazee wetu 7,800 tayari ambao sasa katika hawa tayari tumeshafanya ile *quantification* kwamba wanapaswa kulipwa ni hawa na tumeshapeleka majina haya

19 MEI, 2026

Hazina, Wizara ya Fedha, ili na wenyewe wafanye uhakiki na hawa wazee tayari waanze kulipwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, rai yangu mimi kwa Waheshimiwa Wabunge akiwemo na ndugu yangu Mheshimiwa Ado mtusaidie kutoka kwenye majimbo yenu. Sisi tutatoa maelekezo na ushauri kupitia Ofisi ya Rais, TAMISEMI, watusaidie sasa kutoa tangazo kwa wale ambao hawana taarifa rasmi...

SPIKA: Mheshimiwa Waziri, ni Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI.

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA: Mheshimiwa Spika, samahani, ni Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI.

Mheshimiwa Spika, watusaidie sasa kutoa tangazo kwa wale ambao hawajafikiwa ili waweze kufikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema hayo, naomba sasa nitoe pia ufafanuzi kwenye hoja ya pili ambayo imejirudia.

Mheshimiwa Spika, hoja ya pili ni namna ya vijana wetu wa kidato cha sita waweze kujiunga kwenye Jeshi la Kujenga Taifa. Kwanza ni nia ya dhati ya Serikali kwamba baada ya kufanya tafiti za kina, tukagundua kama nchi kwamba lipo jambo ambalo tunapaswa kulifanya ili kuhakikisha kwamba tunaongeza ukakamavu, uzalendo, lakini pia na uzalishaji mali kwa vijana wetu.

Mheshimiwa Spika, hapo nyuma kidogo kulikuwa kunakuwa na baadhi ya hata migomo kwenye vyuo vyetu. Sasa tukafanya utafiti na kugundua kwamba ipo haja ya kuwafunza hawa vijana wenzetu uzalendo na nini maana ya kulinda nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tangu Jeshi la Kujenga Taifa lilipoanza, takwimu zinaonyesha kwamba hata ndani ya vyuo vyetu vikuu ambavyo vina watu wa dini tofauti, vyama tofauti, hakuna migomo. Hili ni zao la mafunzo ambayo yanafanyika. *(Makofi)*

19 MEI, 2026

Kwa hiyo, baada ya hiyo Mheshimiwa Rais ameshatuelekeza kwamba nia yake ya dhati ni kuhakikisha kwamba vijana wote wanaomaliza kidato cha sita waweze kujiunga. Ie bajeti yetu ambayo sasa tunaendelea kuifanyia kazi mpaka sasa tuna uwezo wa kuchukua vijana 60,000 lakini tumeweka malengo yetu kama wizara kupitia JKT kwamba tuweze kuchukua vijana 140,000. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, sasa katika malengo yale tumeweka yale ya muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu. Malengo yetu yamewekwa kwamba kufikia mwaka 2031 tuwe tayari tuna uwezo wa kuchukua vijana wote wanaomaliza kidato cha sita, hilo ni lengo la kwanza na lengo. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, lengo la pili ambalo pia ni maelekezo ya Mheshimiwa Rais ni kwamba yale mafunzo ya miezi mitatu, bajeti ya Serikali ikiruhusu tutayaboresha siku za usoni ili yaweze kwenda zaidi ya miezi mitatu kama ilivyokuwa zamani. Hii inamaanisha nini, hii inamaanisha kwamba si kila kijana anayeenda kwenye Jeshi la Kujenga Taifa anaenda ili aajiriwe kwenye vyombo vya ulinzi na usalama, hapana.

Mheshimiwa Spika, tunawapeleka pale ili wakajifunze wengine namna ya kujitegemea na kutengeneza maisha yao kupitia uzalishaji mali. Kwa hiyo, tunaingiza mfumo ambao tutakuwa pia na sisi tunafanya *vocational training*. Hiyo itatusaidia na itasaidia hata Wizara yetu ya Vijana kupitia Ofisi ya Rais ili iweze kupitia Wizara yetu ya Ulinzi na sisi tuwe chanzo cha kufunda wale vijana na kuweza kupanua wigo wa ajira za kujitegemea.

Mheshimiwa Spika, kwenye hili, hayo ndiyo maelezo ambayo tuna uhakika kwamba utekelezaji unaendelea na mpaka sasa hata bajeti ya mwaka huu imeongezewa kwa ajili ya kuweza kutengeneza miundombinu wezeshi ya kuweza kuongeza vijana kwa mwaka ujao. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, tatu ambalo nilipenda pia nitolee ufafanuzi kidogo ni fidia. Ni kweli kwamba lazima nikiri michango

19 MEI, 2026

ya Waheshimiwa Wabunge na wale wenzetu wachangiaji wote. Sisi kama jeshi ni kweli kwamba tuna uhitaji wa baadhi ya maeneo ambayo yapo kimkakati. Yapo kimkakati ili kuweza kuimarisha ulinzi na usalama wa nchi yetu. Uzuri uliopo ni kwamba wananchi wetu ni waelewa sana. Jeshi linapoonesha nia ya kutaka eneo, wanakuwa wepesi sana wa kuweza kukubali kwamba sisi tunaweza tukapisha.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwenye yale maeneo yote ambayo tumeyafanyia uthamini, mpaka sasa tumeshazungumza na wenzetu wa Wizara ya Fedha na tumeshalipa zaidi ya shilingi bilioni 12 kwenye huu mwaka unaoishia wa 2025/2026. Lakini kwenye bajeti hii ya sasa tumetenga zaidi ya shilingi bilioni 30 ili tuweze kulipa zile fidia za haya maeneo yote ambayo tayari uthamini umeshakufanyika.

Mheshimiwa Spika, tuna imani kwamba maeneo yote ambayo yamefanyiwa uthamini, Serikali yetu kwa kushirikiana na wenzetu wa Wizara ya Fedha italipa zile fedha baada ya kuwa bajeti mpya imeanza kutekelezwa. Hivyo tunaomba Waheshimiwa Wabunge muelewe kwamba ukweli ni kwamba sisi ndio tunaopaswa kuzuia migogoro na wananchi waweze kuliheshimu jeshi, lakini pia waweze kuiheshimu Serikali yetu na kuhakikisha kwamba wanakuwa wao ndio walinzi namba moja wa kutoa taarifa za kiusalama na kuwa na mapenzi na nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho naomba niwashukuru sana ndugu zangu wa Wizara ya Ulinzi, nikianza na Katibu Mkuu Dkt. Faraji Mnyepe; pia Mkuu wetu wa Majeshi na Mnadhimu Mkuu wa Jeshi letu la JWTZ. Namshukuru pia ndugu yetu Mkuu wa JKT na Wakuu wa Kamandi wote ambao mmefika hapa, Wakuu wa Idara, Wakuu wa Mashirika yetu ya SUMA-JKT, Mzinga pamoja na Nyumbu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa niwashukuru ninyi Waheshimiwa Wabunge kwanza kwa imani kubwa ambayo mmeipa nchi yetu na mmempa Mheshimiwa Rais ya kuhakikisha kwamba Wizara yetu ya ulinzi inakuwa ni Wizara nyeti na hii

19 MEI, 2026

inamaanisha kwamba wote tunaelewa nini maana ya amani hata tuwe na malengo ya namna gani ya *Vision 2050*, kama hatuna usalama ndani ya nchi yetu, kama hatuna amani ndani ya nchi yetu, kama hatulindi mipaka yetu sisi wenyewe kwa ku-*identify* adui, hiyo kazi yote ambayo tunaipanga haitaweza kufikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, heshima mliyotupa sisi tutailinda na sisi tupo kwa ajili ya kutekeleza Ilani ya Chama Cha Mapinduzi, lakini pia na *Vision* yetu ya 2050 iweze kufikiwa jinsi inavyopaswa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Spika, naafiki. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante hoja imeungwa mkono.

Katibu.

NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE: Kamati ya Matumizi.

SPIKA: Kamati ya Matumizi.

KAMATI YA MATUMIZI

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Katibu.

NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:

KITABU CHA PILI

MATUMIZI YA KAWAIDA

Fungu 57 – Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa

Kifungu 1001- *Administration and Human*

19 MEI, 2026

Resources Management.....Sh. 29,038,233,400

MWENYEKITI: Katibu guillotine.

NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:

Fungu 57 – Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa

| | |
|---|---------------------------|
| Kifungu 1001- <i>Administration and Human Resources Management.....</i> | <i>Sh. 29,038,233,400</i> |
| Kifungu 1002 - <i>Finance and Accounts Unit.....</i> | <i>Sh. 381,970,000</i> |
| Kifungu 1003 - <i>Policy and Planning Division.....</i> | <i>Sh. 925,261,000</i> |
| Kifungu 1004 - <i>Internal Audit Unit.....</i> | <i>Sh. 385,577,000</i> |
| Kifungu 1005 - <i>Procurement Management Unit.....</i> | <i>Sh. 325,720,000</i> |
| Kifungu 1006 - <i>Legal Services Division.....</i> | <i>Sh. 585,277,200</i> |
| Kifungu 1007 - <i>Government Communication Unit.....</i> | <i>Sh. 274,760,200</i> |
| Kifungu 1008 - <i>Monitoring and Evaluation Unit.....</i> | <i>Sh. 287,392,800</i> |
| Kifungu 1009 - <i>Information and Communication Technology Unit.....</i> | <i>Sh. 32,708,391,600</i> |
| Kifungu 2001 - <i>Industries, Construction and Agriculture Division.....</i> | <i>Sh. 618,178,000</i> |
| Kifungu 2002 - <i>Military Research and Development Division.....</i> | <i>Sh. 1,537,139,400</i> |
| Kifungu 2004 - <i>Estate Management and Building Consulting Division.....</i> | <i>Sh. 691,059,000</i> |

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Fungu 38 – NGOME

| | |
|---|------------------------------|
| Kifungu 1001- <i>National Defence Headquarter (NDHQ).....</i> | <i>Sh. 3,157,737,843,000</i> |
| Kifungu 1006 - <i>Defence Forces Headquarter Command (DFHQC).....</i> | <i>Sh. 5,570,902,000</i> |
| Kifungu 1007- <i>Land Forces Command (LFC).....</i> | <i>Sh. 10,559,233,000</i> |
| Kifungu 1008- <i>Air Forces Command (AFC).....</i> | <i>Sh. 7,064,172,000</i> |
| Kifungu 1009- <i>Navy Command (NC).....</i> | <i>Sh. 4,412,698,000</i> |
| Kifungu 1010- <i>Military Hospitals (MH).....</i> | <i>Sh. 10,196,670,000</i> |

19 MEI, 2026

Kifungu 1011- Reserve Force Command (RFC).....Sh. 2,585,416,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi
bila mabadiliko yoyote)*

Fungu 39 – Jeshi la Kujenga Taifa (JKT)

Kifungu 1001- The National Service Force.....Sh. 626,273,760,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi
bila mabadiliko yoyote)*

NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:

KITABU CHA NNE

MIRADI YA MAENDELEO

Fungu 38 – NGOME

Kifungu 1001- National Defence Headquarter.....Sh. 54,867,636,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi
bila mabadiliko yoyote)*

Fungu 39 – Jeshi la Kujenga Taifa (JKT)

Kifungu 1001- The National Service Force.....Sh. 19,929,926,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi
bila mabadiliko yoyote)*

Fungu 57 – Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa

Kifungu 1003- Policy and Planning Division.....Sh. 350,000,000

Kifungu 1008 - Monitoring and Evaluation Unit.....Sh. 400,000,000

Kifungu 1009 - Information and Communication

Technology Unit.....Sh. 4,000,000,000

19 MEI, 2026

Kifungu 2001 - *Industries, Construction and
Agriculture Division*.....Sh. 48,086,301,560
Kifungu 2002 - *Military Research and
Development Division*.....Sh. 265,253,378,909
Kifungu 2004 – *Estate Management and
Building Consulting Division*.....Sh. 33,646,410,531

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi
bila mabadiliko yoyote)*

NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Matumizi imekamilisha kazi yake.

MWENYEKITI: Bunge linarejea.

(Bunge Lilirejea)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Mtoa Hoja.

T A A R I F A

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA: Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 126(3) ya Kanuni za Kudumu za Bunge za mwaka 2025 ninaomba kutoa taarifa kuwa Bunge lako limekaa kama kamati ya matumizi kujadili mpango wa makadirio ya matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka wa fedha 2026/2027 na limekamilisha kazi zake. Naomba taarifa ya kamati ya matumizi ikubaliwe na Bunge.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MAENDELEO YA VIJANA: Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa lamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

19 MEI, 2026

*(Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Wizara ya Ulinzi
na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha
2026/2027 Yalipitishwa na Bunge)*

SPIKA: Hoja imeungwa mkono. Mheshimiwa Ado ndiyo hukusema, siyo hukusema, umekaa tu. *(Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, kwanza nichukue nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Waziri na timu yake kwa kweli wamefanya kazi nzuri sana. Tunapongeza vyombo vyetu vinavyoongozwa na *CDF (Chief of Defence Forces)* na timu yake ya JKT, kwa kazi nzuri mmeifanya na mnastahili kupigiwa *salute*. *(Makofi)*

Watanzania sasa hivi hawajui nchi hii ilipotoka, na bila kujua historia ya Taifa lako au *culture* ya Taifa lako huwezi kuelewa Utanzania ni nini. Tunajidharau, lakini mataifa ya nje wanatupongeza kwa msimamo na kazi za kujitolea kwenye amani ya mataifa mengine. Nchi hii ya enzi za Mwalimu ndiyo iliyokomboa mataifa mengi ambayo yalikuwa chini ya mkoloni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, vita ya Kagera Amin hakuamini, alifikiri anafanya mchezo tu matokeo yake alikimbia Uganda akaenda kufanya kazi *Bureau de Change* Saudia kwa kazi iliyofanywa na vyombo vya nchi hii. *(Makofi)*

Tulivyoanza kutoa masharti kugharamia JKT hamjui haya na masharti yaliyowekwa na taasisi za pesa za kimataifa, Mwalimu alipewa masharti elimu bure mpaka chuo kikuu ondoa, afya ondoa, JKT ondoa na baya kabisa tukaambiwa tuisafirishe mafuta Tanzania. *Refinery* yetu iliambiwa isisafishe mafuta *simply* kupata mikopo, lakini tulisimama. *(Makofi)*

Tulisimama tulikuwa na Watanzania wazalendo lakini tukiwa na Jeshi la Wananchi ambalo lilikuwa lina uzalendo, hongereni sana makamanda wetu kwa kazi mnazofanya. *(Makofi)*

19 MEI, 2026

Mheshimiwa Spika, mpaka leo katika ukanda huu ndicho chombo kilichoaminiwa kusimamia amani kwenye mataifa mengine. Haya yanatokana na usimamizi wa viongozi waliopita kuanzia Mwalimu, Mzee Mwinyi, Mkapa, Kikwete, Magufuli na sasa tunaye Mama Samia. *(Makofi)*

Kwa hiyo Watanzania muwe *proud* kwani nchi kutambulika kimataifa. Tuendeleo kupendana, tuendeleo kushikamana, tuna Taifa moja tuna ndiyo maana juzi nimesikia kiongozi mmoja anakuja Tanzania kuwa balozi sitaki kumtaja, alikuwa anahojiwa nchini kwao na akasema *Tanzania is a strategic partner* kwa mambo mengi tu. *(Makofi)*

Walipotaka kujenga Bandari ya Bagamoyo hoja haikuwa biashara tu, hoja ilikuwa kusaidia vilevile nchi za Magharibi mwa Afrika kama Congo na maeneo mengine. Meli ikitoka Bandari ya Tanzania kwenda *West Coast* ya *DRC* ni siku 18 tu, kwa treni ni siku tatu, *that was the idea* lakini tumeikosa hiyo fursa kwa mipango ya Mungu. Tuendeleo kushikamana na tuimarike kiuchumi na jeshi hili limepewa kipaumbele na ndiyo maana mtu mwenye hoja, Mbunge, fursa yake ni kwenye Kamati, anakwenda kwenye Kamati, anajenga hoja yake na anajibiwa na vyombo viko pale na Mwenyekiti wa Kamati yupo pale, Wajumbe wa Kamati wapo pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *funding* za ziada za chombo hiki si lazima zitoke zisemwe hapa, tukisema hapa tutajivua nguo na mambo ulinzi hayataki masihara. Kwa hiyo Rais Samia yupo *very serious* na kuhakikisha vyombo hivi vinapata huduma zinazostahili. *(Makofi)*

Zipo changamoto, siyo kwetu tu, duniani kote hata majeshi haya makubwa, changamoto hazikosekani, *as long as* tunaishi changamoto zipo, lakini *where there is a challenge, that is where the way is*. *(Makofi)*

Ninawashukuru sana *CDF* na timu yako, *JKT* na wengine wote kwa uzalendo wenu na kazi kubwa mliyoifanya kwenye nchi yetu. *(Makofi)*

19 MEI, 2026

Mimi nilipata fursa ya kukaa kwenye Kamati hii kwa miaka 16 nilikuwa Makamu Mwenyekiti na kama *Mwenyekiti for all this time*. Tangu inaanza Bunge mimi niko kwenye kamati ya NUU, ilikuwa *Foreign, Defence and Home and Security*, kama Marekani kwa namna Kamati hii ilikuwa inafanya kazi na sasa ipo chini ya Mheshimiwa Najma wanafanya yale yale. Tujivunie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri, ninakushukuru sana umeleeza vizuri kuhusu fidia za haya majeshi na baadhi ya wale wa vita ya Kagera. Mimi nili-*participate* vita vya Kagera, nilikuwepo na nilipata medali mbili; ya kwanza kuwepo jeshini kipindi kile na ya pili kuvuka mpaka. *(Makofi)*

Sasa mimi sikuvuka mpaka kwa majeshi ya miguu, mimi nilivuka mpaka kwa juu kwa anga, yote kuvuka mipaka hiyo. Kwa hiyo Ado ukitaka mambo njoo nikwambie na Mwalimu alisema ninawapa *bonus*, nchi yetu bado maskini, lakini Mama Samia akasema hapana, ile mishahara ilikuwa ya miezi miwili, baada ya shule kuisha tukapewa mishahara wa miezi miwili kila mtu *cash and that time it was a lot of money*, ndiyo maana Rais Samia anasema tuwakumbuke maveterani wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri hongera sana na CDF hongera sana. Tunatunza wazee wetu walio *participate* kwenye vita chini ya maelekezo ya Mheshimiwa Rais. Sasa Mheshimiwa Ado na wewe una TV zako jioni unakuwa nje nje ukayaseme haya. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyosema Wabunge wenye hoja kwenye masuala ya Wizara ya Ulinzi muende kwenye Kamati ya Ulinzi mkaseme yote, shida zenu zote ili mpewe majibu.

Baada ya maneno haya, nawashukuru tena Wabunge kwa michango mizuri na ninaahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa 3.00 asubuhi. *(Makofi)*

*(Saa 7.24 Mchana Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Jumatano,
Tarehe 20 Mei, 2026 Saa Tatu Asubuhi)*